ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake

37.Mhe. Ashura Sharif Ali - Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Saba – Tarehe 27 Juni, 2011

(Kikao Kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASLISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:
Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Mkaridio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka fedha 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: Ahsante Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 111

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Kukosa Boti za Uokozi

Mhe. Ussi Jecha Simai - Aliuliza:-

Kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria Namba 7 ya mwaka 1999, Idara ya Zimamoto na Uokozi ndio yenye jukumu la kuzima moto na kuokoa maisha ya watu na mali zao Zanzibar. Jambo la kushangaza ni kwamba, Idara hii haina hata boti moja ya Uokozi hali ambayo inawaathiri kiutendaji kama ilivyotokea kuungua kwa meli ya M.V. Serengeti na kushindwa kuuzuia moto pamoja na kufika mapema lakini walikosa chombo cha kuwafikisha katika eneo la tukio kwa wakati.

(a) Je, ni lini Serikali itakipatia kikosi cha Zimamoto na Uokozi boti za uokozi za kisasa.

(b) Kwa kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu, Je, lawama na vilio vya wananchi kuhusiana na jambo hilo wazielekeze wapi, Serikali Kuu au Wizarani.

Mhe. Waziri Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 111 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe.Mwakilishi kuwa Sheria Nam. 7 ya mwaka 1999 imeipa jukumu la kuzima moto na uokozi Kikosi chetu cha Zimamoto na Uokozi.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaelewa jukumu hilo na jitihada maalum zimechukuliwa kukiimarisha Kikosi hicho kwa kuongeza vifaa na kuanzisha vituo vipya katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba. Ni kweli kuwa Kikosi cha Zima Moto na Uokozi hakina boti zakwe wenyewe za uokozi na kuzimia moto.

Hata hivyo, Kikosi hichi hufanya kazi kwa karibu sana na vikosi vyengine katika kukabiliana na maafa. Hivyo kwa hivi sasa yanapotokea majanga ya moto baharini Shirika la Bandari ambalo lina boti ya kuzimia moto na KMKM ambayo ina boti za uokozi hushirikiana kwa pamoja na Kikosi hichi katika kukabiliana na majanga.

Vile vile, serikali imeuona umuhimu wa kuwepo kwa boti ya kisasa kwa kikosi cha Zimamoto naahidi kuwa hili litashughulikiwa ipasavyo.

Mhe. Salum Amour Mtondoo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Naomba kumuuliza Mhe. Waziri Idara inauhusiano gani na wachimbavisima vya kienyeji, yaani visima vya makalbi ili kuwapa taaaluma kwa ajili ya usalama wao.

Mhe. Waziri Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, idara haina uhusiano moja kwa moja, isipokuwa serikali nafikiri imeshatoa maelezo mengi sana kutoka Shirika la ZAWA kwamba wanapotaka kuchimba visima basi wapate ruhusa maalum kutoka Idara hiyo ya maji kwa ajili ya usalama.

Kuna baadhi ya matokezeo ambapo visima kama hivyo vinavyochimbwa bila ya mpango maalum hutokea hatari. Wapiganaji wetu hawa wa Zimamoto wanaitwa kwenda kuokoa. Wameshafanya matukio kama haya mengi ya kwenda kuokoa watu, imetokea kwa bahati mbaya vimetubukia visima vyenyewe au watu wameingia. Yanapotoea matukio ndio hasa idara yetu inapoitwa. Ahsante.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza .

Kwa kuwa hiki kifungu cha Zimamoto na Uokozi kina jukumu la kufanya mambo yote mawili yakitokea. Wenzetu wanatumia moto uongo au uokozi uongo ili kuwazoesha wale Wazimamoto au waokozi. Je, Idara hii imeandaa mambo haya kwa mwaka mara ngapi au inatarajia kuandaa kitu gani wakati wa kuwazoesha wazimamoto hawa.

Mhe. Waziri Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kumepangwa maana yake yale ni matokeo ya kupangwa kwa makusudi masuala ya moto wa uongo. Lakini lile linafanywa makusudi kufanya wawe tayari kwa matokeo kama yake. Pia kuwapa mazoezi vikosi vyetu. Hayo yameshafanywa uwanja wa ndege. Na hivi karibuni sina hesabu kamili ya mwaka mzima vingapi.

Hili karibuni pia limefanyika zoezi kama hilo Bandarini. Hilo ni jambo la kawaida kama alivyosema kuwafanya watu wetu wajue nini wafanye yanapotokea masuala kama hayo. Ni suala zuri na tunazidi kuwaelimisha watu wetu na sisi tutazidi kufanya mambo kama hayo ya moto wa uongo ili kuwapa upeo watu wetu kufahamu nini hasa wafanye yanapotokea. Ahsante.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, Wizara ina mpango gani kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano kuondosha ujenzi holola ambao wakati wa maafa ya moto yanapotokea huwa ni usumbufu.

Mhe. Waziri Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, Idara yetu ya Zimamoto imekuwa ikiwasiliana kwa karibu zaidi na Wizara ya Ardhi, Makaazi kwa lengo kwamba washirikishwe kwenye majenzi yote, hata zile bodi za ujenzi mtu wetu awepo kwa sababu ya kuangalia michoro na usalama wa jengo kabla haya hayo majengo hayajajengwa.

Pia hata wizara nyengine kama ulivyosema Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu nayo tunaomba kwamba watushirikishe wakati wa mipango yao ya ujenzi wa barabara na mambo mengine.

Nafikiri utakubaliana na mimi kwamba kuna barabara nyingi mitaani utaona kuna njia zetu za maji ambazo zimewekwa kwa dharura inapotokezea wakati wa moto. Utakuta visaruji vile zimeandikwa *water horse*. Vile ni vya maji akiba au vya maji yanapotokezea madhara ya moto. Kwa hiyo nakubaliana na wazo lako kwamba ni vizuri Wizara hizi mbili zikaishirikisha idara yetu kikamilifu wakati wa upimaji wa viwanja hata wakati wa majenzi kwa ujumla.

Nam. 164

Utambuzi wa Mali za Serikali

Mhe. Omar Ali Shehe - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu Serikali ya Mapinduzi ilikosa utaratibu uliorasmi wa kuzitambua mali za Umma na hivyo kupelekea watu wachache waitumie fursa hiyo kujitwalia mali hizo kama vile Ardhi, Majengo, Samani, Vyombo vya Usafiri na kadhalika. Serikali ina mpango gani wa kuzitambua na kuziweka katika kumbukumbu mali hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 164 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli serikali ina mali nyingi ikiwa ni pamoja na ardhi, majengo, samani, vyombo vya usafiri na kadhalika. Kwa muda mrefu sasa mali za serikali hazijawekewa utaratibu mzuri wa kuziorodhesha pale zilipo pamoja na kufahamu thamani yake. Hata hivyo Mhe. Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuzifahamu na kuziwekea kumbukumbu mali za serikali. Serikali imeandaa mpango maalumu kama ifuatavyo:-

(a)Imeandaa madaftari matano

(1) Vyombo vya moto,
(2) Majengo,
(3) Mitambo na Mashine,
(4) samani na vifaa na
(5) Mashamba

Ambapo kila mkuu wa taasisi ya serikali atalazimika kuziorodhesha mali za serikali zilizo chini yake.

(b) Mali za serikali zitawekewa nambari maalum kwa lengo la kuzitambua kwa haraka zaidi.

(c) Kuzifanyia tathmini mali zote za serikali. Kwa kuwa eneo la tathmini lina gharama, tathmini hiyo itatupatia thamani ya mali itafanywa kwa awamu.

Mhe. Spika, lengo ni kuwa na orodha sahihi ya mali za serikali ambazo zitakuwa endelevu. Hata hivyo, kazi ya awali ya kuorodhesha mali za serikali inatarajia kukamilika tarehe 30 Juni, 2011.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri lakini.

(a) Ni ukweli kuwa kuna mali nyengine ambazo serikali hata haijui kuwa ni zake. Je, serikali itatumia mbinu gani kuweza kuzitafuta na kuzijua mali hizo.

(b) Kwa kuwa wamiliki wa mali hizo wanaendelea kuzitumia kwa muda mrefu, bila shaka kitu kinachotumiwa huwa kinapungua thamani yake. Je, serikali itakapozipata mali hizo itadai fidia kwa wanao miliki.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:

(a) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, kwanza tutaanza na taasisi za serikali ili kuona kwamba wote wanaorodhesha zile mali wanazozitumia. Lakini tukibaini kwamba bado kuna mali za serikali ambazo hazitumiwi na taasisi basi si vibaya tukatoa matangazo ili kuweza kuziorodhesha. Tutafanya hivyo na kila anaeelewa tunatoa nafasi hiyo kuweza kutoa taarifa ili tuweze kuziorodhesha.

(b) Mhe. Spika, kama kuna mtu anatumia mali za serikali na kama halipii kodi yoyote ile basi kwa busara kabisa tutaangalia uwezekano wa kuandaa malipo ili waweze kulipia pale ambapo tokea walipoanza kuzitumia. Hiyo itakuwa ni kufanya hivyo kwa sababu mali ya serikali ni mali ya taifa na fedha zinazopatikana zinatumika kwa maendeleo ya nchi yetu. Ni dhahiri kwamba tutaangalia uwezekano huo na hatutofanya kwa kumkomoa mtu lakini tutafanya kwa faida ya taifa letu na wananchi wetu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Nilikuwa nataka kujua ni utaratibu gani unaotumika kuhaulisha mali za serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza inategemea mali gani ambayo Mhe. Mwakilishi anayoizungumza, kama ni shamba kuna utaratibu kwa mujibu wa sheria za ardhi. Kama mali ni magari, kwa hivyo kuna utaratibu kwa mujibu wa sheria ya vyombo vya moto. Kuna sheria ambazo zinatakiwa zifuatwe katika kuhaulisha mali za serikali.

Nilivyomfahamu Mhe. Mwakilishi, kuhaulisha maana yake kuitoa katika mkono mmoja kuipeleka katika mkono mwengine.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

(a) Kwa kuwa katika kutayarisha daftari ya mali za serikali inaonekana hakuna fomula maalum, kuna wengine wanatumia daftari lakini wanatofautiana. Katika *particulars*, kuna wengine wanatumia compyuta, sasa ni utaratibu gani ambao waziri atatwambia ni mzuri zaidi katika kuhifadhi mali za serikali.

(b) Je, mashamba yale ya heka tatu tatu waliyogaiwa wananchi zile ni mali za serikali au ni mali ya waliogaiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:

(a) Mhe. Spika, nataka kumwambia Mheshimiwa katika utaratibu ambao tumeutoa kila Mkuu wa Taasisi kuorodhesha mali kama yeye ataorodhesha kwa kutumia kalamu, kwa kutumia chaki, kama ataorodhesha kwa kutumia compyuta, vyovyote anavyotaka, atuletee tu sisi orodha. Lakini sisi ile orodha ambayo atakayoniletea Wizara ya Fedha mimi nitaiweka kwenye *system* maalumu na ile ndio itakayokuwa orodha halali ya serikali. kwa hivyo kwetu sisi tutaiweka katika *system* ili tuweze kuitambua.

(b) Kwanza Mhe. Spika, nataka ifahamike kwa mujibu wa sheria iliyopitishwa na Baraza lako Tukufu kuwa ardhi ni mali ya serikali. Lakini shamba kama shamba yule aliyogaiwa anayo haki ya kulitumia kwa faida yake na familia yake.

Nam. 138

Tofauti ya *Scale* za Mishahara ya Walimu

Mhe. Rufai Said Rufai - Aliuliza:-

Katika nchi nyingi duniani uzoefu unaonyesha *'scale'* za mishahara ya walimu wanaofundisha Vyuo vya Ualimu ni tafauti na zile za Walimu wa Sekondari. Hapa Zanzibar *'Scale'* ya Mwalimu wa Chuo mwenye *Master*, mfano ni sawa na mwalimu wa Sekondari mwenye *Master*.

(a) Je, Wizara yako haioni kwamba ipo haja ya kuangalia upya muundo wa *'scale'* za mishahara ya walimu kwa vile kufundisha Vyuo ni kazi kubwa.

(b) Je, Wizara yako haioni kuwa suala hili linapelekea baadhi ya Walimu kuacha kufundisha katika Vyuo kwa kukosa motisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Alijibu:-

Mhe. Spika , kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 138 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:

Ni kweli kwamba katika baadhi ya nchi, ngazi za mishahara za wakufunzi wa vyuo vya ualimu hutofautiana na ngazi za mishahara za walimu wanaofundisha Skuli za Sekondari na Msingi. Tofauti hiyo inatokana na tofauti ya sifa za kielimu baina ya wakufunzi na walimu na hata muda wa kufanya kazi baina ya vyuo na skuli za sekondari ingawa sehemu zote mbili zina umuhimu wake na changamoto zake.

a) Wizara imeuona umuhimu wa kuangalia upya muundo wote wa utumishi wa walimu ili kufanya marekebisho ya mishahara ya wakufunzi na walimu.

b) Wizara haina taarifa rasmi ya kuwepo kwa wakufunzi wa vyuo vya ualimu walioacha kufundisha vyuoni mwao kwa sababu ya kuwa na ngazi ya mishahara yao inalingana na ngazi za mishahara ya walimu wa skuli za sekondari. Ahsante.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa utaratibu huu huwa unaanza skuli za msingi, sekondari na vyuo kwa walimu ambao wanauwezo zaidi ya wengine, hutegemewa kusomeshwa *primary* lakini anao uwezo akapangiwa asomeshe sekondari. Huwa anasomesha sekondari lakini uwezo wake akapangiwa kwenda vyuo. Je, wizara ina utaratibu gani wa wazi wa kuwaeleza walimu ambao wanapandishwa daraja hizi na viwango vyao vya mishahara au posho zao kwamba. zinaongezeka *automatically* akipata nafasi hii.

(b) Walimu hawa ambao wanasomesha vyuoni, ambao posho zao au mishahara yao haipandi kuna nafasi nyingi wanazozikosa na badala yake wanakimbilia Tanzania Bara. Je, Wizara ina mpango gani kwa kuweza kuwatia motisha walimu hawa ili kuweza kubaki hapa na kufundisha watoto wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali langu la mwanzo la msingi kuwa Wizara imeliona hilo na tunaangalia upya muundo wa utumishi. Kwa hivyo nadhani hilo suala la kwanza tayari ilikuwa tushalijibu.

Swali lake jengine Mhe. Spika, niseme ukweli ambao haufichiki kuwa tuna matatizo ya mishahara ikiwa kama ni vyuo, ni walimu wa skuli ya primary au ya sekondari, lakini hata watumishi wa serikali na taasisi mbali mbali.

Serikali kwa sababu imeliona hilo tatizo ndio maana katika bajeti hii ya mwaka 2011/2012 imetamka rasmi kwamba inafanya marekebisho ya mishahara.

Mhe. Spika, tatizo la mishahara si tatizo la Wizara ya Elimu tu hili ni Wizara zote. Bila shaka mishahara ambayo itarekebishwa itawavutia na kuwatia moyo wafanyakazi wetu ili waweze kulisaidia taifa lao. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, swali langu ni kwamba tatizo hili la mishahara halihusu tu vyuo vya walimu na skuli za kawaida, lakini pia hata Chuo Kikuu cha Serikali SUZA ambacho huwa kinaendeshwa kwa kupewa ruzuku na serikali.

Mhe. Spika, nilitaka anithibitishie tu je, katika marekebisho hayo ya mishahara pia yatajumuisha Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar ambacho wahadhiri wake wamekuwa wakilipwa chini sana ya viwango vinavyokubalika, kinyume na ahadi ambayo kuwa imetolewa hapo mwanzoni wakati chuo hichi kinaanzishwa, kiasi ambacho wahadhiri wengi sana wamekuwa wakikimbia na kusababisha kuanguka kwa hadhi ya elimu katika chuo kile.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, Chuo Kikuu cha SUZA nacho kimo katika marekebisho haya ya mishahara. Ijapokuwa tunajua kuwa hichi Chuo kina bodi yake ambayo inajiamulia mambo yake wenyewe. Lakini madhali kimo katika serikali basi kimo katika marekebisho haya ya mishahara.

Nam. 94

Madaktari Wanaotoroka Kazini Usiku Hospitali ya M/mmoja

Mhe. Mohammed Said Mohammed - Aliuliza:-

Hospitali ya Mnazi Mmoja inategemewa sana na wananchi wa Zanzibar wakiamini kwamba ndio Hospitali pekee ya Serikali yenye huduma na vipimo bora pamoja na wataalamu wenye ujuzi wa kutosha. Katika hospitali hiyo kumejitokeza baadhi ya madaktari wanaoingia zamu za usiku kutokaa kazini, badala yake huripoti kazini na kutia saini daftari la mahudhurio, kisha wanarudi nyumbani hadi alfajiri. Vitendo hivyo vinasababisha usumbufu mkubwa kwa wagonjwa wanaofikishwa hospitalini hapo.

(a) Je, hospitali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba madaktari wanaotakiwa kuwepo kazini wakati wa usiku wanakuwepo muda wote.

(b) Je, adhabu gani anapewa daktari aliyetakiwa kuwepo kazini usiku na badala yake hakuwepo.

(c) Wizara haioni kwamba ipo haja ya kutowa namba maalum za simu ili wananchi waweze kutoa taarifa za maovu wanayofanyiwa hospitalini hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 94 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, utaratibu maalum umepangwa kwa madaktari kuwepo kazini wakati wa usiku *(first on call)* kwa kila Idara za Hospitali hiyo. Kama kuna haja ikitokezea haja ya daktari bingwa *(second on call)* anafuatwa na gari la hospitali kwa kuja kutoa huduma.

Kesho yake asubuhi, kunakuwa na *morning meeting* ripoti zinatolewa za wagonjwa wote waliolazwa usiku na kama kuna tatizo linashughulikiwa hapo hapo.

(b) Mhe. Spika, endapo itabainika kuwa ushahidi na kuthibitisha kwa daktari kufanya kosa hilo basi hatua za kinidhamu za kiutumishi zitachukuliwa dhidi yake mara moja.

(c) Mhe. Spika, kimeanzishwa kitengo maalum cha mahusiano ambapo nambari za simu zimebandikwa kila wodi. Maafisa wanahusika ni kutoka *Quality Control Unit na Public Relation Officer* wapo kwa ajili ya kupokea taarifa hizo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Waziri huoni kwako ni busara kufanya ziara za mara kwa mara wakati wa usiku ili kubaini vitendo hivi.

b) Mhe. Naibu Waziri utakubaliana na mimi kuwa kulikuwa na chumba katika sehemu ya Mapinduzi Kongwe chenye kulala madaktari. Je, chumba kile kiko na kama hakiko kinatumika kwa matumizi gani hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ziara za mara kwa mara kama unavyopendekeza ni suala muafaka na baada ya matatizo yaliyojitokeza kuna utaratibu maalum tumeupanga na tutakuwa tunafanya hivyo. Nashukuru kwa kutunabahisha.

Kuhusu Chumba cha Mapinduzi Kongwe ambacho unasema kulikuwa kunalala madaktari, ni kwamba sasa hivi hakitumiki tena kwa sababu tumetayarisha vyumba viwili katika Mapinduzi Mpya na ndiko wanakolala madaktari. Kwa hivyo, madaktari wanaohusika wanalala pale katika Mapinduzi Mpya na cha Mapinduzi Kongwe kinatumika kwa shughuli nyengine.

Mhe. Salmini Awadh Salmini: Mhe. Spika, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi hii kumuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ni hospitali ya rufaa hapa kwetu Zanzibar na kwa kuwa Hospitali kama ya Al-Rahma inaweza kumudu kuweka madaktari wakati wa usiku wanakuwepo pale.

Je, Mhe. Spika, haoni Mhe. Naibu Waziri sasa ipo haja ya madaktari wetu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuweza kulala pale kama vile wanavyolala pale katika Hospitali ya Al-Rahma kuliko utaratibu uliopo sasa huu wa *on call.*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nimesema kuna madaktari wanalala Mapinduzi mpya na wapo hivi sasa huwa wanalala huko.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja fupi sana la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri alikiri

kwamba zinakwenda gari za hospitali kuwachukua wale *on call*, haoni iko haja ya kila daktari kupewa gari yake ili akaja daktari mwenyewe kuliko kumpigia simu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naona maombi yamekuwa makubwa kuliko uwezo wangu wa kujibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni jambo zuri kwamba kila daktari awe na gari yake, lakini utaratibu huo ni utaratibu unaohitaji mpango wa kukopeshwa gari hizo, hivi sasa uwezo wa kumpa kila daktari gari yake hatujawa nao pale mambo yatakaporuhusu tutafanya hivyo. Kwa sasa tunamuhudumia daktari kwa gari ambazo zinakuwa ziko maalum na wakati wowote huwa wanaletwa kuhudumia wagonjwa. Mhe. Spika, nadhani hili sio jambo jipya ni la maisha marefu kufanyika hivyo, nakushukuru Mhe. Spika.

Nam. 75

Kilimo Kwanza

Mhe. Shadya Moh'd Suleiman - Aliuliza:-

Sera ya taifa katika kukuza uchumi kupitia kilimo ni Kilimo Kwanza. Kwa kuwa wananchi wetu wengi hutegemea kilimo katika kujikwamua kimaisha lakini utaratibu wanaoutumia ni ule wa miaka ya nyuma tokea enzi za mababu zetu yaani hulima kwa kutumia jembe la mkono, huku wakikabiliwa na matatizo ya ukosefu wa dawa za kuulia magugu, mbolea na utaalamu.

(a) Mhe. Waziri, kwa utaratibu huu ni kweli tutaweza kuleta mapinduzi ya kilimo.

(b) Mhe. Waziri, unawaambia nini wakulima ili waweze kujenga matumaini ya baadae badala ya kulima kwa hasara.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 75 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili hivi sasa inatelekeza mpango wa mapinduzi ya kilimo kwa jina la mageuzi ya kilimo kwa Zanzibar. Katika mpango huu kilimo cha kisasa kinapewa mkazo kwa kutumia pembejeo ikiwemo mbolea, mbegu bora, dawa pamoja na huduma za matrekta.

Naomba kuwathibitishia Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa kwa kipindi cha mwaka 2009/2010, pembejeo kama mbolea, mbegu na dawa za kuulia magugu zilikuwepo za kutosha kiasi ambacho hazikumalizika kutumika na zikaendelea kutumiwa kwa msimu wa 2010/2011.

Mhe. Spika, msimu huu wa 2010/2011 tayari pembejeo hizo zimenunuliwa na kusambazwa vituo vyote vya kilimo. Kuwepo kwa pembejeo hizo na wataalam kuwa karibu na wakulima kunathibitishwa na wakulima wenyewe sambamba na kuongezeka kwa maeneo ya kilimo mabondeni na hivyo tunatarajia mavuno pia yataongezeka.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana Wajumbe wa Baraza lako ambao wametoa fedha kwa kuwanunulia wakulima wa majimbo yao pembejeo na kuwapatia huduma za matrekta. Hata hivyo, natoa agizo tu kwa kuwa nchi yetu ni visiwa na mazingira yake ni nyeti na maji yetu yanatoka ardhini, kwa hivyo matumizi ya madawa ya sumu lazima yafanywe kwa tahadhari kwa vipimo maalumu ili yasiharibu mazingira , na ndio maana dawa zinaagizwa kwa kiasi ya mahitaji tu na sio vyenginevyo.

Mhe. Spika, kuhusu matumizi ya jembe la mkono, naomba kutoa ufafanuzi kuhusiana na suala hili yapo maeneo ya mabonde ya mpunga huko Pemba matrekta hayawezi kufika na hivyo wakulima inawalazimu kutumia jembe la mkono. Aidha, matumizi ya zana za kisiasa kama matrkekta na *powertiller* yanatumika zaidi katika kilimo cha mpunga wa maeneo yaliyo tambarare na yenye kilimo mchanganyiko cha juu na maweni hata hivyo jembe la mkono litaendelea kutumika pale ambapo matrekta hayawezi kutumika.

Mhe. Spika, wizara yangu inaahidi wakulima kuwa kwa hatua za mageuzi ya kilimo zinazochukuliwa na Serikali, wawe na matumaini makubwa kuwa kilimo chetu kitabadilika na kuwa cha kisiasa na hatimae tutafikia lengo lililokusudiwa la kuongeza uzalishaji, kupunguza umasikini na kuongeza tija kwa wakulima.

Mhe. Spika, kauli mbiu kwa mageuzi ya kilimo ya nchi kwetu ni Mapinduzi ya Kilimo na si kilimo kwanza, kauli mbiu hii imebuniwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Moh,d Shein, ndio kauli mbiu aliyoitumia wakati wakiomba ridhaa ya wananchi na ndio kauli mbiu alizotumia na kuitolea ufafanuzi wa kina wakati wa uzinduzi wa Baraza lako hili na katika Sherehe za Mapinduzi na kuahidi wananchi wa Zanzibar kwamba atayasimamia Mapinduzi ya Kilimo kama ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inavyoelekeza.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri kwa sasa hivi umejibu suala zuri sana kwamba jembe la mkono ni jembe ambalo wananchi wanalitumia kwa mabavu. Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wa kuwatafutia wananchi hao hizi *powertiller* kwa njia ya mkopo wa nafuu.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa Zanzibar neno mapinduzi lina maana pana sana kwengineko maana yake hutofautiana na hapa kwetu. Zanzibar maana ya mapinduzi ni mageuzi ya haraka yaliyo endelevu na yenye tija na maslahi kwa walio wengi. Hiyo ndio maana ya mapinduzi kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wakati akitoa hotuba ya bajeti ya wizara yake alitoa ufafanuzi wa kina nini dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sekta ya kilimo.

Mhe. Spika, naomba niwathibitishie Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwamba mipango ya kuwawezesha wakulima wa nchi yetu pamoja na kuwapatia zana za kisasa za kilimo imeshaandaliwa na naweza kuthibitisha kwamba tunakwenda nalo vizuri na tayari tumeweza kupata *powertiller* 50 kutoka Serikali Iran tutaendelea kutafuta *powertiller*, matrekta na zana nyengine za kisasa. Hata hili wazo la kuwapatia wakulima wetu matrekta yao wenyewe hilo tayari limeshaanza kufanyika kupitia miradi ya *TASAF* na *PADEP* na tutaendelea kufanya hivyo wakati na nafasi itakaporuhusu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kuniona na mimi ili nipate kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na makusudio mazuri ya serikali kufanya mapinduzi ya kilimo katika nchi yetu, lakini katika mapinduzi hayo ya kilimo namuomba Mhe. Waziri ajue kama si mapinduzi ya kilimo katika mabonde ya mipunga tu, bali inastahiki kufanya mapinduzi ya kilimo kwa nchi nzima.

Mhe. Spika, kama atakubaliana na mimi jambo hilo kwani kuna maeneo ambayo ni ya Kanda ya Mashariki hayana mabonde ya kulima mipunga, lakini kuna sehemu za kulima vilimo ambavyo vinastawi katika nchi yetu tena vya aina nyingi. Mhe. Spika, wananchi wa Zanzibar kupitia hizo sehemu ambazo ziko kame kama vile Micheweni, Makunduchi, Kizimkazi na baadhi ya sehemu nyengine ambazo ni sehemu za mawe.

Je, pamoja na hayo amejiandaa vipi wizara yake kupitia wataalamu alionao wa kilimo kufanya utafiti au kuwafundisha wananchi wa maeneo hayo yenye ukame ili kulima vilimo vyengine ambavyo vinastawi kama vya biashara ili

wananchi wajipatie faida kwa kula na kuuza ili kupata fedha. Je, kupitia wizara yake imejiandaa vipi kuwasaidia wananchi wao kwa kuwapa elimu ili waweze kulima vilimo mbadala ambavyo vinaweza kutoa tija zaidi kwa serikali yetu pamoja na wananchi wenyewe.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana kwa suala hilo na niwathibitishie Wajumbe wa Baraza hili tukufu na wananchi wa Zanzibar kwamba hii sio wizara ya mpunga, wizara ninayoiongoza mimi ni Wizara ya Kilimo na Maliasili, tunaposema kilimo ni kilimo kwa upana wake na kwa maana yake hiyo.

Mhe. Spika, napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kama wizara yangu imejiandaa vizuri sana, sio kwa kilimo cha juu kwa maana cha maweni na maeneo ya makaani, lakini kilimo cha mboga mboga, kilimo cha viungo, kilimo cha mihogo, viazi vikuu, ndizi, viazi vitamu, uwele, mtama na kadhalika.

Mhe. Spika, hivi sasa tayari wakulima wetu wana mwelekeo mzuri kuelekea kwenye kilimo cha biashara, hayo mtayakuta Shehia ya Machui wanalima muhogo kwa wingi sana kwa kutumia mbegu za kisasa na kwa ajili ya biashara, mengine hayo mtayakuta Jimbo la Donge wanalima mananasi kwa wingi sana na kwa ajili ya biashara na maeneo mengineyo uliyoyataja.

Mhe. Spika, dhamira ya serikali kupitia programu zake mahsusi ambazo tayari zipo tutaona mengine kuona matunda yake mara moja katika msimu ujao wa kilimo, lakini mengine yatakuja kupitia programu zetu mbali mbali.

Mhe. Spika, sio hivyo tu bali tuna programu mahsusi za *microfinance* yakuweza kuanza kuwasaidia wakulima wetu fedha kwa maana ya kukopa bila ya kuwa na dhamana na kwa riba ndogo katika msimu ujao.

Mhe. Spika, hiyo ni hatua yetu ya mwanzo na maandalizi yetu kwa kweli yamepewa sifa pamoja na kuwa na sera ya *microfinance*. Ni hatua yetu ya mwanzo kuelekea katika Benki ya Wakulima kwa hiyo tumejipanga vizuri sana na naamini nitakapokuja kusoma hotuba ya bajeti ya wizara yangu tutatoa ufafanuzi mpana sana juu ya namna ya maandalizi ya wizara yangu ilivyo kwa sekta ya kilimo na sekta ya maliasili.

Nakushuru sana Mhe. Spika.

Nam. 21

Serikali Kuimarisha Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:-
Pamoja na jitihada inayochukuliwa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara (UUB) katika kushughulikia njia za ndani (*feeder roads*) wakiwezeshwa na mfuko wa barabara, jitihada hizo zinakwamishwa na upungufu uliopo wa zana na magari ya kubebea mizigo.

Je, wizara inachukua hatua gani za dharura kuziba pengo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu imeanza kutenga fedha kutoka mfuko wa barabara kwa ajili ya kufufua mitambo pamoja na magari ambayo yamelala kwa kukosa *"Spares"* pesa hizo hutolewa sambamba na matengenezo ya barabara husika zinazotekelezwa au iwe kwa kazi maalum ambayo itahitaji chombo hicho kutengenezwa. Hivyo, tatizo hilo litapunguza na kutoweka muda mfupi ujao kulingana na upatikanaji wa fedha za kufufulia vyombo hivyo,

Mhe. Spika, serikali kupitia fedha za msamaha wa madeni ilinunua magari manane makubwa ya kubebea mizigo ya (*IVECO*), *buldozer* moja, gari la kubebea maji moja, gari la kubebea mafuta moja pamoja na vifaa vyengine vya matengenezo ya mitambo. Aidha, katika utekelezaji wa mradi wa barabara za vijijini Kusini Pemba, Serikali imeweza kununua magari mengine mawili aina ha hino mapya, magari madogo manne, *motor grader* mbili mpya, pamoja na vifaa vingine vya kufanikisha ujenzi na matengenezo ya barabara.

Mhe. Spika, kwa kupitia mfuko wa barabara tumekuwa tukipata fedha kwa ajili ya ununuzi wa vipuri kwa malengo ya kufufua magari, mitambo na vifaa vilivyolala. Ni mategemeo yetu kuwa tukiweza kuvitunza vizuri vifaa vilivyopo na kutatua tatizo la vifaa vitakuwa vimepungua sana na halitokuwa kikwazo katika utekelezaji wa shuhguli zetu za kazi za kila siku.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza. Mhe. Spika, mara nyingi njia zetu za ndani zinapotiwa fusi na Idara hii ya UUB Pemba *roller* huwa haipiti na baada ya muda mfupi fusi lile huwa linakokotwa na maji linakwenda zake. Kwa marekebisho haya wanayoyafanya Mhe. Naibu

Waziri anatuhakikishia Baraza hili kwamba kuanzia bajeti hii inayokuja kila panapotiwa fusi na wao *roller* itapita ili barabara zetu ziwe madhubutu na ziweze kuhimili mvua.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu mama kwa kupitia mfuko wa barabara tunaendelea kupata fedha kwa ununuzi wa vifaa, napenda nimthibitishie Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kwamba vifaa hivyo vikipatikana tutaendelea kuboresha utengenezaji wa barabara hizo za feeder road na tutahakikisha kwamba huo usumbufu uliopo na matengenezo katika barabara hiyo unaondoka.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri kule Kitope kuna njia inayotoka Kitope na Kinduni na kwa kuwa huko nyuma iliwahi kupewa msaada na Mfuko wa Baraza lakini pesa hizo zikawa kidogo hazikuweza kukidhi haja ya kumaliza barabara ile. Je, Mhe. Waziri una mpango gani wizara yako kuimaliza barabara ile ili wananchi wakaondokana na usumbufu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, utaratibu wa Mfuko wa Barabara si aghlabu kuanza kujenga barabara upya, lakini kwa kuwa barabara hiyo ya Kitope kuelekea Kinduni imeshaanzwa kujengwa namthibitishia kwamba tutaendelea kuzungumza na Mfuko wa Barabara wakitusaidia fedha tutaijenga.

Nam. 67

TVZ na STZ Kuingia Katika *Digital*

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Kwa kuwa upatikanaji wa habari na taarifa sahihi na kwa wakati ni muhimu katika kufikia maendeleo ya kweli katika jamii. Na kwa kuwa wananchi wa Zanzibar wanapendelea kuona dhana hiyo inatimia haraka. Na kwa kuwa Serikali katika mwaka huu wa fedha imelenga kuimarisha uwezo wa Televisheni ya Zanzibar (TVZ) na Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) katika kutumia teknolojia ya kisasa ya digital kwa kununua vifaa vinavyotumia teknolojia hiyo.

(a) Je, Mhe. Waziri, ni lini malengo hayo yatatimia.
(b) Je, Serikali itasaidia vipi Shirika la Magazeti la Serikali kununua mtambo wa rangi wa uchapishaji ili waweze kuchapisha magazeti yao hapa hapa nchini badala ya kupeleka Tanzania Bara ambapo ni gharama kubwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 67 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imelenga kuimarisha uwezo wa TVZ na STZ katika mwaka huu wa fedha ili kuviwezesha vyombo hivi kununua vifaa vinavyotumia teknolojia ya *digital*. Kinachoendelea hivi sasa ni kuvipa uwezo vyombo hivi wa kuwa na vifaa vya kazi vya kisasa katika studio pamoja na kuweka miundombinu ya mitambo ya *digital*. Hatua itakayofuata ni kuwatayarisha wananchi kwa kuwapatia ving'amuzi ili waweze kupokea matangazo kwa njia hiyo mpya ya *digital*.

Mhe. Spika, nchi za Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania zimejpangia kuanza kurusha matangazo kwa mfumo wa *digital* kuanzia mwaka 2012 kwa lengo la kujiweka sawa na matatizo yoyote yale pindipo yakitokea. Hiki ni kama kipindi cha mpito hadi mwaka 2015 ambapo nchi zote wanachama wa ITU – Shirika la Mawasiliano la Kimataifa (Tanzania ni mwanachama) zitalazimika kuachana kabisa na urushaji wa TV kwa njia ya *analog* na badala yake kutumia mfumo huo mpya wa *digital*.

(b) Mhe. Spika, wizara yangu imelipa umuhimu mkubwa suala la kupatikana mtambo wa rangi wa uchapishaji magazeti ya Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar, ambapo imechukua hatua mbali mbali ikiwemo kuandika mapendekezo ya mradi wa ununuzi wa mtambo huo na kuuwasilisha Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ili uwe miongoni mwa miradi inayofadhiliwa na Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012. Lakini kutokana na uhaba wa fedha mradi huo haukuweza kutengewa fedha katika bajeti hii.

Mhe. Spika, jitihada nyengine zilizochukuliwa ni kuandikwa mapendekezo ya miradhi *"Project Proposal"* na kupelekwa kwa washirika wa maendeleo mbali mbali ili kusaidia shirika kupata mtambo wa kuchapisha magazeti ya rangi kwa lengo la kuchapisha magazeti ya Serikali hapa hapa nchini badala ya kupelekwa Tanzania Bara.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mara ya kwanza na naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ahadi ya kuifunga mitambo ya televisheni na redio kwa

ajili ya kuingia mfumo mpya wa matangazo imekuwa ikitolewa kwa muda mrefu na tumeambia mwezi wa nne, mwezi wa tano hadi sasa tunaambiwa ni mwezi wa saba. Lakini taarifa ambazo ziko ni kwamba mitambo hii imeletwa hapa kwa jina la mtu mwengine na sio la serikali kupitia Wizara ya Habari. Naomba kujua hii taarifa hii ni kweli na kama ni kweli imekuja hapa kwa jina la mtu mwengine Wazanzibari wanaomba kumjua ni nani aliyeleta mitambo hii kwa niaba ya serikali.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli mitambo ililetwa kwa jina la mtu mwengine lakini hiyo hali imesharekebishwa na hivi sasa mitambo ipo ya Pemba iko Pemba na ya Unguja ipo hapa, kilichobakia hivi sasa ni taratibu za kiufundi na za kisheria, lakini wakati wowote tunafunga mitambo hiyo pengine wala isifikie Augasti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali mojoa la nyongeza. Mhe. Spika, tulikuwa tunaomba kutajiwa jina la huyo mtu ambaye mitambo hii ililetwa kwa jina lake na kwa nini iletwe kwa jina lake isiwe kwa jina la serikali ambayo ndio inayoleta mitambo hiyo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli hii imekuja kupitia Wizara ya Fedha jina siwezi kulikumbuka lakini baadae nitakupa hilo jina.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza fupi kabisa. Mhe. Spika, wananchi wa Zanzibar wana hamu ya kusikiliza televisheni Zanzibar na Sauti ya Tanzania Zanzibar na hivi sasa tuko katika mchakato wa kipindi cha bajeti, wananchi wana hamu ya kuwasikia wajumbe wao katika Baraza la Wawakilishi, na Sauti ya Tanzania Zanzibar pamoja na TVZ, hivyo tunaoneshwa tukiwa Barazani kipindi cha kuanzia saa 3:00 mpaka 4:30 kipindi cha maswali na majibu na televisheni wanaonesha aidha usiku katika vipindi maalum, yaani kutoka Baraza la Wawakilishi ni vile vipindi vidogo vidogo vya kuwakatisha katisha wananchi.

Sasa je, kwa sababu wazee wanasema “isiyo mkami hujikama wenyewe”, ni lini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar italiwezesha Baraza la Wawakilishi ili waweze kuhudumia vipindi kuonesha wananchi moja kwa moja kutoka Baraza la Wawakilishi mpaka linapomaliza muda wake.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli lakini hilo suala tayari nimeshazungumza na vyombo vyangu kwamba waoneshe *live* maana yake *through out*. Vyombo vya Televisheni pamoja na Redio. Lakini vile vile tukumbuke kwamba tuna matatizo ya bajeti, kwa kweli

ni gharama, lakini pamooja na hivyo tutavionesha kadiri tunavyoweza kwa sababu mkumbuke kwamba ni bajeti ambayo tumeikuta kidogo hamna kitu, tunakwenda hivyo hivyo na *Alhamdulillah* kidogo kuna mabadiliko. Nimejaribu kuzungumza nao na hivi sasa wanaonesha *almost through out*. Kwa hivyo, nawaomba Wajumbe tuwe na stahamala kidogo haya masuala tutayarekebisha na mtafaidika nyote. Ahsanteni sana.

Nam. 217

Uingizwaji wa Bidhaa Mbovu

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Zanzibar hivi sasa imekuwa dampu la bidhaa mbovu kama vile vifaa vya majumbani, magari na hata vyakula.

(a) Je, wizara haioni kutokudhibiti bidhaa hizo kuingizwa nchini kunaweza kuleta madhara kwa wananchi hapo baadaye.

(b) Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba wizara imeshindwa kudhibiti uingizaji wa chakula na vifaa vibovu hapa nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 217 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, uagizwaji wa bidhaa zisizofikia viwango vinavyokubalika hapa nchini ulichangiwa kwa kiasi kikubwa sana na kukosekana kwa sheria ya kusimamia viwango na ubora wa bidhaa. Katika kukabiliana na tatizo hilo Mhe. Spika, ndipo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ilipoandaa Mswada wa Sheria ambao tayari umeshawasilishwa katika kikao cha Baraza lako tukufu cha mwezi wa Januari mwaka huu.

Ndani ya sheria hiyo, serikali ikusudia kuunda Taasisi ya Viwango ya Zanzibar ambayo itakuwa na mamlaka ya kuweka na kusimamia viwango vya bidhaa za aina zote zinazozalishwa na zinazoingizwa hapa nchini. Mhe. Spika, sheria hiyo tayari hivi sasa ipo katika hatua ya uwekwaji saini na Mhe. Raiz ili hatimaye iweze kutumika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa mitumba ya TV, Friji

pamoja na Viyoyozi (*IC*), vimekuwa vikiingiza au kuleta *chemical* mbali mbali ambazo zina sumu. Je, waziri haoni kwamba ipo haja sasa kudhibiti kuingizwa kwa mitumba hiyo ili kudhibiti uenezi wa *chemical* hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, nimesema katika jibu langu kwamba tatizo hilo serikali imeliona na kwa kuwa kulikuwa hakuna sheria ndio kupitia wizara yangu imeshaleta sheria, na sheria ile imewasilishwa ndani ya Baraza hili na kujadiliwa kwa kina na hatimaye ikapitishwa sasa tunasubiri Mhe. Rais aitie saini ili iweze kutumika. Ndani ya sheria hiyo Mhe. Spika, yote hayo hayatatokea tena ikianza kutumika, lakini kwa vifaa ambavyo vimeshaingia ndio vimeshaingia hivyo. Lakini sasa tutazuia vyegine ambavyo havitafikia viwango pamoja na vyenye matatizo kama hayo aliyoyasema Mheshimiwa hatatokea tena.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko napenda kuongeza majibu ya ziada kwa ajili ya faida ya Baraza lako tukufu.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Nassor Salim Ali kwa kuona matatizo ambayo tunaweza kuyapata katika jamii hasa athari za kimazingira kwa kutokudhibiti bidhaa chakavu na mbovu hasa hizi ambazo zameuliza kwenye suala lake la ziada la TV na vifaa vya umeme na kwa lugha ya kitaalamu takataka hizo huitwa *E-West***.**

Ofisi yangu ambayo ndani yake ina jukumu la kutunza na kudhibiti mazingira yetu yasichafuliwe, lakini kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaishi katika hali ya usalama, na kwa kuwa utupaji wa takataka hizo ambazo zinaingizwa ndani ya visiwa vyetu kwa wingi sana, vifaa hivyo vya *electronics* na umeme ni hatari, basi tayari imeshaandaa kanuni ya udhibiti wa uingizaji wa bidhaa chakafu za *electronic* na umeme. Hivi sasa kanuni hizo ziko katika hatua za mwisho za kisheria ili zipitishwe na ziweze kutumika. Ahsante.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa vile bishara zote zinapelekwa kwa matajiri. Je, chakula cha hakiba likitokea janga liko chini ya nani? *(Makofi)*

Mhe. Spika: Sijui kama swali hili lina mahusiano moja kwa moja na suala liliopo. Nikuombe basi Mheshimiwa ungetengeneza swali la msingi ukamuuliza Mhe. Waziri.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, lakini kwa sababu biashara hiyo wamekiri kuwa imeshamiri Zanzibar kwa nguvu na inaweza kutusababishia madhara mbele yake, ana anasema kuwa tayari kanuni imeshatungwa ili kudhibiti hii hali. Napenda kumuuliza Mhe. Waziri, pamoja na kwua tunasubiri kanuni j, ni watu wangapi ambao wameweka katika orodha yao ili kanuni ikiwa tayari kwa ajili ya kuwachukulia hatua.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais alipokuwa akijibu amesema kwamba wizara iko katika maandalizi ya kanuni. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Subeit akawa mstahamilivu akasubiri kanuni hizo zikaandaliwa na bila shaka atapata majibu ya swali lake kuwa ni watu wangapi na kwa kiasi gani.

Nam. 55

Tatizo la Uhaba wa Maji Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Maji yana umuhimu wa pekee katika maisha ya binadamu; na ingawa tunaamini kuwa visiwa vyetu vyote vya Zanzibar vina hazina ya kutosha ya maji, wananchi takribani wote wa Zanzibar wamo kwenye dimbwi la matatizo ya maji.

(a) Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wa kuwaondoshea wananchi wa Zanzibar dhiki hiyo.

(b) Je, wizara yako haioni kuwa ukubwa wa wizara yenyewe ni moja kati ya sababu zilizopelekea suala la maji kupewa uzito mdogo na hivyo kukosa kipaumbele katika utendaji wa shughuli za wizara yako.

(c) Je, serikali haioni kuwa ipo haja ya kuliweka suala la maji kwenye wizara maalum na kuhakikisha kuwa suala la maji Zanzibar linapata msukumo unaostahiki na kuweza kushughulikiwa kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 55 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, awali ya yote kimsingi napenda kukubaliana na Mhe. Mwakilishi juu ya imani yake kuhusu kuwepo kwa hazina kubwa ya maji katika Visiwa

vya Zanzibar ukilinganisha na baadhi ya visiwa. Kwa kuwa Zanzibar imezungukwa na maji ya bahari, napenda kuchukua fursa hii kutoa indhari ya kuwa tuwe waangalifu katika matumizi ya hazina hiyo.

Kuhusu suala la wananchi takriban wote wapo katika dimbwi la matatizo ya maji, naomba kwa heshima na taadhima kutokukubaliana na Mhe. Mwakilishi, hii ni kwamba, kwa mujibu wa takwimu za sasa wastani wa asilimia 81 (81%) ya wananchi wanaoishi mjini Unguja na Pemba wanapata huduma ya maji safi na salama, ingawa kwa baadhi ya maeneo maji hayo yanapatikana kwa mgao (*rationing*) na asilimia ipatayo 61 (61%) ya wananchi wanaoishi vijijini huduma ya maji safi na salama ambapo kwa jumla wastani wa asilimia 72 (72%) ya wananchi wote wa Zanzibar wanapata huduma hiyo ukilinganisha na Tanzania Bara ambapo wao wapo chini ya asilimi 70 (70%) ya upatikanaji wa maji kwa nchi nzima. Baada ya maelezo hayo machache naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) *JICA, AFDB, UN Habibat, JPAS, ACRA, Multilateral Debt Relief Initiative (MDR)* na jitihada za kupata wafadhili wengine zinaendelea ili kuondoa kabisa tatizo la maji Zanzibar.

Mhe. Spika, swali nambari (b) na (c) namuomba Mhe. Mwakilishi atustahamilie kwa muda mdogo tu, kulifanyia marekebisho kutokana na koseo lililofanyika katika maandishi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri anasema hakubaliana na mimi. Je, atakubaliana na mimi kuwa Majimbo ya Unguja na Pemba ni 50, na kwa takwimu alizozitoa hapo ni kwa majimbo 10 tu yanayokosa maji. Kwa idhini yako Mhe. Spika, atakuwa tayari kutuhesabu waheshimiwa wangapi tunaokosa maji katika majimbo yetu.

Pili Mhe. Spika, kuna mpango wa kufunga mita za maji kwenye nyumba, ni mita ngapi ambazo zimeshafungwa kwa muda huu, nyumba ngapi zimeshasajiliwa mita hizo na kiasi gani serikali inapata kwa kukusanya mapato hayo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa ufafanuzi katika maswali ya ya a, b, na c. swali la (a) Mhe. Spika, mara nyingi nimekuwa nikizungumza katika Baraza lako tukufu kwamba suala la maji linashughulikiwa sana.

Hivi karibuni nilizungumza kuna mradi wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambayo imeshakubali na tumeshatia saini waraka wa kuchimba visima mwanzo nilisema 52 nimekosea, naomba radhi ni visima 34 Unguja na Pemba

ambavyo hivi visima kila kimoja kitajitosheleza wenyewe kwa umeme, mabomba, usambazaji na kila kitu ili kusaidia kuondosha tatizo la maji kwa kiwango kikubwa.

Lakini katika swali la (b) Mhe. Mwakilishi ametaka kujua wizara yangu ina mpango gani wa kulipunguza tatizo hili au kuondosha, kama suala hili amesema kwa sababu ya wizara ni kubwa haikupewa kipaumbele cha kutosha. Mhe. Spika, nasema wizara yangu hata na serikali kwa ujumla imetoa kipaumbele kikubwa sana katika suala la maji.

Mhe. Waziri wa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wakati anasoma bajeti yake aliitaja Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati imewekewa kipaumbele nambari tatu ukiacha Wizara ya Elimui na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Afya. Kwa hivyo, si kweli kwamba wizara yangu haikutoa kipaumbele katika kuliondosha tatizo la maji, tatizo la maji linashughulikiwa kweli kweli.

Swali la (c) Mheshimiwa alipendekeza kwamba wizara au idara hii ya maji iundiwe wizara yake maalum ili ipate *attention* ya kutosha. Mhe. Spika, tutakumbuka Mwenyekiti wa Wenyeviti, *comrade* Hamza Hassan Juma.

Huyu namwita *comrade* kwa sababu ni mwenzangu wa karibu sana, alisema wakati anasoma hotuba yake kwamba serikali hii imepanga wizara nyingi, lakini leo kunakuja *suggestion* kwamba maji yawe na wizara yake ni mitazamo miwili tofauti. Mitazamo hii kama ni lazima basi mwenye maamuzi ni Rais mwenyewe ndiye anayepanga wizara zake na ndiye anayechagua mawaziri wake. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tatizo la maji linashughulikiwa, tumelipa kipaumbele kikubwa na sioni kama kuna haja ya kulipa wizara yake maalum.

Mhe. Spika, kuhusu suala la mita, bado mita hatujazifunga katika maeneo yote na zile zilizofungwa zimefungwa kwa majaribio tu kuhakikisha zinafanya kazi, haziharibiwi, lakini azma ya kununua mita ipo na tukifanya hivyo tutaweza kurikodi idadi ya maji yanayotumika, kuwatoza wanaotumia maji kwa uhakika na kwa uadilifu. Kwa hivyo, idadi ya mita zipo. Hizo takwimu alizozitaka Mheshimiwa zitapatikana wakati hizo mita zitakapofungwa na zikianza kufanya kazi. Ahsante sana.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, suala mali limekuwa kama ni donda ngugu hapa Zanzibar hasa kwa baadhi ya maeneo na wanaoathirika zaidi na matatizo haya ni wanawake na watoto. Naomba kumuuliza Mhe. Waziri, wizara yake ina mpango gani wa kuwasaidia angalau magari ya maji wale watu ambao wanashida zaidi ya maji japo wiki mara moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali hilo kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri wangu kutokana na swali la (b) na (c) kulijibu wakati nilisema tupewe muda kidogo. Lakini kwa bahati nzuri Mhe. Waziri wangu yuko makini na kiwanda cha kujibia kiko hapa hapa. Kwa hivyo, namshukuru sana kwa kuyajibu maswali hayo vizuri.

Baada ya hapo namjibu Mheshimiwa kuwa wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji itajitahidi hususan katika kipindi cha Mwezi wa Ramadhani katika maeneo yale ambayo maji hayajafika au yana upungufu kuwapelekea magari ya kuwasaidia wanawake hao maji.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na Mhe. Waziri na jitihada za serikali, lakini Mhe. Spika, mimi nataka kuuliza swali kwamba, suala la maji kama linavyozungumzwa imekuwa ni kadhia kwa miaka 47 na serikali inaonesha jitihada kubwa za kuweza kulitatua tatizo hili, hata wafadhili wa nje ambapo inafikia pahala wananchi wanajenga matumaini kutokana na maelezo wanayoyapata serikali yao pamoja na wafadhili na hususan suala la hivi karibuni la mradi wa Japan katika Mkoa wa Mjini ambalo wananchi walijenga matumaini ya kupata maji. Je, Mhe. Waziri haoni kwama kuna tatizo katika idara yake na sio visima. Kwa sababu visima vimeshakuwa vingi na mpaka vinahatarisha maisha ya nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, namshukuru Mheshimiwa kwa kuthamini jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuliondosha tatizo la maji.

Mhe. Spika, kuchimba visima ili kupata maji ni lazima, hakuna njia nyengine mbadala ya haraka haraka kwa sababu wananchi wa Zanzibar hawana uzoefu wa kuvuna maji ya mvua ili kuyatumia kwa mahitaji yao, ukiacha kidogo kwa kufulia. Sasa kuchimba visima ni aula na visima hivi tutakavyoendelea kuvichimba tutavichimba baada ya utafiti kumalizika. Hivi sasa tunaendelea na utafiti katika hayo maeneo ambayo tumeya-*identify* kwamba tutachimba visima hivyo wala hatutohatarisha maisha ya wananchi.

Mhe. Mwakilishi namuomba aendelee kuwa mstahamilivu tunajua tatizo la maji kama aliavyosema mmoja aliyechangia kwamba ni donda ndugu, tunajua tatizo la maji ni muhimu kuondolewa na *Inshaallah* tutaliondosha. Lakini tutaliondosha kwa mashirikiano ya wafadhili na ya wananchi kwa ujumla pamoja na wawakilishi, watusaidie kuunga mkono jitihada zetu hizi na *Inshaallah* huko twendako hali itakuwa nzuri.

Nam. 165

Mkataba wa Muungano

Mhe. Omar Ali Shehe - Aliuliza:-

Tanzania ni muungano wa nchi mbili huru, yaani Tanganyika na Zanzibar ambazo ziliungana chini ya Mkataba wa Muungano ambao ulitambua mambo kumi na moja ya Muungano. Baada ya Miaka 47 ya Muungano wetu mambo hayo yameongezeka na kufikia zaidi ya thelathini.

Je, Mkataba wa Muungano au Sheria zilizotungwa na Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar na kuthibitisha Mkataba huo, ziliweka utaratibu gani wa namna ya kupunguza au kuongeza mambo hayo ya Muungano.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 165 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kuwepo kwa mambo ya Muungano kumeelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 4 (3) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, na pia orodha ya mambo ya Muungano imetajwa katika nyongeza ya kwanza ya katiba hiyo. Mhe. Spika, kwa mujibu wa orodha ya nyongeza ya kwanza, mambo ya Muungano yaliyoorodheshwa ni 22 na sio zaidi ya 30.

Mhe. Spika, ibara ya 98(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka masharti ya kufuatwa endapo patatokea mabadiliko kwenye mambo ambayo yameorodheshwa kwenye orodha ya pili. Orodha hiyo imeorodhesha mambo 8, moja ya mambo hayo ni orodha ya mambo ya Muungano.

Mhe. Spika, mabadiliko yoyote ya mambo yaliyotajwa katika orodha ya nyongeza ya pili yanahitaji kuungwa mkono kwa kura za Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na Theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar.

Kwa maana hiyo, ikiwa jambo la Muungano lililopo katika orodha ya mambo ya Muungano linataka kuondolewa katika orodha hiyo, basi ni lazima theluthi mbili ya Wabunge kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Zanzibar wakubali, vyenginevyo jambo hilo halitoondolewa. Hata hivyo, kama kuna jambo ambalo linataka kuengezwa katika orodha ya mambo ya

Muungano, basi pia ni lazima theluthi mbili ya ya Wabunge kutoka Bara na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Zanzibar wakubali, vyenginevyo halitakuwa jambo la Muungano.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize swali Mhe. Waziri. Je, katika mambo hayo ambayo yaliongezwa kutoka 21 hadi yaliofikia sasa, yalifuata utaratibu huo wa thuluthi mbili kutoka kila upande.

Pili, Mheshimiwa kama tulivyosema kwamba Muungano wetu ulikuwa chini ya mkataba wa Muungano, na inasemekana kwamba mkataba ulitakiwa uridhiwe na Bunge la Tanganyika kwa wakati ule na vile vile uundiwe sheria na Baraza la Mapinduzi kwa wakati ule. Kuna taarifa kwamba Bunge la Tanganyika liliridhia mkataba ule. Je, Baraza la Mapinduzi nalo liliridhia likatunga sheria ya kuukubali mkataba ule. Kama ikiwa tulikubali ni *decree* nambari ngapi iliyopitishwa na Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ni kweli kwamba mambo ya Muungano katika mkataba wa Muungano mwanzo yalikuwa 21, hivi sasa katika katiba hii tuliyonayo ni 22. Sasa swali ni kwamba je, ilifuata utaratibu huo? Mimi naamini ulifuatwa utaratibu huo, kwa sababu wakati wote huo tulikuwa na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano ambao wanatoka upande wa Zanzibar.

Kwa hivyo, na wao kwa sababu walijua au walikuwa wanajua utaratibu huu naamini wasingelikubali kupitisha hayo bila ya kutumia utaratibu huo. Kwa hivyo, swali lako la kwanza naamini kwamba utaratibu huo ulifuatwa na ndio mambo hayo yakawepo.

Pili ni kweli kwa wenzetu Tanzania Bara wao kulikuwa kuna sheria ambayo iliridhia, kwa Zanzibar hilo ni suala ambalo linaulizwa ulizwa kama tuliridhia au hatukuridhia. Lakini napenda niseme mbele ya Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba kwa sheria kuna mambo ambayo ukishakukaa nayo kwa muda mrefu yale inakuwa yamekubalika kisheria.

Kwa mfano, hata wewe Mhe. Omar kama una eneo lako unalima kwa miaka 40 hujaulizwa sasa hawezi tena mtu kuja akasema eneo lile ni lake. Kwa maana hiyo, mkataba huu wa Muungano kwa lugha inayoitwa *aqua essence* yaani tumeridhika kwa wakati wote huo hatujaelezea haya. Kwa hiyo, mkataba huu wa Muungano ni halali kwa misingi hiyo.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa sasa suala la Muungano limekuwa midomoni kwa kila mwananchi wa Zanzibar. Kwa kuwa

hivi karibuni huenda tukatoa maoni yetu kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Je, huoni kwamba ipo haja sasa kwa serikali kuwapatia wananchi makala ya hayo mambo ambayo yamekubalika ili kuwapa upeo zaidi wa kuja kuyajadili katika hiyo kanuni.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, sina uhakika unaposema wananchi kupatiwa orodha ya mambo yanayokubalika. Lakini mambo yaliyomo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio mambo yaliyokubalika ya Muungano katika orodha ya mambo ya Muungano.

Hivi karibuni kulikuwa na mjadala na mjadala huu utaendelea katika suala la mambo ya Muungano. Tunafikiri ni jukumu la wananchi wote wa Zanzibar kukaa, kujadili, kusema na kutoa maoni ikiwa yale yanayotaka yaongezwe au kuna mambo ambayo yanataka yapunguzwe. Sasa kauli za wananchi hizo ndio zitazifanya serikali zote mbili kuamua kama mambo ya Muungano yaongezwe au yapunguzwe. Kwa hiyo, ni jukumu la wananchi kukaa kwa pamoja na kujadili kwa urefu kabisa na kwa undani ni mambo gani ambayo wangelipenda yaendelee kuwa ya Muungano au mambo gani wangelipenda yasiwe ya Muungano.

Lakini kwa yale ambayo ni ya Muungano hivi sasa Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaeleza wazi na ni 22 kama nilivyosema katika jibu langu mama.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Spika, swali langu ni kwamba mkataba wa Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar hautoi fursa mahala popote pa kuongeza mambo ya Muungano. Je, nini uhalali wa mambo haya kuongezwa kupitia katika Bunge la Muungano hasa ikizingatiwa kwamba watu mashuhuri Zanzibar akiwemo Rais Mstaafu Dk. Salmin Amour Juma wakati akiwa rais aliwahi kutamka kwamba Zanzibar inatambua mambo 11 tu ya asili ya Muungano.

Lakini hata Mhe. Waziri mwenyewe katika waraka wake maarufu ambao umechapishwa katika kitabu cha *Zanzibar and The Union Question* alihoji uhalali wa mambo haya yaliyoongezwa katika Muungano. Kwa hiyo, nilitaka kujua kwa sababu mkataba haujapewa fursa ya kuongeza uhalali ni upi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ni kweli na nakubaliana nae kwamba mkataba wa Muungano *(Articles of Union)* hamna kifungu chochote kinachozungumzia suala la marekebisho ya mambo ya Muungano. Lakini historia ya mkataba huu Mhe. Ismail Jussa Ladhu anaujua. Kifungu kimoja cha *Articles of Union* kinasema kwamba kutakuwepo *constituent assembly* ambayo kama ninavyojua ilibuniwa ikawa ni Bunge la Jamhuri ya Muungano na hilo ndilo lililopendekeza kwamba Katiba ya Tanganyika wakati ule iwe *adopted*

kuwa ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano na baadae ikaja mpaka Katiba ya 1977. Ndani ya Katiba ya 1977 ndiko kwenye kifungu cha mabadiliko haya.

Kwa hivyo, *Articles of Union* zilikuwa *adopted* katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano na humo ndimo mlimokuwa na kifungu cha kurekebisha ama kupunguza au kuongeza mambo ya Muungano. Ndio maana hivi sasa tunatumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 ama kurekebisha au kupunguza mambo ya Muungano. Suala la kwamba kuna matatizo katika suala hili ni suala jengine ambalo sote tunalikubali.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kwa Mwaka 2011/2012

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea na hoja tuna matangazo mawili. Nimeombwa na Mhe. Haji Faki Shaali Mwakilishi wa Jimbo la Mkanyageni aliponipigia simu jana wakati wa jioni nikuarifuni kwamba baba yake mzazi Mzee Faki Shaali amefariki jana mnamo saa za asubuhi tarehe 26 mwezi huu na alizikwa hiyo hiyo jana mnamo saa za mchana. Kwa hiyo, ameniomba nikupeni taarifa ili tujumuike nae katika msiba huo uliomfika wa kufiwa na baba yake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amlaze marehemu mahala pema peponi.

La pili nimeombwa wale wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wakutane katika chumba cha kamati namba 2 hivi punde kuna jambo muhimu wakapewe taarifa. Baada ya jambo muhimu hilo niwaombe basi wajumbe hawa warudi ukumbini ili tuendelee na kazi tunayoikusudia kuifanya kwa wakati huu.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo, sasa namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuja hapa ili kuwasilisha hotuba yake ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru lakini kabla ya kuwasilisha rasmi hotuba yangu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naomba uniruhusu kuwaomba radhi Wajumbe wa Baraza lako tukufu kutokana na matatizo kidogo ya ufundi yaliyotokea katika utayarishaji wa kitabu changu.

Nawaomba wajumbe katika ukurasa wa 20 mara tu baada ya kifungu cha 47 kuna ukurasa wa ziada umegaiwa ambao unaanzia kifungu cha 47 (a) mpaka 46 (e). Naomba uchukuliwe kama ni sehemu ya hotuba yangu. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ukurasa wenyewe ndio huu nafikiri kila mmoja amepatiwa. Kama kuna mjumbe ambaye hakupata basi watendaji wanaweza kumpelekea.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama kamati ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili, kuchangia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kazi za kawaida na za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutoa hotuba yangu ya Mmakadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Pia kwa kutuwezesha kukutana katika kikao hichi cha kwanza cha Bajeti ya Serikali ya Awamu ya Saba yenye muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kikao ambacho ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, napenda uniruhusu kwa niaba yangu na kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kumpongeza kwa dhati Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa Oktoba, 2010. Uchaguzi huo umempa nafasi ya kuanza vyema kuliongoza Taifa letu katika hali ya amani na utulivu mkubwa chini ya Mfumo mpya wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, amani, upendo na mshikamano ni nyenzo muhimu katika uendeshaji wa nchi yetu. Kwa mnasaba huu, napenda kuchukua fursa hii adhimu na ya kipekee kumpongeza Rais wa Zanzibar wa Awamu ya Sita, Dk. Amani Abeid Karume kwa moyo wake wa kijasiri wa kukutana pamoja na Maalim Seif Sharif Hamad, Katibu Mkuu wa CUF ambaye sasa ni Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar katika awamu hii ya saba na hatimaye kufikia Maridhiano yaliyopelekea Wazanzibari sote kwa umoja wetu kufanya kazi kwa pamoja kupitia mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na hivyo kutuhakikishia umoja wenye tija kwa Wazanzibari wote.

Zanzibar ni Visiwa vyenye historia kubwa ya upendo, umoja na mshikamano, ni faraja leo hii tupo katika chombo hichi kitukufu tukiwawakilisha Wazanzibari kwa umoja wao huku tukiwa tumefuta kabisa siasa za mivutano

ambazo nazo zimebaki kuwa ni sehemu tu ya historia ya Visiwa hivi. Maridhianao haya yaliyoasisiwa na Viongozi wawili hawa leo hii yanatupa nafasi sote Mawaziri na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupanga na kujadili khatima ya nchi na wananchi wetu katika kuwaletea maendeleo yao ya kiuchumi na kijamii.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kuwapongeza Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad na Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kwao. Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi wetu hawa wote wawili kwa utendaji na umahiri wao wa kufuatilia na kutoa ushauri. Ufuatiliaji ambao pamoja na mambo mengine unachangia katika kupatikana mafanikio ya utendaji wa majukumu ya wizara na taasisi zote za Serikali. Pia katika kumsaidia Mhe. Rais, kumshauri kwa uadilifu mkubwa unaomwezesha kuiongoza nchi yetu vizuri.

Mhe. Spika, napenda uniruhusu kukishukuru kwa dhati kabisa chama changu, Chama cha Wananchi - CUF kwa kuniamini, kuniteua na hatimae kunipendekeza kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwanza kuwa Mwakilishi lakini pia kunipa dhamana ya uongozi kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Napenda nikiahidi chama changu na wananchi wote wa Zanzibar kwamba nitatekeleza majukumu yangu kwa kadri *Allah* atakavyonijaalia.

Mhe. Spika, napenda kumshukuru kwa dhati Mhe.Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa imani aliyonayo kwangu kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Napenda kumhakikishia Mhe. Rais na wananchi wote kwa ujumla kuwa nitafanya kazi zangu kwa juhudi maarifa na kwa kadri ya uwezo nitakaojaaaliwa katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, napenda kumshukuru kwa dhati Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad kwa ushauri wake na miongozo anayonipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku. Kwa hakika busara, hekima na uwezo wake wa kusimamia majukumu yake, unanipa changamoto kubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Namuahidi kuwa sitomuangusha katika kazi zangu za kumsaidia kutekeleza majukumu yaliyo chini ya ofisi yake.

Mhe. Spika, napenda uniruhusu kukupongeza wewe binafsi na wasaidizi wako kwa kuliongoza Baraza hili Tukufu kufuatana na sheria na kanuni za Baraza, lakini zikichangiwa sana na hekima na uadilifu mlionao wewe pamoja na watendaji wako.

Mhe. Spika, naomba pia kuchukua nafasi hii kuipongeza Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura na Makamo Mwenyekiti Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Viti Maalum kwa kufanya nao kazi kwa karibu zaidi na kuisaidia sana Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Ushirikiano wanaotupa unaonesha mwanzo mzuri wa mafanikio makubwa wa ofisi yetu kutokana na michango ya Wajumbe wa Kamati hii. Aidha, naomba kuwapongeza Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kutoa michango yao mizuri pamoja na mashirikiano na mshikamano wanaouonesha katika kuleta maendeleo ya nchi yetu na Taifa letu kwa ujumla.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi yetu. Vile vile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wakurugenzi pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa juhudi, bidii na ustahamilivu katika kutekeleza majukumu yao ya kazi na kuleta ufanisi kwa Taifa.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais napenda kutoa mkono wa pole kwa Mhe. Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto pamoja na familia ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Bi. Rahma Mohammed Mshangama aliyefariki dunia tarehe 15/04/2011. Tutamkumbuka marehemu kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi. Amin.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo naomba sasa uniruhusu nitoe maelezo ya utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 na malengo ya mwaka wa fedha 2011/2012 ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2010/2011

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ni ofisi mpya iliyoundwa kutokana na mabadiliko ya 10 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Mabadiliko hayo yaliweka misingi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Hivyo, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imepangiwa kutekeleza majukumu yake kupitia sekta muhimu ambazo zinaundwa na Idara na Tume zifuatazo:

1. Ofisi Kuu Pemba
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
3. Idara ya Uendeshaji na Utumishi

4. Idara ya Mazingira
5. Idara ya Watu wenye Ulemavu
6. Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya
7. Tume ya UKIMWI

Muundo wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais unaonekana katika kiambatanisho Nam.1.

Mhe. Spika, ofisi yetu ni mpya lakini katika taasisi saba zilizo chini ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Idara mbili na Tume mbili zilikuwepo kabla ya kuundwa kwa Ofisi hiy. Taasisi hizo nne zilizokuwepo ni Idara ya Mazingira, Idara ya Watu wenye Ulemavu, Tume ya UKIMWI na Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Hivyo, naomba niwasilishe malengo na utekelezaji wake katika kipindi cha mwaka 2010/2011 kama ifuatavyo:

MALENGO 2010/2011

Mhe. Spika, naomba niwasilishe malengo ya taasisi hizo nne yaliyopangiwa na utekelezaji wake kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

1. Kuendeleza kazi za utoaji wa elimu ya mazingira kwa jamii na wawekezaji.

2. Kufanya mapitio ya miradi 180 pamoja na kuratibu tathmini za kimazingira kwa miradi 20 ya maendeleo.

3. Kukamilisha utengenezaji wa viwango vya kimazingira kwa bidhaa za mitumba.

4. Kukamilisha kazi za uhifadhi wa kasa pamoja na kufanya utafiti juu ya mazingira ya maisha ya wanyama hao.

5. Kuendelea kusimamia upigaji marufuku uingizwaji na matumizi ya mifuko ya plastiki.

6. Kutekeleza kazi za mpango wenye uwiano wa maeneo ya pwani.

7. Kuendeleza kazi za kupunguza idadi ya kunguru kwa kutumia mitego na sumu.

8. Kuandaa miongozo juu ya huduma za dawa za kulevya.

9. Kutoa huduma za upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa hiari *(Voluntary Counselling and Testing-VCT)* kwa watumiaji wa dawa za kulevya na jamii kwa ujumla.

10. Kuelimisha jamii juu ya athari za matumizi ya dawa za kulevya.

11. Kuanzisha mfumo wa uwekaji kumbukumbu za watu wenye ulemavu.

12. Kuhamasisha jamii juu ya haki na fursa sawa za watu wenye ulemavu.

13. Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu.

14. Kuandaa vikao vya Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu.

15. Kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Kupambana na UKIMWI.

16. Kuwapatia wananchi elimu ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI.

17. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za kupambana na UKIMWI.

UTEKELEZAJI 2010/2011

IDARA YA MAZINGIRA

Mhe. Spika, hadi kufikia Mei, 2011 Idara ya Mazingira iliweza kutekeleza shughuli zifuatazo katika malengo iliyojipangia.

Mhe. Spika, ofisi yangu kupitia Idara ya Mazingira iliendeleza kazi za utoaji wa elimu ya mazingira kwa jamii na wawekezaji ambapo mikutano ya kuelimisha jamii juu ya uhifadhi wa mazingira imefanywa kwa wananchi wa Shehia 14 za Wilaya ya Magharibi. Aidha, vipindi vya redio vinavyohusu maliasili, mifuko ya plastiki na tathmini ya athari za kimazingira vimetayarishwa na kurushwa kupitia Zenj FM na Sauti ya Tanzania Zanzibar. Vilevile wajumbe 49 wa Kamati za Mazingira ya Shehia ya Nungwi Wilaya ya Kaskazini "A" wamepatiwa mafunzo kuhusu Mabadiliko ya Ttabia nchi *(Climate Change)*. (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 2)

Mhe. Spika, jumla ya ripoti 45 za uanzishaji wa miradi ya uwekezaji *(feasibility studies)* ikiwemo 42 Unguja na 3 Pemba zimefanyiwa mapitio na kutolewa

ushauri wa kimazingira kwa hatua zinazofuata. Miradi 14 imefanyiwa Tathmini za Athari za Kimazingira *(EIA)* na kupewa vyeti vya mazingira kwa hatua za utekelezaji. Aidha, miradi 26 ya uwekezaji imefanyiwa ukaguzi na tathmini *(monitoring and evaluation)* katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 3)

Mhe. Spika, kanuni za udhibiti wa bidhaa chakavu za elektroniki na za umeme *(e-waste)* imeandaliwa kwa kuwashirikisha wadau husika. Aidha, kanuni hiyo iko katika hatua za mwisho za kisheria ili iweze kutumika.

Mhe. Spika, ufuatiliaji juu ya maisha ya kasa umefanyika kwa kuwahoji wanavijiji wa Shehia 8 za Nungwi, Matemwe, Kiwengwa, Bumbwini Makoba, Uroa, Chwaka, Chukwani na Fumba. Asilimia 53 ya waliohojiwa wamesema kuwa mazalio ya kasa yameharibiwa kutokana na kuongezeka harakati za maendeleo katika ukanda wa pwani. Mipango inafanywa ili kuimarisha kamati za vijiji za udhibiti na uhifadhi wa kasa.

Mhe. Spika, usimamizi juu ya upigaji marufuku uingizwaji na matumizi ya mifuko ya plastiki umeendelea. Vipindi vya redio vimetayarishwa na kurushwa ili kuishajihisha jamii kutoitumia mifuko hiyo. Aidha, mikutano sita (6) imefanywa kwa wafanyabiashara wa Zanzibar, Manispaa, pamoja na viongozi wa wafanyabiashara katika masoko ya Mwanakwerekwe, Darajani na Mikunguni. Mkutano mwengine ulikuwa wa pamoja kati ya taasisi za Ofisi ya Mwanasheria, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, KMKM, Jeshi la Polisi, Mahakama, Ofisi za Upelelezi na Idara ya Mazingira. Madhumuni ya mikutano hiyo ilikuwa ni kushauriana juu ya kufanikisha usimamizi wa marufuku ya mifuko ya plastiki ikiwa ni pamoja na kutambua kasoro zinazojitokeza.

Sambamba na jitihada hizo, mabango ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki yametengenezwa na kuwekwa katika maeneo ya Uwanja wa Ndege, masoko ya Mikunguni na Mwanakwerekwe. Kiasi cha tani 68 za mifuko ya plastiki zilikamatwa katika maeneo ya Bawe na Ras Shangani.

Mhe. Spika, Kamati kumi (10) za Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Ukanda wa Pwani *(Integrated Coastal zone Management Committee -ICM)* zimewezeshwa kwa majaribio katika ngazi ya Shehia Unguja na Pemba ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa kazi za Mpango Wenye Uwiano kwa maeneo ya ukanda wa pwani.

Kamati hizo zimeanzishwa katika Shehia za Nungwi, Chwaka, Bububu, Nyamanzi, Mtende na Bumbwini Makoba kwa Unguja na Pemba ni Shehia za Chokocho, Ndagoni, Gando na Tumbe Mashariki. Aidha, wajumbe wa kamati hizo tayari wamewezeshwa kutambua na kuweka vipaumbele kwa matatizo

yanayowakabili na kuandaa mipango kazi ya miaka mitatu (3) ili kutatua matatizo waliyoyaibua.

Idara inaendelea na jitihada za kutafuta wafadhili wa kusaidia utekelezaji wa mipango hiyo. Sambamba na hayo, Idara imeweza kutoa elimu ya usimamizi shirikishi wa ukanda wa pwani kwa wajumbe wapatao 500 wa Kamati za Wilaya na Shehia Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kazi za kupunguza idadi ya kunguru kwa kutumia mitego na sumu zimeendelea kutekelezwa kwa mashirikiano kati ya Idara ya Mazingira na Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2011 jumla ya kunguru weusi wapatao 300,000 wameuliwa. Aidha, ili kufikia lengo la kuangamiza kunguru hapa nchini mradi maalumu umeandaliwa na utaanza utekelezaji katika mwaka ujao wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Idara ya Mazingira ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi 199,803,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 50,000,000/= ikiwa ni mchango wa Serikali kwa ajili ya baadhi ya miradi iliopo ndani ya Idara ya Mazingira. Hadi kufikia mwezi wa Juni, 2011 jumla ya Shilingi 38,248,718/= sawa na asilimia 19.14 zimeingizwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 22,000,000/= sawa na asilimia 44 zimeingizwa kwa ajili ya fedha za miradi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Idara ya Mazingira ilipangiwa kukusanya shilingi 6,000,000, na hadi kufikia mwezi wa Aprili 2011, Idara imeweza kukusanya shilingi 1,898,000 sawa na asilimia 31.7

TUME YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Spika, hadi kufikia Mei 2011 Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya iliweza kutekeleza shughuli zifuatazo katika malengo iliyojipangia.

Mhe. Spika, Tume iliweza kukamilisha uandaaji wa muongozo wa huduma za makaazi *(Sober Houses)* kwa marekebisho ya watumiaji wa dawa za kulevya *(Guideline on the Establishment of Residential Drug Recovery Centre)* zinazoendeshwa na taasisi zisizo za kiserikali (*NGOs*). Kazi hiyo ilifanywa kwa kushirikiana na Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Tanzania, Kitengo cha Dawa za Kulevya na UKIMWI cha Muhimbili Dar-es-Salaam na wadau mbali mbali wa hapa nchini.

Mhe Spika, Tume iliweza kutoa huduma za upimaji wa Virusi vya UKIMWI kwa hiari *(Voluntary Counselling and Testing)* kupitia kituo chake cha Huduma Rafiki cha Sogea. Kwa kipindi cha Julai 2010 na Aprili 2011, jumla ya watu

mia saba na sitini (760) walipatiwa huduma hiyo, wakiwemo wanawake mia tatu na tisini na sita (396) na wanaume mia tatu na sitini na nne (364).

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilichukua juhudi za makusudi za kuongeza kasi ya uwajibikaji wa vyombo vinavyohusika na usimamiaji na udhibiti wa dawa za kulevya kwa kukutana na vyombo hivyo.

Mhe. Spika, kazi ya kuelimisha na kushajiisha jamii juu ya athari za matumizi ya dawa za kulevya, iliendelea kufanyika kwa makundi mbalimbali. Jumla ya wanafunzi elfu nne na tatu (4,003) waliweza kupatiwa taaluma juu ya athari za matumizi ya dawa za kulevya, (wanaume 1,717 na wanawake 2,286) katika skuli za Unguja na Pemba.

Aidha, Masheha (144 Unguja na 58 Pemba) na maofisa (30) wa wilaya nne za Unguja na wilaya mbili za Pemba, waliweza kupatiwa taaluma ya dawa za kulevya. Wilaya zilizofaidika na taaluma hiyo ni Mkoani na Chake-Chake kwa Pemba na Magharibi, Kaskazini "A" na "B" pamoja na Wilaya ya Kusini kwa Unguja. Vilevile, jumla ya vipindi saba vilirushwa kupitia vyombo mbali mbali.

Mhe. Spika, Tume kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia (AZAKI) imeanzisha huduma za makaazi na marekebisho kwa watumiaji wa dawa za kulevya *(Sober Houses).* Jumla ya nyumba tano Unguja na mbili Pemba zimeanzishwa ambazo, hadi kufikia mwezi wa Mei 2011, vijana 698 wakiwemo wanaume 680 na wanawake 18 wamepitia katika nyumba hizo. Aidha, Tume iliweza kufanya juhudi za kuwajengea uwezo vijana 25 waliowacha kutumia dawa za kulevya kwa kuwapatia mafunzo ya kompyuta.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi 64,928,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 50,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Hadi kufikia mwezi wa Juni, 2011, jumla ya shilingi 28,769,599/= sawa na asilimia 44.31 za fedha za matumizi ya kawaida zimeingizwa, na jumla ya shilingi 20,000,000/= sawa na asilimia 40 zimeingizwa kwa ajili ya fedha za matumizi ya miradi ya maendeleo.

IDARA YA WATU WENYE ULEMAVU

Mhe. Spika, hadi kufikia Mei 2011 Idara ya Watu Wenye Ulemavu iliweza kutekeleza shughuli zifuatazo katika malengo iliyojipangia.

Mhe. Spika, mfumo wa uwekaji kumbukumbu kwa watu wenye ulemavu tayari umeanza. Idara imekusanya taarifa za watu wenye ulemavu katika Shehia 65 za Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kati ya hizo, Shehia 36, Wilaya ya Kaskazini "A" na 29 za Kaskazini "B". Hadi kufikia mwezi wa Mei, jumla ya watu 3007

wameshasajiliwa. Kabla ya kuanza kwa kazi hiyo, Idara ilifanya mikutano tofauti na baadhi ya wadau ili kupitia fomu ya ukusanyaji taarifa kwa kupata maoni yao pamoja na kufanya vikao na Masheha na watendaji wa wilaya hizo.

Mhe. Spika, Idara kwa kuhamasisha jamii juu ya haki na fursa za watu wenye ulemavu, ilifanya mazungumzo na waandishi wa habari kutoka vyombo mbali mbali vya habari kuhusu maendeleo na changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu ikiwemo unyanyasaji unaofanywa na waendesha daladala, unyanyasaji wa kijinsia na ushiriki wa watu wenye ulemavu katika masuala ya uchaguzi. Vile vile, Idara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Watu Wenye Ulemavu kwa kuandaa shughuli mbali mbali ikiwemo mashindano ya michezo iliyowashirikisha watu wenye ulemavu.

Aidha, Idara ilifanya vikao vya uhamasishaji wa haki na fursa za watu wenye ulemavu katika vijiji vitatu (3) Pwani Mchangani - Wilaya ya Kaskazini "A", Mangapwani Kaskazini "B" na Chuini Wilaya ya Magharibi, Jumla ya watu 98 walifikiwa. Katika kuwahamasisha watu wenye ulemavu kujishughulisha na kazi za kimaendeleo, Idara ilifanya juhudi ya kuwapatia mafunzo ya Kiingereza na kompyuta vijana 16. *(Tafadhali angalia kiambatanisho Nam. 4)*

Mhe. Spika, Idara inaendelea na kubuni mikakati na mbinu mbali mbali za kutunisha mfuko wa maendeleo ya watu wenye ulemavu. Hadi kufikia mwezi Mei, 2011 Idara imeweza kukusanya shilingi 3,030,000/= kutoka kwa taasisi mbali mbali na watu binafsi.

Mhe. Spika, Idara iliandaa vikao vinne vya Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar. Vikao hivyo vilijadili shughuli mbali mbali za watu wenye ulemavu ikiwemo changamoto na jinsi ya kuzipatia ufumbuzi. Katika kufanikisha hilo, Baraza lilifanya ziara katika taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuona zinajumuisha masuala ya watu wenye ulemavu katika mipango, sera na sheria. Tayari baadhi ya taasisi za Serikali na binafsi zinatoa ushirikiano mkubwa katika kuwashirikisha na kujumuisha watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara ya Watu Wenye Ulemavu ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 211,615,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Juni, 2011, jumla ya shilingi 90,226,385/= sawa na asilimia 42.64 ya fedha za matumizi ya kawaida zimeingizwa.

TUME YA UKIMWI

Mhe. Spika, hadi kufikia Mei 2011 Tume ya UKIMWI iliweza kutekeleza shughuli zifuatazo katika malengo yake iliyojipangia.

Mhe. Spika, Tume iliweza kuendelea na shughuli za uandaaji wa mkakati wa pili wa kupambana na UKIMWI. Utayarishaji wa Mkakati huo ulijumuisha mashauriano ya kina kwa makundi mbali mbali katika jamii. Mkakati huu umetoa uzito kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuambukizwa Virusi Vya UKIMWI (*VVU*) (wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao, wanawake wanaofanya biashara ya kuuza miili yao, na wanaotumia dawa za kulevya na hasa wanaojidunga sindano) na kuyashughulikia maeneo ambayo yana tabia hatarishi kwa kiwango kikubwa.

Tofauti na mkakati wa zamani ambao ulilenga zaidi kwa jamii nzima. Mkakati umechelewa kumalizika baada kupitiwa na kuhitaji kufanyiwa marekebisho zaidi. Hivi sasa mkakati uko katika hatua za mwisho za mapitio, licha ya kuchelewa kumalizika, mambo ya msingi katika kuweka mazingira mazuri ya utekelezaji wake yamefanyika.

Mhe. Spika, utafiti uliofanywa na Wizara ya Afya mwaka 2008 juu ya kiwango cha maambukizi na tabia zinazohusiana na maambukizi ya *VVU* ndani ya Vyuo vya Mafunzo umebaini kuwa ni asilimia 2.8 ya maambukizi. Kiwango hiki ni kikubwa ukilinganisha na kile kilichopo katika jamii cha asilimia 0.6. Hali hiyo imepelekea haja ya kuandaliwa mkakati maalum ili kudhibiti tatizo hilo. Katika hatua ya mwanzo, tume imefanya mikutano na viongozi wa Vyuo vya Mafunzo na makamanda 25 kwa nia ya kuwahamasisha. Hatua ya pili ilikuwa ni zoezi la kuandaa mkakati husika. Lengo kuu ni kuhakikisha kwamba maambukizi ya *VVU* yanadhibitiwa ndani ya Vyuo vya Mafunzo, kwa kuweka hali nzuri ambayo itaondosha mazingira yanayopelekea maambukizi ya *VVU* na maradhi mengineyo.

Mhe. Spika, suala la upatikanaji wa huduma za UKIMWI kwa wote ni la msingi katika mapambano dhidi ya UKIMWI na linahusiana na uzingatiaji wa haki za binaadamu. Katika kuhakikisha kwamba haki za binaadamu zinazingatiwa na makundi yote yanapata huduma wanazostahili na katika kuweka mazingira mazuri ya utekelezaji wa mkakati wa pili. Tume imeandaa rasimu ya Sheria ya Kukinga na Kushughulikia Masuala ya UKIMWI.

Mhe. Spika, katika kuwapatia wananchi elimu ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI, Tume imejikita kutoa elimu zaidi kwa njia ya redio na televisheni. Hivyo, Tume ilirusha matangazo mafupi ya redio mara 570 kupitia idhaa za Sauti ya Tanzania Zanzibar, *Hits FM*, *Zenj FM*, Redio Jamii Micheweni na Annur. Tume pia ilirusha hewani kupitia *Zanzibar Cable* na TVZ mara 150. Maudhui ya matangazo yamelenga kupunguza unyanyapaa ambao utafiti umeonesha kuwa bado upo ingawa umepungua kidogo.

Pia, Tume ilirusha hewani mara 60, matangazo yanayolenga kuzuia udhalilishaji wa kijinsia ili kupunguza maambukizi ya *VVU* kupitia idhaa tofauti za redio na mara 45 kupitia TVZ na *Cable TV*. Vile vile, Tume iliandaa filamu fundishi *(documentary film)* inayoonesha hali halisi katika jamii kuhusiana na udhalilishaji wa kijinsia.

Mhe. Spika, Tume ilizitembelea wizara zote (13) za serikali ili kuona utekelezaji wa shughuli za UKIMWI. Katika ufuatiliaji huo, Tume imebaini kuwa tokea kumalizika kwa mradi uliokuwa ukizisaidia sekta zote *Tanzania Multisectoral AIDS Project* (TMAP), utekelezaji wa shughuli za UKIMWI umedhorota katika sekta nyingi.

Mhe. Spika, baina ya mwaka 2006 na 2008, Tume ya UKIMWI kwa kushirikiana na wizara husika, ilitayarisha mitaala ya UKIMWI ili kuwezesha mafunzo ya UKIMWI kuwa endelevu na kutolewa kwa mpango mzuri zaidi. Vyuo vilivyohusika ni Utawala wa Umma - Forodhani, Kituo cha Mafunzo ya Amali Mwanakwerekwe na Mkokotoni, Chuo cha Kilimo Kizimbani, Chuo cha Usimamizi wa Fedha Chwaka pamoja na Mfuko wa Kujitegemea. Tume ilifanya ufuatiliaji kuangalia namna mitaala hiyo inavyotumika.

Matokeo yameonesha kwamba hali ya ufundishaji inatofautiana baina ya vyuo hivyo. Chuo cha Utawala wa Umma ni cha mwanzo kwa kuutumia mtaala ipasavyo ikifuatiwa na Mfuko wa Kujitegemea ingawa wamekwama kutokana na upungufu wa fedha. Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, Vyuo vya Mafunzo ya Amali na Chuo cha Kilimo Kizimbani hawajawahi kuutumia mtaala huo licha ya kupatiwa mafunzo na vifaa.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/12, Tume ya UKIMWI ilikadiriwa kutumia Shilingi 440,000,000/= .(shilingi 382,000,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 58,000,000/= kwa kazi za maendeleo). Katika kipindi hicho, Tume pia ilikadiriwa kutumia dola za Marekani 528,567.06 kwa matumizi ya kazi za kupambana na UKIMWI kupitia misaada ya Jumuiya za Kimataifa.

Hadi kufikia mwezi wa Juni 2011, fedha zilizoingizwa ni shilingi 330,735,124/= (sawa na asilimia 86) na dola 528,567.06 kutoka fedha za wahisani sawa na asilimia 100.

OFISI YA FARAGHA YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Kwanza wa Rais inajukumu la kumsaidia Makamu wa Kwanza wa Rais kuweza kutekeleza majukumu yake vizuri pamoja na kutoa huduma kwa kiongozi huyo. Hivyo basi Ofisi hii inaratibu shughuli zote za Mheshimiwa Makamu wa Kwanza Rais pamoja na

kuhudumia nyumba pekee ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais iliyopo Unguja.

Mhe. Spika, kuanzia kipindi cha Disemba 2010 hadi June, 2011 Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais ameweza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mabadiliko ya 10 ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 kwa kumshauri na kumsaidia Rais wa Zanzibar katika kuiongoza vyema nchi yetu na kwa umahiri mkubwa.

Mhe. Spika, Makamu wa Kwanza wa Rais amefanya ziara moja ya kiserikali nje ya nchi iliyozihusisha nchi za Uholanzi, Falme za nchi za Kiarabu na Oman. Katika ziara hiyo alipata nafasi ya kukutana na kufanya mazungumzo na wawekezaji mbali mbali ili kuwashajihisha waweze kuwekeza hapa Zanzibar. Aidha, Makamu wa Kwanza wa Rais alikuwa na mazungumzo na viongozi mbali mbali wa Serikali za nchi hizo ili kuona uwezekano wa kuisaidia Zanzibar kuweza kupiga hatua za haraka zaidi katika kujiletea maendeleo.

Kwa upande wa Serikali ya Oman ambapo alizungumza pia na Naibu Waziri Mkuu wa Oman, nchi ambayo iliahidi kuisaidia Zanzibar katika vipaumbele vyake vya kuleta maendeleo. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kufuatilia utekelezaji wa makubaliano hayo imeunda Kamati Maalum ya Baraza la Mapinduzi kufuatilia na kuratibu ahadi za wenzetu. Aidha, kamati ya wataalamu nayo imeundwa kwa ajili ya kukaa na timu ya wataalamu ya Oman ili kufanya mapitio ya maombi ya Zanzibar yaliyowasilishwa Serikali ya Oman kupitia ziara ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na kutembelea taasisi zote zilizo chini ya Ofisi hii pamoja na taasisi zisizo za Kiserikali na jumuiya za kiraia ambazo zinasaidiana na Ofisi yetu katika kutekeleza majukumu yake, ameshafanya ziara ya kuzitembelea wizara na taasisi mbali mbali za serikali ili kukagua shughuli za maendeleo na kushauri utekelezaji wa majukumu yao kwa ajili ya kuharakisha shughuli za maendeleo. Ziara zilifanywa katika Wizara ya Kilimo na Maliasili, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambapo alitembelea bandarini na uwanja wa ndege.

Mhe. Spika, Makamu wa Kwanza wa Rais amefanya mazungumzo na viongozi na mabalozi mbali mbali wa ndani na nje ya nchi, amekuwa akikutana na makundi tofauti ya jamii yakiwemo; Taasisi zisizo za Kiserikali, Asasi za Kiraia (AZAKI), Jumuiya za Kidini na hata mwananchi mmoja mmoja. Nia ni utekelezaji wa mabadiliko ya 10 ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 ya uundwaji wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar

na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika jitihada za kuiletea maendeleo Zanzibar kwa haraka zaidi, kudumisha amani na utulivu na kujenga mshikamano wa Wazanzibari wote.

MALENGO YA MWAKA 2011- 2015

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni Ofisi mpya iliyokabidhiwa dhamana nyingi ambazo zina changamoto kubwa katika jamii yetu. Masuala magumu na mazito ya kuhifadhi mazingira, mapambano dhidi ya dawa za kulevya, masuala ya watu wenye ulemavu na uratibu wa shughuli za UKIMWI, ni masuala mtambuka ambayo Taasisi zote za Serikali, Taasisi zisizo za Kiserikali na jumuiya za kiraia na wananchi mmoja mmoja lazima tushirikiane katika kutekeleza majukumu yetu haya katika kipindi hichi cha miaka mitano ijayo.

Mhe. Spika, muelekeo wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika utekelezaji wake wa majukumu katika kipindi hichi cha awamu ya saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyo chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa kitaifa 2011-2015 ni kama ifuatavyo:

(a) Kuweka mkazo mkubwa katika kutunza mazingira yetu na kuhakikisha kwamba uvunaji wa matumizi ya raslimali zisizorejesheka kama vile mchanga, udongo, mawe, kokoto na kifusi zinawekewa utaratibu ambapo kila mmoja wetu atapaswa kufuata kwa ajili ya kutumia raslimali hizo kwa matumizi endelevu na kuhifadhi mazingira. Tutaendelea kutunza na kuhifadhi mazingira ya nchi kavu na baharini ili kuendeleza bioanuai tuliyonayo ambayo baadhi yake ni adimu duniani.

Aidha, mkazo mkubwa tutauweka katika kupambana na uharibifu na uchafuzi wa aina zote za mazingira ikiwa ni pamoja na kushirikiana na washirika wa maendeleo katika kuandaa mikakati ya kujikinga na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

(b) Kusimamia na kutetea usawa, haki na fursa za watu wenye ulemavu ili kuhakikisha kwamba jamii yetu inakuwa jamii jumuishi. Kwa kufanya hivyo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na washirika mbali mbali itaandaa mkakati ili kuhakikisha kwamba masuala ya watu wenye ulemavu yanaingizwa katika mipango ya maendeleo.

(c) Kupambana na uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevya ili kunusuru afya za vijana wetu na kuongeza nguvu kazi ya taifa letu. Tutashajihisha jamii kuendelea kuzisaidia nyumba za makaazi za marekebisho zilizofunguliwa zinazowahudumia watumiaji wa dawa za kulevya sambamba na kukamilishwa kituo cha tiba na marekebisho ya vijana kinachojengwa Tunguu. Shabaha kubwa ikiwa ni kutoingiza wala kusambaza dawa za kulevya hapa Zanzibar.

(d) Kuendelea kudhibiti maambukizi mapya ya UKIMWI pamoja na kuondosha kabisa unyanyapaa katika jamii na kuhakikisha kwamba makundi yote yanapata hudumu bora za UKIMWI. Kazi hii itafanyika kwa kutekeleza mkakati wa pili wa kupambana na UKIMWI kwa kuzishirikisha sekta zote.

MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa ruhusa yako naomba sasa nieleze malengo kwa mwaka 2011/2012.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba ina jukumu la kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa upande wa Pemba.

MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

1. Kusimamia na kuratibu shughuli zote za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba.
2. Kuimarisha mazingira ya utendaji wa kazi.
3. Kujenga uwezo wa wafanyakazi.

Mhe. Spika, ili Ofisi kuu Pemba iweze kutekeleza majukumu yake, ninaliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi 135,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

IDARA YA MIPANGO, SERA, NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara hii ni mpya imeundwa kufuatia kuundwa kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar mapema mwaka 2011. Majukumu makubwa ya Idara hii ni kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, kukusanya na kutunza takwimu na kuratibu shughuli za utafiti kwa idara zote ziliopo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

1. Kusimamia na kuratibu shughuli zote za mipango, sera na utafiti katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

2. Kuweka utaratibu utakaowezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ndani na nje ya nchi kwa wepesi.

3. Kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo ya taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo

4. Kutafuta raslimali ambazo zitasaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

Mhe. Spika, ili Idara iweze kukamilisha majukumu yake iliyojipangia ninaliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 15,000,000 kwa matumizi ya kawaida na Shilingi 155,000,000 kwa matumizi ya shughuli za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, kama ilivyo idara ya Mipango vile vile Idara hii ni mpya imeundwa kufuatia kuundwa kwa Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais wa Zanzibar mapema mwaka 2011. Majukumu makubwa ya Idara hii ni kusimamia udhibiti wa bajeti, kushughulikia masuala ya ajira, haki na maslahi ya wafanyakazi pamoja na kuwapatia mafunzo.

MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

1. Kusimamia shughuli zote za uendeshaji na utawala.
2. Kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji wa kazi
3. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari.
4. Kuwajengea uwezo wafanyakazi.

Mhe. Spika, ili Idara iweze kukamilisha majukumu yake, ninaliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya shilingi 704,204,000 kwa matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

IDARA YA MAZINGIRA

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira inafanya kazi kwa kutekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira Zanzibar ya mwaka 1992 pamoja na sheria Na. 2 ya kusimamia mazingira endelevu ya mwaka 1996 na Kanuni zake.

Malengo makuu ya Idara ya Mazingira kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Zanzibar ni kukusanya na kuhifadhi taarifa za kimazingira, kutoa taarifa za kimazingira ili ziweze kusaidia katika kutayarisha na kutekeleza mipango ya kimaendeleo, kufuatilia mwenendo wa hali ya kimazingira ndani na nje ya visiwa vyetu pamoja na kuandaa utafiti wa kimazingira, kukabiliana na matatizo ya kimazingira na kuwahamasisha wadau kuchukua hatua za kuhifadhi mazingira na kutoa elimu ya mazingira kwa jamii.

MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2011/2012 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuongeza uelewa wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine.

2. Kuhakisha kwamba miradi ya maendeleo inazingatia vigezo vya utunzaji wa mazingira.

3. Kudhibiti uingizaji wa bidhaa chakavu zinazoharibu na kuchafua mazingira.

4. Kuendelea kuzuia uingizwaji na matumizi ya mifuko ya plastiki.

5. Kuandaa Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sera mpya ya Mazingira.

6. Kutekeleza mradi wa kuangamiza kunguru weusi hapa Zanzibar.

7. Kuandaa mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi *(climate change strategy)*.

8. Kuweka utaratibu mzuri wa uvunaji wa maliasili zisizorejesheka.

Mhe. Spika, ili Idara iweze kutekeleza majukumu yake iliyojipangia ninaliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi 239,158,000 kwa ajili ya shughuli za kawaida. Aidha Idara ya mazingira imepanga kukusanya jumla ya Shilingi 9,000,000 kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

IDARA YA WATU WENYE ULEMAVU

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Idara ya Watu Wenye Ulemavu mwaka 2008. Idara hii inafanyia kazi Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya 2004. Malengo ya Idara ya Watu Wenye Ulemavu kwa mujibu wa

Sheria ya mwaka 2006 ya watu wenye ulemavu ni Kuratibu, kuwezesha, kuelimisha na kutetea usawa wa haki na fursa kwa watu wenye ulemavu.

MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, Idara ya Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2011/2012 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuendeleza usajili wa watu wenye ulemavu kwa kupata taarifa zinazohitajika juu ya watu wenye ulemavu.

2. Kuongeza uelewa wa jamii, juu ya sera, sheria, na mikataba ya kimataifa ya haki za watu wenye ulemavu.

3. Kujenga uwezo wa Idara, Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar na jumuia za watu wenye ulemavu.

4. Kuratibu shughuli za Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar.

Mhe. Spika, ili Idara iweze kutekeleza majukumu yake, ninaliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi 177,995,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

TUME YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Spika, Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa ya Kulevya, ni moja ya taasisi iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Majukumu ya Tume ni kuratibu mapambano dhidi ya biashara na matumizi haramu ya dawa za kulevya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi, kuelimisha jamii athari za matumizi ya dawa za kulevya kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habarí, taaluma katika taasisi za elimu na sehemu za kazi na jamii kwa ujumla na kutoa huduma za ushauri nasaha pamoja na tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya.

MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

1. Kuwasilisha mswada wa marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar katika ngazi zinazohusika kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho.

2. Kuwajengea uwezo watendaji wa sekta ya madawa ya kulevya.

3. Kuendeleza upigaji vita dawa za kulevya.

4. Kuandaa Sera ya Madawa ya Kulevya Zanzibar.

5. Kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa watumiaji wa dawa za kulevya.

6. Kuziendeleza juhudi za taasisi zisizo za kiserikali (*NGO's*) zinazotoa huduma za makaazi na marekebisho kwa vijana wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya *(Sober Houses).*

Mhe. Spika, ili Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya iweze kukamilisha majukumu yake iliyojipangia, ninaliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 142,527,000 kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

TUME YA UKIMWI

Mhe. Spika, Tume ya UKIMWI ni taasisi ambayo imeanzishwa kwa Sheria No. 3 ya mwaka 2002. Ni chombo kinachojitegemea kilichopo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Majukumu makuu ya Tume ni kuratibu muitiko wa taifa wa kupambana na UKIMWI, kuzijengea uwezo taasisi zinazopambana na UKIMWI, kufuatilia na kutathmini muitiko wa taifa, kutetea masuala ya UKIMWI na kuandaa miongozo ya kitaifa ya kupambana na UKIMWI.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

1. Kutekeleza mkakati wa taifa wa pili wa kupambana na UKIMWI, kwa kuzishirikisha sekta za serikali, sekta binafsi na AZAKI katika ngazi zote.

2. Kuimarisha utekelezaji wa *programs* za habari, utetetezi na mawasiliano kwa ajili ya kuleta mabadiliko ya tabia kwa makundi yalio katika hatari zaidi ya kuambukizwa na jamii kwa jumla.
3. Kuimarisha mipango ya ufuatiliaji, tathmini na utafiti inayohusiana na shughuli za UKIMWI na maeneo yanayohusiana nayo na

4. Kuongeza uwezo wa Tume na wadau katika kuratibu, na kutekeleza shughuli za UKIMWI kwa mfuatano huo.

Mhe. Spika, ili Tume ya UKIMWI iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi 472,000,000/- kwa ajili ya shughuli za kawaida, na Shilingi 90,000,000/- ikiwa ni mchango wa serikali kwa ajili ya shughuli za maendeleo na Shilingi 1,300,000,000/-

ikiwa ni mchango wa washirika wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

SHUKRANI

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa kunisikiliza kwa utulivu na ustahamilivu wakati wote nilipokuwa nikitoa maelezo yangu.

Ni matumaini yangu kwamba Baraza lako tukufu litatoa mchango ambao utaisaidia ofisi yangu, kutatua matatizo ambayo yapo katika jamii hasa kwa yale makundi, ambayo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina wajibu wa kuyasimamia maslahi yake, na pia matatizo ambayo Ofisi ilikutana nayo katika utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha utekelezaji cha mwaka 2010/11.

Mhe. Spika, naomba nichukuwe fursa hii kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe wote, kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya ofisi yangu. Nathubutu kusema kwamba, mafanikio niliyoyaeleza katika hotuba yangu hii ni matokeo ya ushirikiano mkubwa wa wadau mbali mbali wa ndani na nje, na hivyo sina budi kuwashukuru wote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi marafiki na mashirika ya kimataifa, ambayo yameisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendeleza sekta mtambuka ikiwemo UKIMWI, Mazingira, sekta ya Madawa ya Kulevya na Ulemavu.

Nchi hizo ni pamoja na Marekani, Uholanzi, Finland, Norway, Brazil na Australia pamoja na mashirika ya Kimataifa ikiwemo *UNDP*, *UNICEF*, *UNFPA*, *UNAIDS*, *WHO*, *World Bank*, *UNODC*, *CDC*, *AIHA*, *ICAP*, *UNEP*, *UNFCC*, *TSF*, *Save the Children*, na nchi na mashirika mengine ambayo kwa njia moja au nyengine yanatuunga mkono katika shughuli zetu za maendeleo ambayo sikuyataja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa taasisi mbali mbali za serikali zikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama, taasisi zisizo za kiserikali na jumuiya za kiraia zinazojishughulisha na mapambano dhidi ya UKIMWI, kupiga vita madawa ya kulevya, utunzaji wa mazingira na kutetea fursa sawa kwa watu wenye ulemavu, kwa mchango wao mkubwa na mashirikiano yao katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. *(Makofi)*

Naomba nikiri mbele ya Baraza lako tukufu kwamba ushiriki, uwajibikaji, na umahiri wa wadau hawa, umewezesha kusaidia kupatikana ufanisi katika

utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yetu. Nawaomba waendelee kutupa mashirikiano hayo katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, shukrani za pekee zimwendee Mpiga Chapa Mkuu pamoja na wafanyakazi wote wa Kiwanda cha Upigaji Chapa kwa kufanikisha uchapaji wa hotuba hii, na wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha utekelezaji wa kazi za Ofisi yetu. *(Makofi)*

Mwisho napenda kuwashukuru wananchi wote kwa ujumla kwa kufanikisha kazi za maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

HITIMISHO

Mhe. Spika, shukurani za mwisho sio kwa umuhimu napenda kuzitoa kwa familia yangu na hasa mume wangu pamoja na watoto wangu, kwa kunivumilia kipindi chote ambacho ninapokuwa sipo na wao na kunipa ushirikiano ambao unaniwezesha kutekeleza vyema majukumu yangu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iweze kufanikisha kazi zake kwa ufanisi kama ilivyojipangia, naliomba Baraza lako tukufu sasa liidhinishe matumizi ya jumla ya Shilingi 1,573,000,000/- kwa mwaka wa fedha 2011/12. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,493,000,000/- kwa kazi za kawaida na Shilingi 155,000,000/- kwa kazi za maendeleo.

Aidha, ninaomba liidhinishe matumizi ya jumla ya shilingi 1,862,000,000/- kwa ajili ya Tume ya UKIMWI, ambazo 472,000,000/- kwa kazi za kawaida, shilingi 90,000,000/- kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa serikali na shilingi 1,300,000,000/- ikiwa ni mchango wa washirika wa maendeleo. (Tafadhali angalia kiambatanisho Nam.5).

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Waziri kwa kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Nakushukuru sana umetumia dakika 55. hoja imeungwa mkono hii ikiashiria kwamba sasa ijadiliwe.

Kwa taratibu zetu sasa naomba kumkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi ya Viongozi wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kabla ya yote

naomba uniruhusu kusoma taarifa ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Kwanza naomba uniruhusu nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar, pia nimpongeze Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kuwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais. Pia nimpongeze Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Naamini viongozi hawa Mhe. Spika, wataiongoza Zanzibar na kuiletea matumini mapya. *(Makofi)*

Vile vile naomba kumpongeza Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa wizara hii. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu ampe uwezo na amuwezeshe kuyatekeleza yote yanayohitajika, Amin. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba uniruhusu kusoma taarifa hii.

Mhe. Spika, taarifa ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu Kitaifa juu ya utekelezaji wa Bajeti kwa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia kukutana tena mbele ya Baraza lako tukufu, ili kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hii ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa rais 2011/2012 kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, aidha kwa niaba ya kamati nakushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, ili niwasilishe taarifa ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na Mapato na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka 2011/2012.

Mhe Spika, pili napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar ili kuwaongoza, tunamuombea kila la kheri katika kazi yake hiyo ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atamsaidia. Pia tunawapongeza kwa pamoja wasaidizi wake wakuu Makamu wa Kwanza na wa Pili wa Rais kwa kazi zao za kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa

ushirikiano na umakini wao wakati wa kuchambua na kujadili Bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Naomba niwatambulishe wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Salum Haji - Mjumbe
4. Mhe. Mgeni Hassan Juma - Mjumbe
5. Mhe. Mohammed Haji Khalid - Mjumbe
6. Mhe. Salma Mohammed Ali - Mjumbe
7. Mhe. Ussi Jecha Simai - Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu
9. Ndg. Ramadhan Kh. Masoud - Katibu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe Waziri ameelezea muundo wa Wizara yake hasa kwa kuwa Wizara hii ni mpya ambapo ni kama hivi ifuatavyo :-

- Ofisi Kuu Pemba;
- Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
- Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
- Idara ya Mazingira;
- Idara ya Watu Wenye Ulemavu;
- Tume ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya na Kurekebisha Tabia na
- Tume ya Ukimwi.

Mhe Spika, Mhe. Waziri ameelezea kwenye kitabu chake muelekeo wa bajeti ya wizara yake mwaka 2011/2012, ambao ndani yake unahusisha Utekelezaji wa Bajeti (matumizi ya kawaida na kazi za maendeleo) ya mwaka 2010/2011. Makadirio ya mapato yaliyopangwa yaliyotakiwa kuchangiwa na ofisi hii kwa mwaka 2010/2011. Maombi ya fedha ya Ofisi kwa mwaka 2011/2012.

Maoni na Ushauri wa Kamati Kuhusiana na Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2010/2011 na Mwelekeo wa Bajeti ya Ofisi ya Mwaka 2011/2012

Idara ya Mazingira

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia idara hii kwa jitihada zinazofanywa, ikiwemo ya upigaji vita uharibifu wa mazingira na ushajihishaji wa upandaji miti. Mbali na mafanikio hayo idara inakabiliwa na changamoto za ukosefu wa ushirikiano kutoka kwa wadau (viongozi, taasisi za serikali na wananchi).

Katika suala la uchimbaji mchanga na kifusi katika maeneo yasiyoruhusiwa rasmi na serikali na suala la kuwepo kwa gari za punda ambazo huchangia kuharibu mazingira. Hata hivyo, Kamati imeshauri yafuatayo kwa idara hii:-

- Idara ya Mazingira ishirikiane na Idara ya Misitu kuendeleza zoezi la upandaji wa miti kila mwaka kwa lengo la kutunza mazingira;

- Serikali ipige marufuku utumiaji wa misumeno ya moto kwa sababu inaendelea kuharibu mazingira kwa kiasi kikubwa. Hivyo kuwe na leseni maalum kwa yeyote atakaeruhusiwa kumiliki msumeno wa umeme na kila anapokwenda kutumia msumeno huo ni lazima apate kibali na muongozo wa Idara ya Mazingira;

- Idara ya Mazingira Pemba ambayo inamiliki honda moja tu kwa ajili ya kufuatilia shughuli za mazingira,inahitaji kupatiwa usafii wa kutosha, ili ifanye kazi zake kwa ufanisi;

- Jamii ikatae matumizi ya mifuko ya plastiki lakini pia jitihada za makusudi zinahitajika kuzuia uingizwaji wa mifuko hiyo hapa Zanzibar. Miongoni mwa jitihada hizo ni kuifanyia marekebisho Sheria ya Utunzaji Mazingira, ambayo inaonekana kutoa mwanya kwa waingizaji na watumiaji wa mifuko ya hiyo. Baada ya marekebisho hayo kunahitajika kuwepo kwa utekelezaji wa sheria hiyo, kwa yule atakayekwenda kinyume na sheria achukuliwe adhabu kali.

- Serikali izuie ukataji wa matofali huko Pemba hadi kutakapotolewa muongozo na kutayarishwa kanuni za udhibiti na utunzaji wa mazingira, ambapo hivi sasa hali ni mbaya sana kuna uharibifu mkubwa sana mazingira na sisi viongozi wanasiasa tunachangia eti vijana watafanya kazi gani hapa duniani.

  Kwa kweli zipo kazi nyingi za kufanya ambapo mtu atapata riziki bila ya kuhifadhi mazingira, ambayo huko mbele wakeshaacha mashimo makubwa na ardhi ikiwa haifai tena. Je, vizazi vijavyo wataishi vipi. Vile vile kama wazee wao walikata miamba kukawa na mashimo kama wanvyoyaacha hivi sasa wao wangeliridhika? Jamii ni lazima tuwaamshe kwani athari itakujakuwakuta wao wenyewe;

- Tunaitaka Wizara ya Miundombinu waache tabia ya kuchimba vifusi kwa miradi ya Ujenzi wa Barabara hasa inayofanywa na wafadhili bila ya kushauriana na kupata miongozo kotoka Idara ya Mazingira, ambapo wajenzi wakeshaondoka huacha mashimo makubwa, ambayo ardhi ile haiwezi kutumika tena.

  Hapa pia kuna kodi ya asilimia 10 inayotakiwa kulipwa Idara ya Mazingira, ambayo hailipwi na ndio maana hata unapotokea uharibifu wa mazingira kunakuwa hakuna nyenzo za kuhifadhi hali hiyo;

- Kamati pia inashauri idara kuainisha maeneo ya vianzio vya maji, ili kuvihifadhi visikatwe miti na kutoa mungozo wa upndaji miti inayosaidi kuongeza maji ardhini, ili kuzifanya chemchem zetu kuendelea kutoa maji kwa wingi na kwa muda mrefu na zisikauke.

- Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira ishirikiane na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Halmashauri na Mabaraza ya Manispaa kuimarisha mazingira ya usafi katika miji yetu.

Idara ya Watu Wenye Ulemavu:
Mhe. Spika, kamati vile vile inathamini jitihada zinazochukuliwa na Idara ya Watu wenye Ulemavu, katika kuwashajihisha na kuwaendeleza watu wenye ulemavu katika fani mbali mbali, na kuielimisha jamii kuhusu haki zao. Mbali na jitihada hizo kamati pia inashauri yafuatayo juu ya idara hii:-

- Kamati inaona kwamba suala la watu wenye ulemavu katika jamii linamgusa kila mtu wakiwemo viongozi wa majimbo na wengineo. Hivyo kuna haja kwa sisi Viongozi wa Majimbo kuhamasisha na kuwaendeleza watu wenye ulemavu kwa kuanzisha Ofisi za Walemavu katika majimbo, vile vile kuwatafutia misaada mbali mbali, ili kuwaendeleza kielimu na kimaisha.

- Kamati pia inakumbushia kuendelezwa elimu ya Watu Wenye Ulemavu katika jamii kuepuka unyanyapaa unaojitokeza.

- Kamati inasisitiza kutekelezwa kwa Sheria ya Ujenzi wa Majengo rafiki kwa walemavu, kwani inaonekana dhahiri kwamba wajenzi wengi hususan majengo ya serikali,

yanajengwa bila ya kuzingatia mahitaji ya walemavu. Kwa maana hiyo, kamati inaona kwamba kuna haja kwa sheria hiyo kufanyiwa marekebisho kwa yule anayejengewa, ambaye hatekelezi sheria hiyo, achuchukuliwe hatua kali za kisheria.

- Kamati vile vile inaishauri idara hii kuendelea kuwalinda na kuwahifadhi walemavu kwa kutoa elimu ya haki za walemavu katika jamii

- Mhe Spika, tunaiomba serikali kuongeza wafanyakazi katika Ofisi ya Bemba, kwani kuna uhaba mkubwa wa wafanyakazi. Tunaamini Pemba kuna walemavu wengi na ili idara kuweza kuwahudumia ni lazima kuwe na watendaji wa kutosha.

Tume ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya na Kurekebisha Tabia

Mhe. Spika, vile vile tuinaipongeza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Tume ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya na Kurekebisha Tabia, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kupambana na kudhibiti janga hili katika nchi yetu kwa kutumia njia tofauti, kama vile kutoa elimu kwa jamii kuhusu athari za matumizi ya dawa hizi pamoja na maambukizi ya virusi vya UKIMWI; Kushirikiana na Nyumba za Kurekebisha Tabia kwa kuwaendeleza kwa kuwapatia mafunzo vijana waliotayari kuachana na matumizi ya dawa za kulevya. Hata hivyo, mbali na jitihada hizo bado kuna changamoto zifuatazo kwa Serikali na Jamii:-

- Serikali kutokuwa na Nyumba za Kurekebisha Tabia kwa ajili ya kuwarekebisha vijana wanaomaliza vifungo vyao vya miezi sita Vyuo vya Mafunzo. Hali ambayo inawapelekea vijana hao kuhukumiwa kuendelea na vifungo ingawa ni kinyume na Sheria.

- Nyumba zilizopo kwa ajili ya kuwarekebisha vijana walio tayari kuacha kutumia dawa za kulevya ni haba na hazina vifaa vya kutosheleza katika kuwahudumia vijana hao. Vifaa hivyo ni kama vile magodoro na vile vya kusomea.

- Vile vile kuna changamoto kwa vijana hao baada ya kumaliza mafunzo yao katika nyumba hizo hupaswa karudi katika jamii. Pamoja na hayo, kuna baadhi yao kutokana na sababu mbali mbali hurudia kubwia dawa na kuviza malengo ya kuanzishwa kwa nyumba hizi lakini nchi yetu kuendelea kuipoteza kwa kasi nguvu kazi inayoitegemea.

Hivyo kamati inaendelea kusisitiza yafuatayo:-

- Serikali ichukue jitihada za makusudi za kujenga Nyumba za Kurekebisha Tabia kwa Vijana wanaoamua kuacha madawa ya kulevya na wale wanaomaliza kutumikia muda wao Vyuo Vya Mafunzo kama inavyoelekeza sheria.

- Vijana wanaomaliza muda wao katika Nyumba za Kurekebisha Tabia, wapatiwe mafunzo ya kazi za amali katika Vyuo vya Amali vya Serikali, ili waachane na kurudia kubwia dawa lakini pia wapate kujitegemea pale watakapomaliza mafunzo. Hivyo, ni muhimu kwa mazungumzo kati ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wizara ya Kazi na Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi zikazingatia suala hili.

- Kuna umihimu wa kuongezeka Nyumba za Kurekebisha Tabia, kwani zinaisaidia serikali na jamii kwa ujumla. Vile vile tuzingatie kuzisaidia nyumba hizo kwa kuwapatia vijana masuala ya msingi wanayoyahitaji.

- Kamati vile vile inaishauri Tume ya Kupambana na Madawa ya Kulevya kushirikiana na jamii pamoja na polisi katika kudhibiti janga hili la madawa ya kulevya.

Mhe Spika, tunaliomba Jeshi la Polisi kutoa mashirikiano ya kutosha na Polisi Jamii pale wanapowakamata wauza bangi na madawa ya kulevya wasiwapatie dhamana, kwani wanapopatiwa dhamana huanza kufanya vitendo vya rushwa. Kwa mfano, ni juzi tu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi alilaani vikali jambo hili inafaa tumuunge mkono sote.

Lakini kwa upende wa Mahakama na wao jamii inapohamasika kwa kuwakata wahalifu hawa huwa wanawaachia na kusema hakuna ushahidi wakati wamewakamata wananchi, hapa wananchi huvunjika moyo na kuwarejesha nyuma katika kushirikiana na wito wa Jeshi la Polisi kuanzisha Polis Jamii.

Tume ya UKIMWI

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza Tume ya UKIMWI kwa jitihada inazozichukuwa katika mapambano dhidi ya maradhi hatari ya UKIMWI. Tume katika mapambano hayo huwaelimisha wananchi mbali mbali masuala ya kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI kupitia vyombo vya habari, majarida pamoja na kuandaa filamu fundishi zinazohusu UKIMWI.

Kwa upande wa Tume ya UKIMWI kamati inashauri na kukumbushia yafuatayo:-

- Serikali ni vyema ikaongeza fungu katika bajeti ya Tume ya UKIMWI, ili iweze kufanya shughuli zake kwa ufanisi. Kwani kipindi kirefu imekua ikitegemea zaidi fedha za Washirika wa Maendeleo, ambao mitazamo yao kwa nchi zetu hua haitabiriki. Kwani kwa hivi sasa kwa muda mrefu tume imejitahidi kutoa elimu, ambayo imesaidia kwa kudhibiti maambukizi mapya kwani bado maambukizi yamebaki kwa asilimia 0.6 hii ni hatua nzuri ya kupigiwa mfano.

  Lakini hebu tujiulize iwapo Washirika wa Maendeleo wakiamua kwa makusudi kuacha kutusaidia ni kweli tume itaweza kumudu gharama za uendeshaji? Kwa hivyo, hili ni suala la kujiuliza kwa serikali yetu nini cha kufanya, ili kuhakikisha kuwa tunaendeleza namna ya kujikikinga na maambukizi mapya.

- Tume na jamii kuongeza kasi ya utolewaji wa elimu ya UKIMWI, ili kupunguza unyanyapaa unaoendelea kujitokeza hasa sehemu za vijijini.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kamati yetu inaishauri serikali kuweka mikakati katika ugawaji wa mafungu kwa kila idara kwa kuangalia hali halisi ya idara husika, ili ziweze kufanikisha malengo yaliyojiwekea katika kipindi chote cha mwaka wa fedha kwa maslahi na maendeleo ya nchi yetu.

HITIMISHO

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa mara nyengine kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati mbele ya Baraza lako tukufu. Pia naomba Waheshimiwa Wajumbe waichangie, ili kuiboresha na waipitishe bajeti hii bila ya pingamizi zozote. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwisho napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza kwa kunisikiza. Kwa niaba ya kamati naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamu Mwenyekiti. Sasa tuendele kwenye uchangiaji wa jumla. Waheshimiwa Wajumbe, nikumbushe ratiba ya kumaliza shughuli hii ni kesho kipindi cha asubuhi. Kwa hivyo, tupange points zetu vizuri, ili tuwasilishe maoni yetu kwa ajili ya kuchangia bajeti ya wizara hii na hatimaye kumaliza kupitisha kesho saa za mchana.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa mwanzo katika Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nianze katika suala zito ambalo ni mazingira. Katika hotuba ambayo nilikuwa nikiisikiliza hapa iliyosomwa na Mhe. Waziri ilikuwa inaelekeza zaidi katika namna ya kukabiliana na mambo ambayo yapo mbele yetu. Lakini nilikuwa nikijitahidi sana kusikiliza kwa makini kama yale maeneo, kuna mambo ambayo tayari yamekwisha kuathirika katika mtandao huu wa kimazingira yatakuwa yanaelezewa vipi kwa bahati mbaya sikusikia.

Katika jimbo letu la Kikwajuni sisi ni waathirika wakubwa sana wa masuala haya ya maziangira katika maeneo ya Zanzibar hii yote kwa ujumla. Eneo la Kikwajuni hususan katika eneo la shehia za Kilimani nilitarajia labda kutokana na umuhimu na uzito wa masuala ambayo yanatukabili.

Nilitegemea kuona namna gani Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake watakuwa wamejipanga katika namna ya kuona yale matatizo ambayo yanatukabili na namna ambayo kuna hatua gani ambazo zimepangwa na serikali katika kuyatatua na kuweza kuona kwamba tunayanusuru janga kubwa ambalo tunahisi wakati wowote linaweza kutokea katika Zanzibar yetu kwa ujumla.

Lakini hilo katika hotuba hii hatukuona maeneo hayo na matatizo yetu katika eneo lile la Jimbo la Kikwajuni ni makubwa na yanaeleweka kitaifa. Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri amaeneo haya na matatizo ambayo tunayo katika jimbo letu la Kikwajuni ayaangalie kwa umakini zaidi na aangalie namna gani anaweza kutusaidia ili kunusuru nchi kwa ujumla iweze kunusurika na majanga haya.

Eneo la pili ambalo nilikuwa naliangalia kwa makini ni eneo la madawa ya kulevya. Mhe. Spika, nikitizama katika ukurasa wa thalathini na moja Mhe. Waziri hapa alikuwa akizungumzia suala la kazi za kuelimisha na kushajihisha jamii juu ya athari ya madawa ya kulevya, lakini nikiangalia sekta hii na nikiangalia bajeti ambayo imetengwa kwa ajili ya suala hili naona bado suala hili halijapewa kipaumbele kinachostahiki.

Mhe. Spika, serikali yoyote duniani inakuwa inaongozwa na kujengwa na mambo matatu makubwa, tulisema kwanza tuwe na uongozi bora, tuwe na rasiliamali watu lakini tuwe na utawala bora vile vile, vijana wengi ambao tunao sasa hivi wameathirika na madawa ya kulevya, kuna hatari ya kuja kuongozwa na vijana ambao watakuwa na athari hizi za madawa ya kulevya.

Sasa nikiangalia katika bajeti yetu hii suala hili la madawa ya kulevya limepewa kipaumbele namba nane huko liangaliwe vizuri na tuone kwamba wenzetu wanajitahidi na kuonyesha nia ya kweli na kuwasaidia hawa vijana wetu ambao wanaharibika kwa wimbi kubwa sana.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kuchangia ni suala la ulinzi katika aya ya 49 ya hotuba ambayo Mhe. Waziri ameizungumza kifungu c) tunasema kwamba kupambana na uingizaji na uitumiaji wa madawa ya kulevya, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imetengeneza utaratibu mzuri na makini sana katika kuhakikisha kwamba inaimarisha ulinzi katika maeneo yake.

Vile vile kuna watu wa namna tofauti na maeneo tofauti wamesomeshwa hawa kwa pesa nyingi za walipa kodi kwa sababu ya kwenda kutimiza wajibu wao kwa maeneo husika. Cha kushangaza ni kuona kwamba tunao vijana hata polisi vile vile kwa ajili ya kuzuia madawa ya kulevya haya, lakini utaratibu wa kupekua pamoja na udhibiti wa kuangalia namna ya mizigo inayoingia na kutoka kidogo unatilia mashaka.

Kusema kweli watu ambao wanadhibiti maeneo yale kwa ajili ya kuangalia mizigo inayongia na kutoka ni watu wa Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu watu ambao uwezo wao wa kutambua matatizo ya madawa ya kulevya ni mdogo mno, namuomba Mhe. Waziri hili waliangalie kwa kina na wahakikishe kwamba wanalifanyia kazi na utaratibu unaostahiki.

Baada ya maelekezo haya kwa heshima na taadhima na kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkon hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsanta sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia bajeti hii ya Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kutuweka hai na kutupa uzima na tukaweza kuzungumza katika Baraza lako tukufu. Pili namshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake iliyochukua kama dakika 55 kama ulivyosema lakini iliyoeleza mambo karibu yote.

Kwanza kwa sababu tupo katika Afisi za viongozi wetu hatuna budi kuwapongeza lakini sisi tunaoamini mambo ya dini kupongeza haitoshi ila tunawaombe dua, Mwenyezi Mungu awaongoze na awape toufiki ya kutuongoza sisi ili kuweza kutuletea manufaa katika nchi yetu. Dalili nzuri kama nilivyosema mwanzo zimeshaonekana na tunawaomba wachukue njia hiyo hiyo ya kutuletea manufaa kwa nchi.

Mhe. Spika, Afisi hii ya Makamo wa Kwanza wa Rais naona kama ni msingi uliochukua taka taka zote na kupelekwa katika Afisi hii, haya mambo matatu ni mazito sana na wataalam wengi wanaohudumia wanasema ndio *detainment sector* ya maendeleo au umasikini wan chi, kwa hivyo nawaomba sana Mhe. Waziri atizame majukumu haya matatu kwa upeo wake.

Nikianza kuna suala la mazingira wataalam hawa wanaotuzidi sisi wanasema kwamba mazingira ukizungumza tu lazima uwe na sera, inayokuonyesha dira wewe ya wapi unakoelekea. Mhe. Waziri ametutajia hapa kwamba wanatumia sera ya 1992, mimi nilikuwa nimuulize tu inatosheleza kwa haja ya mambo yalivyo hivi sasa, ingawa katika kifungu kimoja kulionyeshwa dalili lakini maneno yamepandana kidogo.

Katika ukurasa wa 26 wa hiki kitabu alisema kuandaa mpango wa mkakati wa utekelezaji wa sera mpya ya mazingira, nilifahamu kwamba wanayo nia labda lakini kama kwamba utekelezaji unakuja mbele sera mpya haijapatina, basi nafikiri mwanzo ingekuwa kuandaa mikakati ya upatikanaji wa sera mpya na utekelezaji wake ikiwa ndio nilivyofahamu mie, laa ipo iyo sera mpya mimi sikuifahamu basi namuomba Mhe. Waziri akija aje atufafanulie, kwamba ipo sera mpya au wanaandaa mkakati wa kupata hiyo sera mpya pamoja na utekelezaji wake.

Mhe. Spika, tukija katika sera wataalam wanasema kwamba ukizungumza tu utekelezaji au sera ya kimazingira ni hatua zilizochukuliwa kwa makusudi hii ndio sera hasa na ndio maana yake kwa mazingira, mbinu zilizochukuliwa kwa makusudi za kuweza kuzishughulikia taratibu zote za kibinaadam ambazo zingeweza kuzuia au kupunguza athari za kimaumbile au athari zinazoweza kupatikana kwa mali asili, hiyo ndio sera ambayo inatakiwa ipatikane. Sasa basi sisi nafikiri jambo la mwanzo kabisa ingelifanya hii wizara mpya ya Makamo wa Kwanza wa Rais ni kufanya tathmini ya athari gani zilizopatikana kwa sababu athari tayari zipo. Tukishaweza kujua athari gani zilizopatikana katika kila hali kwa sababu yapo maeneo mengi yaliyotajwa katika utaalam wa mazingira, maeneo ya bayaanuwai sijui, maeneo ya ukusanyaji wa taka taka, maeneo ya taka taka za viwandani, maeneo ya utunzaji wa rasilimali maliasili misitu, mali zisizohamishika na mali zinazohamishika maeno yote hayo wataalam wanayajua ni kufanya tathmini.

Kwa hivyo mimi nafikiria bajeti ambayo wametoa au wamepewa ni ndogo sana kwa sababu kufanya tathmini ni jambo ambalo lina gharama kubwa, hatuwezi kupanga sera bila ya kufanya tathmini ya matatizo yetu lazima tufanye tathmini ya matatizo yetu tuliyokuwa nayo halafu tuweze kupanga sera tujue mwelekeo wetu.

Mhe. Spika, nikija hapa kwenye malengo ukurasa wa 26 sikuona mimi kama fukwe zimeingizwa katika mazingira, kwa sababu sisi ni visiwa tena vidogo fukwe zinachukua nafasi kubwa katika uhifadhi wa mazingira yetu, hizi lazima zipewe kipaumbele nafikiri Mhe. Waziri amesahau tu kwa sababu juzi leo ya tatu tu nilikuwa namsikia akizungumza kuhusu maeneo yanayoingiliwa na maji chumvi ya mashamba ya watu ambao wanalima, sasa sijui kwa nini leo kasahau kuliingiza. Kwa hivyo mimi nahisi sehemu za fukwe ni muhimu na kuingizwa katika mazingira.

Lakini kifungu namba 8 cha yale malengo ya Idara hii ya Mazingira kidogo Kiswahili hiki mimi kinanifanyia matata, kwa sababu kitu chochote kikivunwa huwa kimeshatimia umri na kiko tayari, sasa unaposema mchanga unavunwa umri wake ni miaka mingapi, na huu ulipandwa lini sasa kidogo hebu tutumie maneno ya Kiswahili fasaha. Juzi yalikuwa yanauzwa makamusi sanifu hapa nafikiri tungemshauri Mhe. Waziri akapata moja hili.

Mchanga unakuwa unachotwa au unachukuliwa, ukimwambia mtu asivune mchanga nae ni mwanafunzi kesho kwenye bonde la mpunga utamwambia vipi asichote mpunga *(Kicheko)* tutumie Kiswahili ambacho hata wale watu tukiwafahamisha kwenye hii elimu ya mazingira wakafahamu tunachowambia.

Mhe. Spika, kuna kitu kinaitwa *Environmentally infect assessment* hii wanafanya hawa watu wa vitega uchumi ili kuona kwamba miradi yao inakwenda sambamba na yale mazingira ambayo yapo pale na yanaruhusu, mimi nahisi kutonana na kazi ambazo tumekuwa nazo za kamati tokea kipindi cha kwanza mpaka hivi sasa nahisi kuna wajibu na haja ya kutizama namna gani Idara hii ya Mazingira inavyofanya hii *environmentally infect assessment* anastahiki kupewa. Kuna haja ya kuikuza hii *environmentally infect assessment* yaani tathmini ya kimazingira, kwa sababu tumeshawahi kwenda sisi tukasikia kwamba kaachiwa yule mwenye mradi kuleta kampuni tatu za kufanya zile *environmentally infect assessment* halafu wle watu wa mazingira wachague moja katika zile, sasa sisi watu wa mazingira ndio tulikuwa tunahitaji kufanya ile.

Kwa nini hatuwi na mashirika yetu au kampuni zetu halafu tukamchaji yule ambae anataka kufanya lile badala ya kuwambia wewe lete tatu halafu sisi tuchague moja, hata hivyo utaalam upo lakini mimi nasema jambo hili liangaliwe ili tusije tukapata malalamiko ya kazi mbili, ikawa mmoja ameshafanya huyu unamwambia hii haikuwezekana nah ii inaleta bughudha wakati mwengine kwa wale watu wa vitega uchumi, kwa sababu mtu anakuwa ameshajitayarisha kanuni ndio zinasema hivyo anapofanya ile wengine huko huko wanaizuia wanasema hatuiamini.

Sasa mimi nafikiri tukubaliane *wan way only* ya kufanya *environmentally assessment* Idara ya Mazingira wenyewe watayarishe wataalam wao ambao kama ni kiwanda kama nini wanajua kwa kupata, *consultancy* ziko nyingi siku hizi unapobonyesha tu kifungo wanatoka wenyewe, hili nafikiri ndio linapaswa kurekebishwa.

Mhe. Spika, kwa sababu mazingira na mambo yote ambayo yamo katika Afisi hii ni yale ayanayoitwa *cross courting issue*s mambo mtambuka, hilo kamusi linasema mambo mtambuka, sasa kwa sababu ni mambo mtambuka sijamsikia Mhe. Waziri hapa akisema kwamba ni vikao gani anafanya na wadau wa Mawizara au watu binafsi kuona kwamba haya mambo yanafanikiwa. Kwa sababu ni sawa sawa na ile Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais sasa ni *wan stop centre* ya mazingira, yaani watu wa ujenzi wawepo pale, watu wa miundombinu, watu wa nishati, watu wanaoshughulikia uvuvi baharini ndio Ofisi yao kwa maana gani ni kwa Afisi ya Uratibu wa mambo hayo yaliyotajwa.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa sababu sasa ni mpya lakini mwaka ujao tunamuomba sana Mhe. Waziri akileta ripoti yake atwambie hasa vikao vingapi walifanya na Idara fulani na fulani kuhusu *situation* hii, vikao gani walifanya na wizara fulani fulani kwa *situation* hii iliyojitokeza, uende na changamoto zilizojitokeza. Hivi sasa mvua tunayopata ni ndogo sana Zanzibar na hasa Unguja Pemba imezidi kidogo mvua lazima kutakuwa kuna athari za mazingira ambazo zimesababishwa nah ii, sisi tunazihitaji sana hizo mvua.

Moja katika mradi mkubwa wambao umo kwa hawa wafadhili ni uvunaji wa maji ya mvua

Mhe. Spika: Mheshimiwa itabidi uelezee yana umri gani.

Mhe. Raishid Seif Suleiman: Kwa hivyo Mhe. Spika, tunamuomba sana Mhe. Waziri pamoja na mambo yote lakini watizame mabadiliko ya hali ya hewa kuona na sisi hatuhusiki katika mabadiliko haya ya hali ya hewa kutokana na mazingira yetu kubadilika, minazi inakwenda kwa wingi sana. Mimi juzi siku ya Jumamosi nilibahatika sana kwenda soko kuu la Mwanakwerekwe, miaka kama mitano au kumi iliyopita nazi iliyokuwa ikiuzwa Unguja leo asilimia ishirini ya saizi ya nazi ile ndio inauzwa kule sokoni, nazi ndogo mimi niliitizama kwa kitu cha upeo kabisa hapa ndipo palipokuwa pakitoka nazi kubwa kabisa Unguja, lakini leo wachilia mbali ya ule wingi hata ile mbuzi yake iundwe mbuzi makusudi sasa kwa ajili ya kukunia nazi zile tu sio zile tunazotumia mini mbuzi. Kwa hivyo haya ni mambo ya kuyatizama kwa nini tunakwenda hivi.

Mhe. Spika, kwa sababu suala la mazingira linaniumiza sana hali tunayokwenda nayo lazima tufanye tathmini tusiende hivi hivi visiwa vyetu vitatupotea na sisi tutavitizama hivi hivi tu.

Mhe. Spika, napenda kuzungumza kidogo kuhusu madawa ya kulevya hii ni msimba Mhe. Spika, kwamba sisi watu wote duniani watatustajabia kwa idadi ya watu wetu tuliyokuwa nayo tukashindwa kuzuia madawa ya kulevya, kwa sababu jambo ambalo liko huko duniani ni ule wingi wa watu na makaazi yao na tamaduni zao zilizokuwa tofauti. Kwa mfano Marekani kule kila kabila duniani lipo na linaishi vile vile linavyoishi kwao. Wachina wana miji yao, wahindi wana miji yao na tamaduni zao zile zile walizokuwa wakiishi kwao, vyakula vyao ni vile vile. Hapa sisi ni watu wenye utamaduni mmoja wenye lugha moja, sura zetu zinafanana itakuwaje tusijuane kwamba huyu anaagiza madawa ya kulevya na huyu haagizi.

Mhe. Spika, unakumbuka ililetwa sheria hapa mwaka 2009 kama hivi ya madawa ya kulevywa wakati ule mimi nilikuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya, kuna ile sheria iliyoletwa na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa wakati ule kwa hivyo ikabidi nifanye utafiti kidogo na mimi niweze kutoa msemo, niweze kusema chochote katika Baraza. Mimi niligundua kutokana na matatizo ya ndani ya serikali ya Zanzibar na Muungano kwamba wakubwa wanalindwa kuleta madawa, tusiwatafute tutamalizika Mhe. Spika.

Mwisho kabisa naomba hao walioathirika basi hiki kitengo chako kifanye kazi ya kweli kweli hizo nyumba zisaidiwe kikweli kweli, na kama kuna kitu ambacho mmeshakitayarisha na sisi mnataka mchango wetu twambieni wazi wazi lakini kuwe *seriousness*, tulipata semina moja Mhe. Spika, ya namna ya fedha zinavyowafikia walengwa wale waliotupa semina na shukuru ni semina hii hii ya Baraza lakini waliona fedaha zinazowafikia walengwa ni *ten percent* ya fedha iliyotoka mwanzo. Sasa hivi nyumba tuzipe kweli hii misaada yetu isiwe huko kwenye Wizara inaandikwa *ten million* lakini wakipelekewa wale wanapewa laki mbili hivi tutakuwa hatufiki, wale wamefanya *research* na wameona kwamba pesa nyingi zinazotolewa kwa ajili ya walengwa kama hao ni *ten percent* inayowafika wenyewe hapo kati kati kila mmoja anachukua fungu lake, tokea mkubwa mpaka kufikia kwa Mhasibu na yeye anatoa yake.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na naunga mkono bajeti hii mia juu ya mia na ishaalla kila la kheri. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na kabla sijaendelea naomba niseme kwamba kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo linalovutia kuliko yote Jimbo la Mji Mkongwe tunaunga mkono bajeti ya Afisi ya Makamo wa Kwanza wa

Rais, ambayo bahati nzuri Mhe. Waziri ni mmoja katika wapiga kura wake wa jimbo hili la Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, pili nichukue nafasi hii kumpongeza Makamo wa Kwanza wa Rais kwanza kwa kuteuliwa kwake kushika nafasi hii na pili kwa umahiri mkubwa anaouonyesha katika kuongoza Ofisi hii, mbali ya yale majukumu yaliyotajwa katika kutawala lakini pia katika kuteleza majukumu yake akiwa kati ya wasaidizi na washauri wakuu wa Rais yeye pamoja na Mhe. Balosi Seif Ali Iddi Makamo wa Pili wa Rais. Tuna imani kwamba watafanya kazi nzuri ya kumsaidia Mhe. Rais ili yale malengo ya kuendeleza nchi yetu yaweze kufikiwa.

Mhe. Spika, sasa naomba niende moja kwa moja katika shughuli za Ofisi hii na naomba na mimi nianze katika suala la mazingira, haihitaji kuelezwa zaidi kuliko umuhimu ambao ameueleza kwa ufasaha mkubwa Mhe. Rashid Seif juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira katika nchi yetu hasa tukizingatia kwamba sisi ni visiwa kwa hivyo athari ndogo tu zinaweza kupelekea janga kubwa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hakuna eneo la Zanzibar ambalo halikuathirika na hata jimbo la Mji Mkongwe nalo halikuweza kukwepa athari za uharibifu wa mazingira. Ukitembea maeneo ya fukwe hasa katika eneo la Bandari mpaka Ras-el-Khaima ukenda kule utakuta kuna uharibu mkubwa wa mazingira.

Lile aneo ambalo sasa hivi kuna chelezo pia kuna sehemu wanapokea samaki. Ukifika pale huwezi kuamini kama unaweza kula samaki ambaye kuwa anapitishwa katika mazingira yaliyokuwepo pale. Kwa hakika ile hali inaweza kukuchefua na huwezi kuamini kwamba tunakaribisha maradhi katika nchi yetu.

Lakini hata lile eneo lilokuwepo karibu na Hoteli ya Bwawani, mpaka lilitembelewa na Makamo wa Kwanza wa Rais ndipo pakachukuliwa hatua baada ya agizo lake kwamba pasafishwe. Lakini sina hakika kama baada ya agizo lile la kusafishwa kama utaratibu ule unaendelea tena. Hili ndio moja katika matatizo yetu makubwa kabisa. Mara nyengine watendaji wetu wamekuwa wanatekeleza maagizo pale linapotoka agizo la mkubwa tu.

Kama sasa hivi tunavyoona mji wa Zanzibar watu wamejitahidi kwenda mbio huku na kule baada ya agizo la Mhe. Rais lakini hatuna hakika kama utaratibu ule utadumu kiasi gani. Kwa hivyo nilikuwa naomba hili nalo pia tusaidiwe, Idara hii ya Mazingira imejipanga kiasi gani kusaidia kusimamia maeneo kama yale, kuona kwamba sio tu kwamba mpaka apite mkubwa ndio mazingira

yasafishwe au yatunze. Kuwe kuna utaratibu unaoendelea, unaoeleweka wa kuhakikisha kwamba masuala ya mazingira yanatunzwa.

Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa tusizungumzie Mji Mkongwe, suala la mazingira ni suala muhimu kwa upana wake katika Zanzibar nzima. Pametajwa hapa athari katika maeneo ya uchumbaji wa matofali na kuipasua miamba. Pametajwa masuala ya kuchimba michanga, kuchimba vifusi, kote kunaleta athari kubwa.

Lakini pia na suala zima la ukataji wa miti ovyo ambao kuwa unaendelea. Alizungumza Mhe. Rashid hapa suala zima la ukataji wa minazi mpaka leo tumeathirika. Nchi ambayo ilikuwa ikisifika huko nyuma, mpaka alama ya utambulisho wa Zanzibar ilikuwa ni mkarafuu na mnazi. Leo mnazi unapotea na sijui kama tutakuwa tuna haki ya kuendelea kuutumia kama ni alama yetu katika visiwa vya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niseme kwamba mimi napata wasi wasi juu ya serikali udhati na ukweli wake katika kusimamia suala hili la mazingira au ni kauli za kisiasa tu. Kwa sababu nilipokuwa nikimsikiliza Mhe. Waziri na kipindi nilipotoka nimekuja kukipitia kitabu chake katika ukurasa wa 12 napata mashaka kidogo. Kimeandikwa kwamba mpaka kufikia mwezi wa Juni 2011 Idara ya Mazingira imeingiziwa asilimia 19.14 tu ya makisio yaliyokuwa yamepitishwa kwa mwaka uliopita.

Mhe. Spika, huku tunasema na tunaimba kila wakati kuhusu mazingira. Lakini kiwango chote kilichoingiziwa idara hii tunaambiwa ni *cross cutting* inaingia kila pahala. *Are you serious* Mhe. Spika*?* Au tunapiga siasa tuonekane na wananchi wetu kwamba tunajali lakini kwa hakika ikija katika utekelezaji hali halisi haioneshi hivyo. Hili baadaye nitakuja kulieleza kwa sababu inaonesha si katika idara hii, inaonekana ni idara nyingi zilizokuwepo katika ofisi hii uingizaji wa fedha ipo chini ya asilimia 50. Lakini hili la mazingira limenipa mshtuko mkubwa sana.

Jengine katika hilo hilo la mazingira tulitegemea idara hii kupitia Afisi ya Makamo wa Kwanza au hata huko nyuma ilipokuwepo katika Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mazingira. iwe ndipo pahala ambapo pana *coordination* na masuala yote ya mazingira na utunzaji wake.

Mhe. Spika, asubuhi ya leo tumeshuhudia hapa, tuna wasi wasi wa *coordination* wa uratibu wa shughuli hizi. Mhe. Mhammed nafikiri aliuliza suali kuhusu uingiaji wa vifaa vichakavu. Naibu Waziri wa Biashara akatujibu suali lile lakini ikabidi anyanyuke Waziri kuja kutoa maelezo ambayo kuwa inaonekana Naibu Waziri hakuwa akiyajua. Nafahamu serikali hapa kwa umoja

wake inawajibika hapa kwa pamoja. Nilitegemea atakapokuja kujibu suala kama lile linalohusu mazingira, Haizuru linahusiana na biashara lakini angalau ange *consult* na ofisi inayohusika na mazingira. Hapo inatupa picha kama vile hakuna uratibu wa shughuli hizi katika serikali. Na tunaweza kuhoji umakini mzima wa masuala haya ya kusimamia mazingira. Waziri akija atupe majibu kuhusu masuala haya.

Nimalizie na suala la mazingira katika nukta nyengine. Ninapoangalia ukurasa wa 26 wa hotuba ya Mhe. Waziri kuna nukta 8 pale alizozitaja kama ni maeneo ambayo yamepangwa kutekelezwa katika mwaka unaokuja wa fedha unaoanzia mwezi wa Julai. Najiuliza tena ile *serioussness* ya suala hili. Ninapoangalia kitabu hichi chenye makadirio nikenda katika shughuli za maendeleo ukiangalia Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, maeneo yaliyotajwa ni mawili tu. Lile la tatu silitii hisabuni linalohusu programu ya uimarishaji wa nyumba za viongozi.

- Kuna mitego ya kunguru milioni 50 ambayo inawiyana na hoja Nam.6 ambayo imetajwa hapa kutekeleza mradi wa kuangamiza kunguru weuzi hapa Zanzibar.

- Mradi wa Usimamizi wa maji taka milioni 30.

Najiuliza Mhe. Spika, haya mengine yaliyotajwa hapa yatapata wapi fedha za utekelezaji wa miradi yake. Au ndio yale yale kwamba tunapanga mipango ambayo hatukusudii kuitekeleza kwa sababu inapokuja katika uingizaji wa fedha hayapo. Haya itakuwa ni ya ghasi ya mwaka uliopita, kwa sababu sio tu kwamba hayatoingiziwa fedha, lakini hata kutengewe hizo fedha hatuzioni hapa. Nilikuwa namuomba Mhe. Spika, atakapokuja Mhe. Waziri katika hili atusaidie.

Mhe. Spika, nije katika suala la pili la Ukimwi. Hili pia ni suala muhimu sana. Tunajua kwamba nchi yetu inaafadhali ukilinganisha na nchi nyengine. Lakini hiyo haitupi sababu ya kutopambana nao ili ikiwezekana tuutokomeze kabisa katika visiwa vyetu.

Mhe. Spika, hapa nataka kuuliza Mhe. Waziri akija atusaidie, kiasi gani Tume ya Ukimwi inahusika katika kuangalia pamopotekelezwa mambo tofautia katika nchi yetu kuona kwamba hakuna vishawishi ambavyo kwamba vitapelekea kuongezeka kwa maradhi ya ukimwi.

Mhe. Spika, Zanzibar siku hizi katika kutangaza utalii imekuwa maarufu katika kuleta mambo ya matamasha na mambo mengine mbali mbali na mengine ambayo zamani yalikuwa ni shughuli za watu wa jamii fulani tu. Kwa mfano

Mwaka Kogwa kule kwetu mimi na wewe Mhe. Spika, Makunduchi. Sasa imekuwa ni tamasha *almost* la kitaifa. Ni kiasi gani Tume ya Ukimwi inafatilia kuona matamasha kama haya hayapelekei kuongezeka kwa Ukimwi wakati yanatuongezea fedha za utalii lakini yanatuletea janga jengine.

Mhe. Spika, hapo hapo katika suala la Ukimwi nataka kuulizia kwamba kiasi gani tunaviangalia vyombo vya habari na hasa vya serikali, kwamba vipindi vyake havisaidii kushajihisha zinaa na mambo mengine yanayokwenda kinyume na maadili yetu ambayo hatimaye yanapelekea kuongezeka kwa maambukizo ya maradhi ya Ukimwi.

Mhe. Spika, huko tunakotoka Idara ya Televisheni ilikuwa hodari sana katika kuchunga vipindi hivyo lakini siku hizi naona kama kuna kuzembea. Sijui kiasi gani Tume ya Ukimwi inahusika katika kuona mambo kama haya ili kupunguza maambukizo mapya.

Mhe. Spika, nikija katika fungu la pesa, vile vile nimepata mshtuko nikiangaliia bajeti ya Tume ya Ukimwi. Unakuta katika bajeti ya maendeleo kuna milioni 90 kutoka katika vyanzo vya ndani. Misaada kutoka nje ni bilioni moja na mia tatu bilioni, jumla bilioni moja mia tatu na tisini milioni. Tukajiuliza hebu waziri akija atwambie kuna shughuli gani hapa? Kuna ujenzi au kuna mradi gani wa maendeleo.

Nauliza haya Mhe. Spika kwa sababu watu wengi wamekuwa wakipiga kelele si kwetu tu. Kwamba miradi hii siku hizi mara nyingi imekuwa inatumika kuendeshea semina na warsha ambayo huwa inapelekea fedha nyingi kupotea huko, kuliko kama alivyosema Mhe. Rashid kuwafikia walengwa.

Mhe. Spika, Zanzibar kuna Chama kinaitwa *ZAPHA PLUS* au jumuiya ya wanaoishi na virusi vya Ukimwi na walioathirika. Sijui kiasi gani kinasaidiwa, ukiangalia hali yake imefikishia kuwa omba omba, kwa kila anayetembelea pale. Je, fedha hizi zinawasaidia watu hawa au zinaishia kama tulivyosema kwenye warsha, makongamano, semina, mikutano na katiba ya Afro, mpaka tunafika pahala unajiuliza kweli fedha hizi zinasaidia kupunguza ukimwi au zinakuwa ni mradi wa baadhi ya watu wanaoendesha shughuli hizi.

Mhe. Spika, jengine ni suala la udhibiti wa dawa za kulevya. Hapa nina masuala kadhaa. Sheria yetu ya kupambana na madawa ya kulevya inasema, mtu ambaye anakamatwa anatumia madawa ya kulevya anahukumiwa kwenda chuo cha mafunzo jumla ya miezi 6 na baadaye akitoka anatakiwa apelekwe katika kituo cha kurekebisha tabia. Zanzibar hatuna kituo hicho.

Hivi karibuni tumeona mkakati mkubwa wa kuwakamata vijana waliokuwa wanatumia madawa haya. Lakini hatujui wakitoka pale watasaidia kiasi gani kama hawatarejea suala hili. Kwa sababu wakishakumaliza hichi kifungu cha miezi sita hakuna pahala ambapo wanapelekwa wakaweza kupata huduma hii.

Huko nyuma ilikuwa suala hili likitajwa katika hotuba za Wizara ya Afya. Hatujui kama na mara hii itakuja katika Wizara ya Afya au ndio limeishia hapa. Tunaambiwa kuna kiwanja Tunguu kwa ajili ya shughuli hii, lakini hatuoni kama kumekasimiwa chochote katika matumizi ili kuweza kuziba suala hili.

Mhe. Spika, nije katika suala *Sober Houses*. Mimi na *doubt* kabisa kauli ya Mhe. Wazirin naomba akija anisaidie nikiangalia ukurasa wa 14 anasema.

> "Tume kwa kushirikiana na asasi za kiraia imeanzisha huduma za makaazi na marekebisho kwa watumiaji wa madawa ya kulevya yaani *Sober Houses"*

Mhe. Spika, mimi ni mtu wa karibu sana na *Sober Houses* kwa sababu binafsi nimekuwa nikiwasaidia katika shughuli zao. Ninavyojua malalamiko yao makubwa moja ni kwamba wanajiendesha wenyewe na hawapati msaada wowote, kutoka serikalini. Inapokuwa tume inakuja kujifichia kwa mgongo wa shughuli wanazofanya wengine kwa jitihada zao na kusema wanafanya kwa mashirikiano. Mimi napata wasi wasi juu ya taarifa zote unazoletewa katika Baraza lako tukufu.

Nilikuwa naomba maelezo ya kina katika suala hili tuelezwe. Na katika hilo hilo nilikuwa naomba kuhoji katika bajeti hii tuliwahi kumsikia Waziri akiahidi kwamba mara hii watafikiriwa kuwekewa fungu la kusaidiwa sober houses. Lakini katika mafungu yote niliyoyapitia katika kitabu hiki kikubwa sikuona fungu lolote la ruzuku au utaratibu wowote wa kusaidia *Sober Houses* zile. Nilikuwa nataka nipewe maelezo kwamba suala hili limefikia wapi.
Mhe. Spika, niseme kwamba yote ni muhimu, kukabiliana na Ukimwi ni muhimu na madawa ya kulevya ni muhimu. Ninapoiangalia bajeti ya ukimwi naona imetuna mno, lakini janga hili la taifa la pili la madawa ya kulevya unapokwenda kuangalia bajeti yake imelala mno. Namuomba Mhe. Waziri aje atupe maelezo kwamba je, hivi ndivyo anavyoweka vipa umbele katika shughuli zote muhimu zilizopo katika Afisi hii ya Makamo wa Kwanza Rais.

Mhe. Spika, nije katika suala la walemavu, tunahitaji kuona majengo. Kuna sheria hapa inataka kuona kwamba majengo yakijengwa yazingatie hali za walemavu. Hatuoni sheria hii ikitekelezwa, kuna tatizo gani? Naomba tupewe maelezo.

Pili vyombo vyetu vya habari vimeshindwa katika kutoa programu zake zimeshindwa kuweka wakalimani wa lugha zinazotumiwa na walemavu. Hii inawaathiri watu wetu wengi na tunao katika nchi yetu.

Mwisho kabisa katika suala la walemavu sijui wale walimu ambao wanashuhulikia elimu ya watu wenye ulavu wanasaidiwa vipi ili angalau kufidia jitihada ya ziada, katika ufundisha wa watu hao.

Mhe. Spika, nimepata wasi wasi nilipokuwa naangalia buku hili. Katika maelezo ya Mhe. Waziri inaonekana hapa tumekuja kupata nyongeza inayohusika na shughuli za Afisi ya Faragha ya Makamo wa Kwanza wa Rais, haijakuwemo katika kitabu hapo mwanzo. Nilipoangalia hiki kitabu chenye matumizi sikuona kabisa katika Afisi ya Makamo wa Kwanza kama kuna fungu linalohudumia Afisi ya Makamo wa Kwanza. Tofauti ilivyo kwenye Afisi ya Rais, Tofauti na ilivyo katika Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais nilikuwa naomba maelezo katika hilo.

Katika hilo hilo Afisi ya Faragha pia huwa inashughulikia ziara kama tulivyoambiwa. Katika hiki kijalida tulichopewa hapa zipo ziara ambazo Makamo wa Kwanza amefanya, tumeelezwa. Lakini maelezo yaliyokuwepo ni ya kijumla jumla mno, tofauti ilivyokuja katika Afisi ya Makamo wa Pili ambayo ilieleza ilifanya ziara wapi na imefanikisha mafanikio gani kwa Zanzibar.

Mimi naamini hata ziara alizozifanya Makamo wa Kwanza zinazo mafanikio lakini bahati mbaya hatukuelezwa. Hebu tuelezwe isije ikawa Makamo wetu wa Kwanza yeye tofauti na wenzake anakwenda huko labda akitembea tu kama mtalii. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba nikushukuru na rejea tena kusema kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la mji Mkongwe naunga mkono hoja hii nikitegemea nitapewa ufafanuzi wa Mhe. Waziri kwa yale ambayo nimeyaibua. Ahsante sana.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pili naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na uhai kufika katika Baraza lako tukufu. Pia naomba nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Zanzibar. Pia nimpongeze kwa kumteuwa Makamo wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad.

Vile vile nitakuwa mwinzi wa shukurani kama sikumpongeza Mhe. Waziri katika Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais pamoja na watendaji wake kwa uchambuzi mzuri wa kitabu chake hiki. Namuombe dua Mhe. Waziri pamoja

na watendaji wake yaliyomo ndani ya kitabu hiki wayatekeleze kwa vitendo na si kwa kubakia ndani ya kitabu hiki tu.

Mhe. Spika, naomba katika mchango wangu niende moja kwa moja katika madawa ya kulevya, jambo ambalo ni adui mkubwa katika nchi yetu na taifa kwa jumla.

Mhe. Spika, naamini Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kama vijana ni tegemeo kubwa la taifa kwa nchi yetu hii, lakini cha kusikitisha Mhe. Spika, vijana wetu wanapotea kwa nguvu kubwa, wanaathirika sana na madawa haya ya kulevya. Sasa namuomba Mhe. Waziri katika hili la kuwalinda vijana wetu kwa kupotea kwa madawa ya kulevya kuna mambo muhimu sana ambayo yanatakiwa yatizamwe na yaangaliwe kwa makini sana.

Jambo la kwanza muhimi Mhe. Spika, iangaliwe namna zinavyoingizwa dawa za kulevya hapa nchini. Kwa sababu tunapowakamata vijana wetu wadogo wadogo kwa sababu ya kula unga na mambo mengine, tuangalie wao vijana wadogo wadogo waliomo mitaani wanayapata wapi madawa hayo? Cha msingi Mhe Spika, ninachokiomba kwa Mhe. Waziri, waweke ulinzi mkubwa na madhubuti katika maeneo yetu yanayoingiziwa madawa hayo vikiwemo viwanja vya ndege, bandarini na sehemu nyengine za vichochoroni ambazo zinaingizwa dawa hizo.

Mhe. Spika, naomba nimwambie Mhe. Waziri katika hili kama hapakuwekwa ulinzi madhubuti katika kulinda madawa ya kulevya hawa wafanyabiashara haramu wanavyoziingiza basi serikali itaendelea kupoteza pesa nyingi za nchi na za wahisani, lakini tatizo hili halitoondoka.

Mhe. Spika, naomba kumuomba Mhe. Waziri atoe adhabu maalum kwa kupitia serikali au serikali kupitia waziri iweke adhabu maalum ya wale watakaokamatwa wakiingiza madawa ya kulevya hapa nchini. Kwani wafanyabiashara hao ni maadui sana wa nchi yetu na hawana imani na vijana wetu. Vijana wetu wadogo wote wameshapoteza akili, hakuna mwenye akili, wezi, tunapata matatizo, mlango ukiuwacha wazi dakika moja tu wameshaingia na wameshachukua chochote kilichokuwepo karibu.

Mhe. Spika, tatizo hili ni sugu na litaendelea kuwa sigu kama bado serikali haijawa makini katika kudhibiti wafanyabiashara haramu hawa wanaoleta madawa ya kulevya hapa nchini.

Mhe. Spika, nataka niingie katika sehemu ya walemavu. Walemavu ni binaadamu sawa na binaadamu wengine na wana haki sawa sawa na binaadamu wengine. Kuna walemavu wa aina nyingi mitaani hasa vijijini, kuna wengine ni

viziwi, mabubu, vipofu, wengine wanaweza kutembea na wengine hata kunyanyuka walipo hawawezi na wapo wengi wa aina hii.

Namuomba Mhe. Waziri walemavu hawa waliokuwa wa kulazwa na kunyanyuliwa kupitia ndani ya majimbo namuomba sana ashirikiane na viongozi n wa majimbo wakiwemo Wawakilishi, Wabunge, Madiwani, Masheha, kwa kuwafatilia hawa. Wazazi wengine waliokuwa na watoto wa aina hiyo wanaona tabu hata kuwatoa au kutoa zile taarifa zao maana yake wao wanawaona wale ndio basi hawana haki yoyote ya kuishi. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri katika hili tushirikiane ili kuwapatia ufumbuzi wenzetu hawa walemavu na matatizo waliyonayo.

Mhe. Spika, nataka nisogee kidogo katika mambo ya mazingira, ingawaje wenzangu wengi wameshazungumza mambo ya mazingira, ukataji miti, upoteaji wa ardhi ni matatizo yanayotuandama Zanzibar nzima. Ni kweli katika kisiwa chetu cha Pemba ndani ya Wilaya yangu ya Wete, hasa ndani ya jimbo langu la Ole, ukataji wa matofali umekuwa mkubwa mno.

Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais walikuja pamoja na watendaji wake kutoa taarifa za ufukiaji wa mashimo baada ya kwisha kuchimbwa matofali. Lakini baadhi ya watu wakayatafsiri vibaya na sisi wenyewe wazazi na vijana tukasema kwa vile vijana hawana kazi ya kufanya basi kazi ya kufanya ni hiyo. Baada ya muda mrefu au baada ya muda mfupi mashimo yale yatakuwa bahari na tutashindwa hata na sehemu ya kuishi, kwa sababu ardhi zetu zote ni za kumong'onyoka, ni mchanga, na maji mengi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri tulisimamie sana suala hili, tuwatafutie vijana wetu mpango mwengine wa kufanya ikiwezekana ili mradi tuepukane na mazingira yetu.

Mhe. Spika, nchi za wenzetu wakati wote huwa wanaimarishwa kupanda miti. Sisi ndani ya nchi yetu tunakata, kupanda inakuwa ni ndogo, hatuna nguvu kubwa ya kupanda miti. Namuomba sana Mhe. Waziri katika hili ahamasishe tupandeni miti kwa wingi *"Kata mti panda mti"* nchi yetu ni ndogo, ardhi yetu ni ndogo haitutoshi. Tukiendelea kukata miti kila wakati bila ya mpangilio tutajishtukia tupo katika mahali pagumu na uchumi wetu utakuwa utakuwa hauwendi mbele bali tunarudi nyuma.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa

kumteuwa Maalim Seif Sharif Hamadi kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Lakini pia nampongeza Waziri wa Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Fatma Fereji kwa tulivyomzoe. Kwa kusimamia vyema majukumu yake ya Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Labda kama alivyosema Mhe. Rashid Seif niwaombee duwa watu hawa na viongozi wote Mwenyezi Mungu awape ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yao muhimu.

Pia nakupongeza wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu katika kitabu hichi cha bajeti cha Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Mengi yamezungumzwa na waliozungumza lakini na mimi nitakuwa ni mchache wa fadhila kama nitakuwa sikuweza kuchangia chochote katika bajeti hii.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 5 unaozungumzia Utekelezaji wa Majukumu kwa mwaka 2011/2012 hapa naruka mpaja ukurasa wa 6 katika yale majukumu ya Ofisi hii. Kuna kipengele cha 5 Idara ya Watu Wenye Ulemavu. Suala hili la watu wenye ulemavu ni suala la kulipa nafasi kubwa, hawa ni wanadamu kama wanadamu wengine.

Nimuulize Mhe. Waziri suala hili kwa taarifa ambayo tumeipokea sasa hivi kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kuishughulikia Viongozi Wakuu anasema kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi katika Idara ya Watu Wenye Ulemavu Pemba. Namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie kwa kina kwa sababu walemavu wanataka wazingatiwe kujulikana, Shughuli na maendeleo yao. Kama kunakuwa na upungufu mkubwa kwa wafanyakazi katika idara hii pale Pemba, basi itakuwa watu hawa tumewakosesha ufanisi wa kufuatiliwa masuala yao.

Mhe. Spika, kwa hili vile vile nilizungumze asubuhi mapema nimepata taarifa kupitia mtandao wa simu kwamba pale Idara hii ya watu wenye ulemavu kuna mfanyakazi mmoja tu, anashindwa hata kupata likizo katika kipindi kirefu kilichopita kwa sababu ya ufatiliaji wa shughuli zake za pele kwamba akipata likizo yeye kutakuwa hakuna mtu ambaye anaweza akalisimamia suala hili.

Mhe. Spika, watu wenye ulemavu wanakumbana na changamoto mbali mbali, wananyanyaswa na baadhi ya watu, wanadhalilishwa na baadhi ya watu. Kitengo hiki kinapaswa kizingatiwe vyema na kuwapa haki zao vizuri, kwani hawa ni binaadamu kama binaadamu wengine. Hawakufanya kosa hawa kuwa walemavu bali ni maumbile tu ya Mwenyezi Mungu mwenyewe alivyopanga kuwa wawe hivyo.

Nataka nitoe kisa kidogo tu kama ni changamoto kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wasikilizaji wetu juu ya suala zima la walemavu, changamoto hii kama ifuatavyo.

Mara moja alikwenda mtu mmoja kwa Mtume Muhammad (SAW) akiwa huyu ni mwenye maradhi ya kifafa, akamuomba Mtume amuombee duwa ili aepukane na maradhi yale, kifafa ni ulemavu. Mtume Muhammad (SAW) akamwambia hivyo wewe hutaki kuwa mtu wa peponi? Akamwambia nataka. Akamwambia basi hivi alivyokujaalia Mungu ndivyo hivi hivi. Basi yule kijana akamwambia basi nakuomba uniombee duwa ili nikianguka nisitirike. Akamwambia hilo umepata. Akaombewa dua kwamba akianguka kwamba asitirike.

Kwa hivyo na sisi tunapaswa kuwasitiri walemavu, kuwatunza na kuwapenda walemavu kwani hawana kosa walilolifanya bali ni maumbile tu ya Mwenyezi Mungu aliyowaumba.

Idara ya Watu wenye Ulamavu Mhe. Waziri amesema katika ukurasa wa 14 Mfumo wa uwekaji kumbukumbu kwa wetu wenye ulemavu tayari umeanza. Idara imekusanya taarifa za watu wenye ulemavu katika Shehia 65 za Mkoa wa Kaskazini Unguja. Ukiteremka hapo chini huoni hata Mkoa mmoja wa pale kisiwani Pemba kwamba umeingizwa katika utaratibu huu. Namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie vyema. Kama tulivyosema kwamba visiwa viwili hivi vinategemeana kwa hivyo ile haki inayotoka hapa na kule kwa sababu kuna watu wanaoathiriwa na tatizo hili hili, basi kuwe na watu ambao watalifuatilia au watalifanyia kazi suala hili.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 16 katika Tume ya Ukimwi. Jamani kama walivyozungumza waliopita. Ukimwi ni janga kubwa sana hapa Zanzibar. Tukifanya mas-hara basi hili litaungamiza umati wa watu wa Zanzibar. Nataka nitoe taarifa ndogo kuna kijitabu kinasema tathmini ya hali na athari za Ukimwi katika sekta ya utalii Zanzibar.

Nimuombe Mhe. Waziri wa Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais awe na uhusiano mkubwa sana pamoja na Wizara ya Habari, Utalii na Michezo. Katika utafiti huu uliofanywa na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ile zamani mwaka 2007, nataka ninukuu maneno haya yafuatayo:

> “Pia kuna sehemu kubwa ya makundi ya watu katika jamii zilizokaribu na hoteli za kitalii ambao ni wahamiaji wa muda, hawa wanahamia katika maeneo ya hoteli za kitalii, wakati wa msimu wa utalii kwa kutafuta wateja na biashara za msimu kama ngono, dawa za kulevya na kuuza sanaa za michoro”

Mhe. Spika, kwa kweli Waziri Katika Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa hili kama hajashirikiana na Waziri wa Utalii kwa kweli itakuwa mikakati yake kuhusiana na suala zima la kudhibiti ukimwi halipatikani. Inaonekana watalii wanaingia kwa wingi sana nao ni chanzo cha ongezeko la Ukimwi kwa mujibu wa kitabu hiki. Hiki kitabu kimefanyiwa utafiti mwaka 2007 na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji. Ni juu yetu kulijua hilo pamoja na kufuatilia na kuweka miundombinu madhubuti juu ya kudhibiti hawa watu ambao wanaingia katika mahoteli yetu kiholela holela.

Mhe. Spika, niendelee kidogo na Idara ya Mazingira. Kama walivyosema waliotangulia. Nchi yetu ni visiwa na visiwa vyetu ni vidogo, kama hatukuwa makini baada ya miaka kadhaa ijayo tunaweza kuvamiwa na bahari na mwisho wake visiwa hivi kudidimia.

Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Waziri kuna maeneo kule Pemba kama Tumbe na Wingwi katika maeneo ya fukwe au maeneo ya bandari, kumekatwa baadhi ya miti au mikoko mpaka maji yamevamia katika maeneo ya bahari ambamo watu wanalima. Ikiwa watu wanamolima mpunga au mihogo yamevamiwa na maji ya bahari kwa kukatwa miti, mwisho wake maji yale yanakwenda wapi? Yanakwenda katika miji na mwisho wake ni kuvifanya visiwa vyetu kuwa ni visiwa vya hatari kwa makaazi na maisha ya watu. Ningemuomba Mhe. Waziri anayehusika na Wizara hii aeke mipango madhubuti inayotekelezeka ili ukataji wa miti ovyo katika baadhi ya maeneo.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Mazingira katika suala zima la kuteketeza kunguru. Kwa kweli kunguru ni tatizo kubwa hapa kwetu sisi visiwani Zanzibar hasa kisiwa cha Unguja.

Nafikiri pamoja na kuuliwa kunguru wengi katika kipindi kilichopita lakini labda ningemshauri Mhe. Waziri katika hili. Mbali ya kuuwa wale kunguru ambao tayari wanaruka, aweke mkakati maalum wa kuyasaka au kuyatafuta mayai ya kunguru. Si vibaya hata kutoa tamko rasmi kama wizara yake itamuwezesha kutoa tamko rasmi kwamba atakaeleta yai la kunguru basi kutakuwa na zawadi fulani. Hili linaweza likasaidia kwa kuwapata kunguru wachanga wachanga ambao labda wangezaliwa kesho au keshokutwa. Kwa haya machache naunga mkono hoja mia fil mia kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Chambani. Ahsante tunashukuru.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, dakika tano hizi Mhe. Spika, hazifiki pahala. Kwanza nikushukuru kwa kunipa muda huu ambao kwa kweli haunitoshi kama nilivyosema ni mdogo, labda jioni nitaweza kupata nafasi ya kuendelea.

Pili nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii ya leo kukutana hapa kwa ajili ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Wizara hii kwa maelezo yake ambayo ametueleza humu katika hotuba yake.

Mhe. Spika, wizara hii kama wenzangu waliotangulia imepewa majukumu mazito sana, hasa haya majukumu matatu haya ni mazito ambayo ni

- Jukumu la kusimamia masuala ya mazingira katika nchi yetu.
- Suala la kusimamia uratibu na udhibiti wa madawa ya kulevya.
- Lakini pia suala la Ukimwi.

Mhe. Spika, masuala haya yote matatu ni masuala mazito. Naweza kuthubutu kusema kwamba majukumu haya yaliyopewa ofisi hii ni majanga katika taifa. Ndio maana nadhani Mhe. Rais ameamua kuyaweka katika Afisi hii nzito Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Hii ni Afisi nzito ambayo imepewa jukumu ya kusimamia mambo haya mazito. Matumaini yangu kwamba yatasimamiwa vizuri ili kuona matatizo yanayotokana na masuala haya yanamalizika.

Mhe. Spika, katika maeneo haya nitaanza kuzungumzia suala zima la mazingira. Kama tunavyofahamu tafsiri ya mazingira ni maeneo ya watu humu tunamoishi. Ni lazima tukiri kwamba nchi yetu hii ya Zanzibar imeathirika sana na uharibifu wa mazingira. Hili jambo ni la ukweli na linahitaji kufanyiwa utafiti wa kutosha.

Mhe. Spika, ukataji wa ovyo wa misitu katika maeneo yetu umekithiri. Suala la uchimbaji wa michanga na masuala ya uchimbaji wa mawe, ukataji wa mawe hasa katika kisiwa cha Pemba nalo limekithiri. Suala la uchafu wa mazingira katika maeneo yetu hasa ya mijini, maeneo ya Mji Mkongwe na maeneo ya Miji yetu pia nayo yamekithiri.

Mhe. Spika, suala la uchafuzi wa mazingira unahitaji kupewa kipaumbele. Ili suala hili liweze kufanikiwa linahitaji mashirikiana ya pamoja kati ya wizara inayohusika kupitia idara yake ya mazingira, lakini pia kupitia katika maeneo mengine, kwa mfano Masheha, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa.

Kama nilivyotangulia kusema mwanzo kwamba masuala ya mazingira ni katika yale maeneo ambayo sisi wenyewe tunaishi. Bila ya mashirikiano ya pamoja kati ya taasisi hizi, kati ya maeneo haya basi suala la mazingira kila siku tutakuwa tunalizungumzia.

Mhe. Spika, suala la mazingira lina uhusiano mkubwa sana na suala la kuimarisha sekta ya utalii. Utalii ni mazingira na bila ya kuwa na mazingira yaliyo bora, mazingira safi, ambayo yatakuwa ni kivutio kwa watalii wetu basi suala la kuimarisha sekta ya utalii itakuwa kila siku tunalizungumzia.

Mhe. Spika, juzi tulipata mualiko kidogo baadhi ya wajumbe wako, lakini mualiko usio rasmi ambao tulizungumza na taasisi moja ambayo inasimamia masuala ya utalii. Moja kati ya maelezo ambayo wametueleza kwamba yanaathiri sana utalii wetu ni masuala mazima ya mazingira yetu.

Serikali ni lazima itoe kipaumbele katika eneo hili ili kuona sekta ya utalii inaimarika. Unapoimarika utalii maana yake na uchumi wetu utaimarika. Kwa hivyo suala la kuhifadhi mazingira katika maeneo mbali mbali ni muhimu. Zaidi ukitilia maanani kwamba sasa hivi kuna mabadiliko haya ya hali ya hewa, semina mbali mbali, makongamano mbali mbali yanazungumzwa juu ya mabadiliko ya hali ya hewa. Wataalamu wa mabadiliko ya hali ya hewa duniani wanaeleza kwamba moja ya kinga kubwa ambayo inaweza ikatusaidia katika nchi yetu ni kupanda miti na kuhifadhi mazingira.

Pamoja kwamba suala la uchafuzi wa mazingira linatokana na masuala ya viwanda. Wenzetu watu wakubwa wenye nchi zenye viwanda wao ndio wanaosababisha uchafuzi mkubwa sana wa mazingira na kusababisha mabadiliko ya hali ya hewa. Sisi hatuna viwanda lakini athari inapotokea inatukumba sote. Ili tuweze kuepukana na jambo hili ni lazima tupande miti kwa wingi, tuache kukata miti ovyo hapo tunaweza tukasaidia katika suala zima la kuepukana na hali hii ya uchafuzi wa mazingira.

Mhe. Spika: Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe, nilitangulia kusema kwamba shughuli yetu hii tunategemea kumaliza kesho, tena wakati wa kipindi cha asubuhi. Pengine baada ya maswali patakuwa na wachangiaji kidogo halafu tena baadaye tumuombe Mhe. Waziri.

Michango inavyoonekana tayari kumeshakuwa na marudio rudio. Haina maana kwamba tusiendelee kuchangia lakini tujaribu kutorudia sana, labda tunakwenda kwenye maeneo ambayo Waziri itamsaidia katika kazi zake kwenye mwaka ujao huu wa fedha kuweza kufatilia katika yale maeneo ambayo tumemwambia kwamba huko kuna matatizo ya mazingira, madawa ya kulevya na mambo mengineyo.

Kimsingi tayari inaonekana kuna marejeo rejeo ambayo kanuni huwa hazitaki hivyo. Lakini najua mtajipanga vizuri ili muweze kumsaidia sana Mhe. Waziri

katika utekelezaji wa mambo yaliyokuwemo chini ya Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Raisi.

Jioni ataendelea Mheshimiwa wangu, Mwenyekiti wa Baraza. Naamini mtakwenda vizuri kiasi cha kwamba kila tunapotumia muda mfupi basi Wajumbe wengi zaidi watapata kutoa maoni yao, ili kusaidia wizara hii iweze kufanya shughuli zake vizuri.

Waheshimia wajumbe nakushukuruni baada ya machache hayo basi naahirisha kikao hichi hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niendelee kutoa mchango wangu ambao niliuanza mapema na Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa katika maeneo yanayohusiana suala zima la uhifadhi wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwamba suala la mazingira ni muhimu na kwa sababu lina eneo pana na ni janga katika nchi yetu. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba maeneo haya yanayohusika na masuala mazima ya mazingira ni lazima wizara yake ifanye kila linalowezekana kuona kwamba wanadhibiti mazingira. Kama nilivyotangulia kusema kwamba mazingira hayahusu Idara ya Mazingira tu au wizara inayohusika, bali inahitaji mashirikiano ya pamoja ili kuona tunapambana na hili. Na kwa sababu mazingira ni sehemu ya uchumi wa nchi, ni sehemu ambayo inaathiri baadhi sekta. Kwa hivyo, ni vyema suala la mazingira tukalipa kipaumbele ikiwa ni pamoja kutoa na serikali itoe kila linalowezekana ili kuona wanawezesha kufanikisha jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia mwisho wa hotuba ya Mhe. Waziri hapa katika malengo ya mwaka 2010-2011 eneo moja ambalo nimelazimika nilizungumze kidogo ni eneo ambalo wanasema kwamba kuendelea kusimamia upigaji marufuku uingizwaji wa matumizi ya mifuko ya plastiki. Mhe. Mwenyekiti, hili ni eneo muhimu ambalo kwa kweli inaonekana utekelezaji wake si mzuri na kwa sababu mifuko ya plastiki inaonekana mitaani.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika ikiwemo Baraza la Manispaa basi lazima wakaze buti

vyenginevyo mifuko ya plastiki itaendelea kurudi na itaanza kuzagaa tena mitaani. Kwa sababu kama tunavyojua wananchi wetu na wafanyabiashara huwa wanaangalia namna ya usimamiaji, wakiona usimamiaji mzuri basi na wao wanarudi nyuma, wakiona usimamizi unakuwa legelege basi na wao wanaitumia ile nafasi kwa kufanya mambo yao.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo nimeingia mashaka kwa sababu kwenye hotuba ya Mhe. Waziri kazungumzia kidogo tu kwamba kiasi cha tani 68 za mifuko ya plastiki zilikamatwa katika maeneo ya Bawe na Ras Shangani. Kwa hivyo, kilichonishtua kwamba Mhe. Waziri amezungumzia tani 68 zilizokamatwa Bawe na Shangani peke yake, lakini hakuweza kuzungumzia *in general* kwamba katika kipindi hiki ni tani za mifuko ya plastiki zimewezwa kukamatwa katika maeneo mbali mbali.

Kwa hivyo, hili kidogo limenipa mashaka kwamba utekelezaji wa shughuli hizi katika maeneo mengine yamekuwa yakusuasua. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho angalau atueleze kwamba mbali ya hizi tani 68 zilizokamatwa katika maeneo ya Bawe na Shangani ni kiasi gani cha mifuko ya plastiki ambayo imekamatwa katika maeneo mengine ili tuweze kupima utekelezaji wa jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika eneo jengine muhimu linazungumzia suala la Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Madawa ya Kulevya. Mhe. Mwenyekiti, hapa Mhe. Waziri ametueleza kwamba kwa kushirikiana na asasi za kiraia wameweza kujenga nyumba 7 Unguja na Pemba ambazo hadi kufikia mwezi Mei jumla ya vijana 698 wakiwemo wanaume 680 na wanawake 18 wameweza kuwekwa katika maeneo haya ya *Sober House* ili kupata elimu juu ya masuala haya kutokutumia madawa ya kulevya.

Kwa kweli sisi tunawapongeza sana katika juhudi zao hizi za kupambana na madawa ya kulevya, na kwa kweli suala la madawa ya kulevya ni janga la taifa ambapo vijana wetu wengi nguvu kazi zimeweza kuathirika kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na juhudi za serikali za kupambana na madawa ya kulevya, lakini bado inaonekana jambo hili linaendelea kwa kasi haidhuru limeanza kupungua. Kwa hivyo, tunaiomba serikali iendelee kupambana na jambo hili ili kuona vijana wetu hawaendelei kuathirika na madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika eneo hilo ameelezea kwamba katika kipindi cha mwaka huu 2011-2012 ameelezea katika malengo yake ni kwamba kuendelea na juhudi za taasisi zisizo za kiserikali zinazotoa huduma za makaazi na marekebisho kwa vijana wanaoacha matumizi ya madawa ya kulevya.

Amerejea kusema kwamba mwaka jana kulikuwa na lengo hili lakini na mwaka huu wanaendelea tena.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nililotaka kulizungumzia ni juu ya umuhimu wa serikali katika kupambana na madawa ya kulevya hasa katika maeneo haya. Kwa sababu nilikuwa najiuliza hawa vijana ambao wanapata makaazi na marekebisho je, baada ya kumaliza muda wao tunawafanya nini?

Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia bajeti hapa ya Mhe. Waziri kwamba hakuna fedha yoyote ambayo imetengwa kwa ajili ya jambo hili. Mhe. Mwenyekiti, wasi wasi wangu mimi kwamba pengine vijana hawa tunaweza kuwa tunawatoa katika majanga haya lakini baada ya muda mfupi watakapokuwa hawana shughuli za kufanya kuna hatari ya vijana hawa kurejea katika shughuli ile ile ya mwanzo ambayo walikuwa wanaifanya. Kwa hivyo, hapa ni sawa sawa na kutwanga maji kwenye kinu kwamba tunafanya juhudi tunawatoa, lakini baadaye hatuwajengei mazingira ambayo yanaweza yakawasaidia kupata shughuli za kufanya baadaye.

Kwa hivyo, hapa serikali inahitaji kutenga fedha, nakumbuka siku za nyuma kulikuwa na shamba kule Tunguu ambalo walikuwa wanapata nafasi ya kujishughulisha na shughuli za kilimo, lakini inaonekana hakuna fedha ambazo zimewekwa kwa ajili hii. Kwa hivyo, mimi naiomba serikali kwa makusudi itenge fedha kwa ajili ya kupambana na masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala la kupambana na ukimwi. Mhe. Mwenyekiti, suala hili nalo ni janga la taifa ambalo kwa kiasi fulani linahitaji msukumo wa hali ya juu. Tunawashukuru wafadhili wetu wameweza kutuchangia fedha nyingi hapa kwa mujibu wa taarifa za Mhe. Waziri karibu shilingi bilioni 1.3 zimetolewa mchango wa Washirika wa Maendeleo katika mapambano haya ya maradhi ya ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, fedha hizi ambazo zinatolewa na wahisani kwa ajili ya kupambana na ukimwi ni lazima zieleweke. Nadhani Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliwahi kusema hivyo kwamba ni lazima zieleweke zinatumika vipi kwa sababu kuna dhana kwamba fedha hizi hazitumiki vizuri. Kwa hivyo, kwa kuwa fedha hizi za michango ya wahisani zinaletwa hapa, zinaidhinishwa hapa, taarifa zinatolewa hapa kwa hivyo ni vyema fedha hizi zikaeleweka matumizi yake.

\Mhe. Mwenyekiti, vyenginevyo fedha hizi nyingi zinaweza zikatumika visivyo na ile juhudi ya wafadhili yakutupa fedha kwa ajili ya kupambana na maradhi ya ukimwi basi ikawa haina mafanikio, pamoja na kwamba sasa hivi hali yetu sio mbaya sana kwa mujibu wa taarifa ambazo nazipata, hali yetu ni nzuri,

maambukizo mapya ya virusi vya ukimwi yamepungua. Lakini lazima fedha zinazotolewa na wahisani ziweze kutumika vizuri ili malengo yale yaweze kufanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina maelezo mengi zaidi nilikuwa namalizia michango yangu hiyo, lakini pia nitake maelezo kidogo kwa Mhe. Waziri juu ya lile ambalo nimelizungumzia la mifuko ya plastiki kwa sababu eneo hili nalo ni eneo muhimu ambalo linaweza likatusaidia katika mapambano ya uchafunzi wa mazingira. Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja na nimtakie kila la kheri Mhe. Waziri pamoja na wasaidizi wake ili wandeleze mapambano haya ili tuweze kufanikiwa na nchi yetu iweze kupata mafanikio. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri kabisa na yenye muelekeo wa ujenzi wa taifa letu. Niwashukuru watendaji wa ofisi hii kwa kazi nzuri walioifanya na leo hii wamemuwezesha Mhe. Waziri kuileta hotuba yake hii hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza kwenye suala la mazingira ingawa wachangiaji waliopita wamelichangia sana na mimi nataka niguse kidogo, mimi nitaanza kwenye hii mifuko ya plastiki. Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa watu wa mazingira kwamba hii inachangia kuharibu mazingira na imepangiwa sheria kabisa kuwa ni marufuku kuingiza hii mifuko, lakini bado mifuko hii inaingia hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, mifuko inaingia na inatumika kwa hivyo inaendelea kutuchafulia mazingira yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo nina wasi wasi na suala hili kwa sababu uingiaji wake haiingii mmoja mmoja inaingia kwa tani hasa. Mhe. Mwenyekiti, ushahidi upo kwa sababu imeshawahi kukamatwa hapa kama utakumbuka vizuri kwenye televisheni mara moja ilioneshwa kama bandal 434 za mifuko ya plastiki imekamatwa na vijana wa KMKM. Vile vile tarehe 3 tukaoneshwa tena imekamatwa mifuko mengine bandal 280 na hao KMKM. Mhe. Mwenyekiti, chakushangaza mifuko ile kesi zake hatuzioni zinavyoendele, mimi nahisi hili ni tatizo na mifuko ile ukiuliza hii kama iko wapi basi utaambiwa haionekani, pengine kesi haijesha na mifuko haipo wamesharejeshewa wenyewe na imeshaingia nchini mwetu.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri hili mimi naomba ni tatizo kwa kuwa inakamatwa halafu inapelekwa kwenye vyombo vya sheria ikishafika huku basi inaachiliwa

tena wanarejeshewa wenyewe. Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja haja utakuja kutuambia kama mifuko ipo na kesi yake imemalizika vipi, tukipata hilo tutaona zile jitihada za serikali za kudhibiti hii mifuko isiingie hapa nchini kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyohisi kwamba hapa pana mchezo fulani unachezwa. Kwa hivyo, hili naiomba sana serikali itusaidie juu ya hili kwa sababu kuharibika kwa mazingira ni kuangamia kwa sisi viumbe huku. Kwa hivyo, mimi naomba serikali hapa ijitahidi katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni uchimbaji wa mchanga ovyo, ile Idara ya Misitu na Maliasili nafikiri wanatoa kibali cha uchimbaji wa maeneo. Lakini bado kuna maeneo yanaendelea kuchimbwa hata kama ule mchanga wenyewe haupo, basi watu wanaendelea kuchimba dongo linakuja kuuzwa ukipita pale Mwanakwerekwe utaona kwenye yale magari kama utaukagua ule mwengine wala sio mchanga safi. Mhe. Mwenyekiti, watu hawa nao pia ni wachafuzi wa mazingira kwa sababu hutuchimbia chimbia tu humu ndio matatizo na baadaye yanatokea mafuriko.

Mhe. Mwenyekiti, hasa maeneo ya kwetu kumekuwa kuna uchimbaji mkubwa wa mchanga maeneo ya Kaskazini “B” na “A” kidogo maeneo ya Mkokotoni kama utakwenda kuangalia yale mazingira ya uchimbaji wenyewe Mhe. Waziri utaona huruma. Kwa hivyo, mimi nahisi wizara ipige mkazo kidogo kwenye eneo hili kuwe kuna utaratibu mzuri wa kutoa vile vibali vya uchimbaji, kutoa vibali holela nako kunatuangamizia maana mashimo yakishakuwa mengi inakuwa ni hatari.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee kidogo kwenye eneo la fukwe kwani fukwe zetu hizi zinajengwa sana, mimi ninavyofahamu uliwahi kutwambia hapa kulikuwa kuna suala la msingi lilikuja kuhusu habari ya ujenzi wa fukwe.

Mhe. Waziri ukasema sio uchafuzi tu wa mazingira ni uharibifu wa mazingira, lakini watu wanajenga kwenye fukwe na vibali vinatolewa na mtoaji vibali ni serikali. Mhe. Mwenyekiti, kama huu ni uchafuzi wa mazingira na watu wanapewa ruhusa kabisa ya kujenga kwenye zile fukwe. Mhe. Mwenyekiti, tukitembea hapa Mjini tukizikagua hizo hoteli zilizopo hukosi hoteli tatu au nne zimejenga kwenye fukwe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemuomba Mhe. Waziri katika hili hebu akae na vyombo husika maana yake najua inawezekana sio yeye anayetoa, lakini kuna taratibu za kiserikali ndio zinazotoa, hebu kaeni pamoja msaidiane katika hili. Mhe. Mwenyekiti, waziri akizuia kuna mwenzake anatoa ina maana hakuna

ushirikiano hapo, hebu kaeni pamoja tutizame itakuwa vipi, kama mnaamua huu ni uchafuzi wa mazingira basi asiwe huyu anapewa na huyu ananyimwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wanapewa vibali kwa makusudi wajenge na wanajenga kwenye fukwe mpaka baharini na haambiwi kitu, na kuna mtu mwengine akigusa tu huko basi kelele zake hazina idadi. Kwa hivyo, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri katika hili ukae na taasisi husika kuweza kulidhibiti kwa sababu tukiacha ujenzi huu ni hatari.

Mhe. Mwenyekiti, hao wenzetu wawekezaji ndio wanakuja lakini wao huwa wanakuja na kuondoka na sisi ndio kwetu hapa itakapokuja kuja kuangamia tunaangamia sisi wao wanaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niingie kwenye madawa ya kulevya, madawa haya ni tatizo sugu sana kwa nchi yetu, lakini mimi naona bado serikali haijafanya bidii zaidi katika hili. Kwani serikali iko zaidi kwenye hawa wanaovuta huo unga, haikuweka mkazo katika wale wanaoleta unga. Mhe. Mwenyekiti, hawa wavutaji kama haujaletwa huu unga basi hawawezi kuuvuta na waletaji hawaleti kwa njia ya uchawi wanapitia katika hivi hivi vyombo vyetu baharini au uwanja wa ndege.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili mimi naona serikali bado haijajipinda kabisa kwa waletaji inajipinda kwa wavutaji. Kwa hivyo, kama mvutaji unamchukua leo unamuweka ndani, kesho ukamtoa unga upo basi atakula tena utamkuta pale pale anasinzia barazani. Kwa hivyo, mimi naomba tuwashughulikie hawa waletaji na tunawajua sana tu, maana waletaji sio malaika ndio sisi tumo humu humu wengine tunaokwenda kuupokea. Mhe. Mwenyekiti, wengine ni wazito kabisa wanene ndio wanaokwenda kupokea hayo mabegi ya unga hapo *airport* yanajuulikana. Mhe. Waziri katika hili hebu tujipinde kama serikali imeamua kweli haitaki unga uingie humu basi hautokuja.

Kwa hivyo, mimi ningeomba serikali ijipinde kwa wale waletaji hao wenzangu mimi wanaosinzia barazani ikiwa haupo hawatosinzia maana hawaupati. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa hebu atupe mkakati hasa uloandaliwa na serikali wa namna gani wataweza kulikomesha suala hili, kama sio hivyo itakuwa ndio tunaimba tu kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye suala la ukimwi kwa kweli suala hili ni kadhia kubwa sana katika taifa letu, maana linatuondoshea wapendwa wetu. Kwa hivyo, mimi ningeishauri serikali katika hili hebu iongeze bidii kwanza ya kuelimisha jamii. Mhe. Mwenyekiti, inaonekana bado suala la kuelimisha liko chini kidogo, hivyo serikali itilie mkazi zaidi katika kuelimisha jamii ili jamii iweze kufahamu hii athari ya ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, ikiweza kufahamu basi nahisi tunaweza tukapunguza hili tatizo, kama vile mtoto unavyomfundisha moto huo utaungua asiguse, basi anakuwa hagusi kwa sababu anajua akigusa ataungua. Kwa hivyo, na hili hebu tuliendeleze najua serikali inatoa elimu maana katika hotuba yake nimeona humu, lakini naomba ile bidii iongezwe zaidi kwa kushirikishwa na hivi vyombo vyengine vya kijamii hivi, tuwashirikishe Mashehe kwa nguvu zaidi, tuwashirikishe Mapadri kwa nguvu zaidi ili na wao wawe wanawaelimisha waumini wao, kwa sababu tukiwashirikisha hawa wakawa wanawaelimisha wale waumini kwa kuwa pale wameenda kuchukua imani nahisi na hili watatoka nalo basi litaweza kusaidia angalau akirudi huku aielimishe ile jamii yake katika familia. Mhe. Mwenyekiti, kama sio hivyo hili suala tutakuwa tunaendelea kuimba lakini utatuzi wake hautokuwepo.

Mhe. Mwenyekiti kwa kujali muda niguse kidogo kwenye suala la walemavu, suala la walemavu mimi ningeliomba serikali izishurutishe hizi taasisi zake au idara na zenye majengo kuwawekea *essence wa*lemavu kuweza kuingia kwenye majengo yale, majengo mengi sana ya serikali hayana *essence* kwa mlemavu kuweza kuingia mle. Kwa hivyo ningeiomba serikali ijikite zaidi kuweka *essence* kwa ajili ya walemavu kuingia katika taasisi zake za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa sababu umenipa dakika mbili nizimalizie mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Mkwajuni naiunga mkono hotuba hii nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nami kunipa nafasi hii katika wakati wa jioni kutoa mchango wangu kidogo katika hotuba ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mimi nitaanza katika sehemu ambayo ni janga letu la taifa ambalo ni jinamizi ambalo tunalo kwa muda mrefu naweza kuthubutu kusema ni mitihani yake Mwenyezi Mungu ametuteremshia waja wake, Mhe. Mwenyekiti mimi nadhani nianzie pale alipomalizia mchangiaji katika sehemu ya ukimwi, ningeliomba kumuuliza tu Mhe. Waziri anasema tume ya ukimwi katika kuandaa kuendeleza na shughuli za uandaaji na mkakati wa pili, Namuomba Mhe. Waziri angalitueleza mkakati wa mwanzo kumepatikana mafanikio gani ili tujue mafanikio yaliyopatikana katika huo mkakati wa mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti hapo hapo mimi nadhani niseme pale katika ukurasa wa kumi na nane anasema kwamba Tume ya Ukimwi imejikita kutoa elimu zaidi kwa njia ya Redio, Televisheni, mimi nadhani baraza lililopita siku moja aliwahi kusema hapa Ukimwi kama ingelikuwa unaondoka kwa makongamano ungelikuwa umeshaondoka na ungelikuwa haupo na wala hatuzungumzii tena

suala la Ukimwi, kama kuondoka kwa makongamano, vipindi vya redio nadhani hakuna hata mmoja asiyejua athari ya Ukimwi, tunaona watu kila siku wanakufa hii athari ya ukimwi inajulikana.

Mhe. Waziri lakini nikuulize juu ya mipango yote aliyojiandaa jinsi ya kuzungumza huku akisema kuna hatari zaidi jinsi ya kuepushwa virusi vya Ukimwi amesema kuna wanaume kwa wanaume ambao wanafanya njia za mapenzi, je amejiandaa vipi kuondosha hasa vile vianzio vya Ukimwi, mara nyingi tunapiga kelele vianzio vya ukimwi kuna Mabaa hebu tuondoshewe haya.

Mhe. Mwenyekiti nakumbuka kwamba alisema jamii iorodheshe na iende kupeleka malalamiko yao kwamba pahala gani pana baa, mimi napendekeza kwamba tusingoje kuwa Ndijani kuna baa watoke watu wa Ndijani waje waseme kwamba ile baa tuondolewe, mimi ningaliomba kuwe na tume makusudi ya kuchunguza wapi pana baa mimi nasema hayafai hasa haya mabaa kuwekwa mitaani. Nasema mabaa hayafai kuwekwa mitaani wakati jamii imeshindwa serikali ndio baba yetu itushughulikie masuala haya. Mhe. Mwenyekiti kutokana na hali ilivyo tutamalizika sote kwa Ukimwi hii ni hatari tunaomba vianzio vya Ukimwi vishughulikiwe.

Juzi katika hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais waliochangia walisema hapa wanawake wanakwenda uchi, kweli wanawake wanakwenda uchi leo unamkuta mtoto wa kike kavaa *jeans*, sheria gani iliyohalalalisha mwanamke avae suruali hakuna sheria, Kwa hivyo tukasema kwanza mzazi awe na jukumu la kumzuia mtoto wake asivae *jeans* huyo mzazi anavaa *jeans* ataweza kumuelimisha mtoto wake? Hapa tunaomba serikali itie mkono wake na kama tunataka kuliondoa hili kwa serikali ni jambo jepesi.

Juzi tu palikuwa na ma-*helmet* yaliyokuwa hayatakiwi yakaletwa ma-*helmet* mengine, mbona watu wote wanavaa ma-*helmet* yanayotakiwa sasa hivi. Kwa sababu lile suala limetiliwa nguvu, vi-*helmet* vya vikapelo havitakiwi, japo watu wanaumia wanasema masikio hawasikii, lakini kwa mujibu wa mkakati uliochukuliwa kila mtu anavaa *helmet* lile. Sasa leo isiwezekane vipi kuona mwanamke anapita njiani amevaa nguo zisizostahiki asiweze kudhibitiwa mwanamke yule. Bado serikali ina jukumu na haijataka kuondoa masuala haya. Kwa hivyo, tunaomba na tunaikabidhi serikali sasa wazazi wameshindwa na hili, tunaomba Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, hili ni moja ambalo linachangia wanawake kwenda uchi na hili nalo tusaidiwe kwa mavazi yasiyostahiki kwa mwanamke wachukuliwe sheria. Mwanamke yeyote asionekane kavaa suruali hata ikiwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa sababu mtoto anafuata kichogo cha mzee wake, kwa hivyo,

watasema hata hao viongozi wanavaa masuruali. Kwa hivyo na hili Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri litizamwe kwa upana wake.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nakwenda katika suala la madawa ya kulevya ambayo yako sambamba haya katika janga la taifa letu. Mhe. Mwenyekiti, mimi hujiuliza katika kichwa changu, hivi kweli madawa ya kulevya yanaweza kumalizika katika nchi yetu? Namuomba Mhe. Waziri aje atueleze mkakati upi madhubuti atakaouchukua hata ionekane kwamba madawa ya kulevya hayaingizwi katika nchi yetu.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, siku moja niliangalia televisheni nikaona kipindi cha mchezo wa kuigiza, bosi kakaa kwenye kiti chake anawapigia simu polisi anawaambia leo nendeni bandari fulani kutaingizwa mzigo mbaya, halafu yeye anawapigia simu watu wake wenye kuleta madawa ya kulevya kuwambia piteni bandari fulani. Kwa hivyo, polisi wanakwenda bandari hii huku na mzigo unapitishwa bandari nyengine.

Wafanyakazi wake wale wanakuja ofisini wanaleta mzigo bosi ndiye mwenye dhamana ya madawa yale. Sasa mimi nikajiuliza katika hali kama hii ikiwa ipo Zanzibar njia gani itaweza kutumika tuondokane na uingizaji wa madawa ya kulevya?

Mimi nasema kwamba, bado serikali haijawa tayari kudhibiti madawa ya kulevya kuingia kwake hapa, na kama tuko tayari kwa miaka kumi sasa hivi tunapiga kelele, miaka mitano iliyopita yote limepigiwa kelele juu ya udhibiti wa uingiaji wa madawa ya kulevya bado haijapatikana *solution* ya kudhibiti madawa hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema siku moja unapotaka kumuuwa panya lazima uzibe mashimo, utakapoyaziba mashimo yote tayari utamuuwa panya kwa urahisi hana tena shimo atakaloingia. Kwa hivyo leo tunataka kudhibiti uvutaji wa madawa ya kulevya bado uingizwaji unatokea, hata tuwapaleke katika viwanda gani hao wakirudi ikiwa wataelimika basi ni kumi na kuna wengine chipukizi watakuja wanainuka nayo wanakula madawa, tutapata wapi manusura? Kwa hivyo, ningeliioma serikali, nimuombe Mhe. Waziri, kwa suala hili jamani hebu tuwe *serious*, tukubali hasa kwamba hili suala linatuumiza na tunataka kuliondosha, hapo tutaliondosha.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu nije katika Idara ya Watu wenye Ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, tunavyotakiwa wakati wowote binadamu tujiandae na mambo matatu, jambo la kwanza tujiandae na mautiu, jambo la pili tujiandae na umahatuti na jambo la tatu tujiandae na ulemavu. Kwa hivyo, ni suala ambalo naweza kusema limetuzunguka, kuna ulemavu wa kuzaliwa na

ulemavu wa kukuta. Kwa hiyo, tumeelezwa katika ukurasa wa 15 hapa, anasema kwamba kuna changamoto zinazowakuta walemavu ikiwemo unyanyasaji unaofanywa na waendesha daladala.

Hili ni kweli Mhe. Mwenyekiti, wenye ulemavu wanapata manyanyaso makubwa katika daladala. Mimi napenda kumuuliza Mhe. Waziri, ni vipi atakaa na Waziri wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na madereva wa daladala ili kuzungumza juu ya changamoto hii inayowakuta walemavu kuwasaidia, mbali na matangazo kutoa kwenye redio. Kwa sababu mtu unapomkabili jambo uso kwa uso ukazungumza naye ukampa athari yake, ukamueleza matatizo yake ni bora, pengine kwenye redio au televisheni ata hasikii aje aambiwe tu, leo watu wa daladala mmetolewa taarifa mnawanyanyasa walemavu. Kwa hivyo, mimi nahisi Mhe. Waziri suala hili akae na Mhe. Waziri wa Miundombinu pamoja na madereva wa daladala na tingo wao kuzungumzia suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa mchango wangu huo mdogo sehemu nyingi zimeshachangiwa naomba niishie hapo nisije nikarejea hayo kwa hayo, kwa sababu mambo ya mazingira yameshachangiwa sana bora nikatishe mchango wangu na ninanunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili niseme machache katika bajeti hii ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mhe. Waziri Bi Fatma kwa umahiri wake na uwelewa katika kufanya shughuli hizi ambazo mimi nilizani zitamhangaisha kidogo kwa sababu ni mgeni wa haya mambo, lakini naona anaweza vizuri.

Lakini la pili nimpe pole, kwa sababu majukumu haya aliyokabidhiwa ni mazito sana na tunaweza tukayaita ni moja katika majanga yanayotuathiri katika nchi yetu. Kwa hivyo, mtu akipewa kushughulikia majanga huwa kapewa kazi nzito. Sasa mimi nampa pole lakini namuombea Mwenyezi Mungu ampe *toufiq* ya kuyaweza mambo haya.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 25 Mhe. Waziri katueleza majukumu ya Idara ya Mazingira na naomba niyataje mbio mbio. Imesema ni ‘kukusanya na kuhifadhi taarifa za kimazingira, kutoa taarifa za kimazingira ili ziweze kusaidia katika kutayarisha na kutekeleza mipango ya maendeleo, kufuatilia mwenendo wa hali ya mazingira ndani ya nje ya visiwa vyetu pamoja na kuandaa utafiti wa kimazingira.

Lakini pia kukabiliana na matatizo ya kimazingira". Sasa haya ni mambo makubwa na kwa mtazamo wangu yangehitaji fungu kubwa la fedha. Kwa sababu ni mambo mazito yanahitaji utafiti na mambo mengine, lakini kapewa shilingi 239 milioni tu, tena kwa mambo yote haya, mishahara umo umo, miradi umo umo.

Sasa kwa maoni yangu mimi hili fungu ni dogo sana labda halafu Mhe. Waziri aje atwambie kama anataka kufanikisha yote haya aliyoyaelekeza humu basi afanye ile *area location* ambayo Mhe. Omar Ali Shehe haipendi hata kidogo. Lakini katika uhalisia wake hizi pesa ni ndogo sana na si dhani kama zitamsaidia sana katika kufanikisha haya malengo ambayo kayaandika humu. Hilo moja.

Nataka sasa nielekee moja kwa moja kwenye uchimbaji wa matofali. Mhe. Mwenyekiti, pale niliposema pakewa kazi nzito basi moja inabainika hapa. Kwa sababu ukiangalia uchimbaji wa matofali una hasara kubwa lakini pia una faida kubwa, mimi nilifika pahali nikawa naumiza kichwa sana hivi kweli kuzuia wananchi wasichimbe matofali itawezekana? Kwa sababu mtu akichimba tofali maana yake kapata ajira, ajira ambayo inamsaidia yeye kujiendesha na familia yake. Lakini kwa upande wa pili kumewasaidia wananchi kupata malighafi ya kujengea jambo ambalo ni kitu kizuri, lakini kuchimba matofali kuna hasara kubwa kwa sababu yanaweka athari ya mashimo makubwa. Sasa katika kukabiliana na hili kwa kweli kunahitaji hekima na busara ya hali ya juu.

Siku moja Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais alikwenda katika maeneo yale ambayo watu wanachimba matofali, kilichotangulia kuelezwa ni kwamba Mhe. Makamo wa Kwanza anakwenda kuwapiga marufuku watu wasichimbe matofali, basi Mhe. Mwenyekiti wale wahusika walichukua familia zao wakasema leo tunamsubiri Makamo akija hapa tumwambie kama tusichimbe matofali basi hawa watoto awachukue yeye aende akawalishe. Kwa maana ya kwamba ni ajira ambayo wameitegemea.

Sasa mimi nadhani nitoe rai kwa wachimba matofali na wachimbaji wa mchanga pia. Kule Pemba mazingira ya kile kisiwa tuna mali nyingi kule, miongoni mwa mali tulizonazo ni milima, kuna milima kule ambayo imekaa tu na wala haitumiki, nafikiri mingine ukiiondoa ni njia moja ya kuleta maendeleo. Kwa sababu kuna barabara zinapita kwenye milima kule, kama tungeikata ile milima basi tungepata urahisi wa kupitisha barabara nzuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri njia mbadala watu waachiwe wachimbe matofali lakini waambiwe kile kipato wanachokipata basi kuwe na tozo maalum kama ni asilimia 10 au ngapi, lakini iwe inakaa kwenye Mfuko wa Mazingira na

hatimaye Idara ya Mazingira itumie fedha zile na nyengine ambazo watazipata kwa wahisani wetu wa maendeleo wakakata ile milima wakafukie mle mwenye mashimo, lakini wasiwazuie watu kuchimba matofali. Katika machimbo ya mchanga hivyo hivyo, huo ni utaratibu unawezekana.

Jambo jengine katika mazingira Mhe. Mwenyekiti, ni ukataji wa miti ovyo. Pia kwa upande mwengine huwezi kuwaambia watu wasikate miti, kwa sababu kuna wajenzi humu mtu akijenga lazima apate milango, madirisha na uwezo wa kutumia milango ile ya *aluminium* wananchi wetu hawawezi ile ni ghali, lazima apate mbao. Sasa ukishamwambia fundi seremala asitengeneze mbao watu watakaa kwenye majumba yasiokuwa na milango. Mimi nadhani kuwe na uratibu mzuri, mtu aruhusiwe kukata mti pengine kuna mvule na mingine anataka kukata ilimradi apate mbao akafanyie shughuli zake, lakini asikate ule mti kwanza mpaka awe amepanda mti mwengine kama ule, tena awe keshaupanda.

Kwa mfano, mti huu nakusudia mwakani niukate basi mwaka mmoja kabla apande mtu na aushughulikie, Idara ya Mazingira ikija iridhike kama huu mti sasa una mwelekeo wa kuja juu ndio apate ruhusa ya kukata. Lakini ukimwambie asikate hilo halitawezekana.

Kuhusu ile misumeno Mhe. Mwenyekiti, ile ni hatari sana, kwa sababu ni njia rahisi kweli kweli ya kumaliza miti. Mti unaoweza kuukata wewe wiki nzima hujaumaliza mtu mwenye msumeno ule anaweza kuukata kwa nusu saa akasafisha kila kitu, sasa ni hatari. Ila nayo katika kuipiga marufuku basi tuchukue hadhari kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja nilikuwa Chake-Chake pale baadae nikaamua kurudi nyumbani, nilipofika njiani kuna jiti la mvinje kubwa limeanguka limekata kwenye barabara sawasawa. Kwa hivyo, gari zinazotoka Mkoani hazina pa kupita wala zinazotoka Chake-Chake kwenda Mkoani haziendi. Wakatafuta mtu mwenye msumeno ule wa mashine na walimuagizia mbali, lakini kwa sababu ana simu akapigiwa simu akafunga msumengo wake kwenye baskeli akakimbia nusu saa keshafika pale, alitumia kama robo saa gari zikaweza kupita. Sasa hiyo ni faida moja kubwa.

Mimi nadhani Idara hii ya Mazingira pamoja na Idara ya Misitu misumeno ile isipigwe marufuku lakini iwekewe udhibiti, kwamba mtu asiutumie mpaka hii Idara kama ni ya Misitu au ya Mazingira au wote wawili lakini wawe wanajua kwamba mtu anachukua msumeno anakwenda pahala fulani kukata mti fulani kwa madhumuni fulani na kibali kiwe kimetolewa. Lakini ukisema unapiga marufuku ile siku moja barabara zitakujakuwa hazipitiki.

Mhe. Mwenyekiti, jammbo jengine ambalo linatuathiri sana ni watu wanaopiga mkaa kwa kutumia misitu hii. Kule kwetu kuna eneo la ukanda wa pwani kulikuwa na msitu wa mkoko mwingi sana, lakini sasa hivi ukienda inaweza kutoka machozi hakuna hata ujiti mmoja. Sasa katika hili naomba Mhe. Waziri awe mkali sana na ikiwezekana awe na usimamizi maalum wa kuhakikisha. Kwa sababu mikoko ile ukiikata unayapa nafasi maji ya kumega sehemu ya nchi kavu sasa, jambo ambalo kwa visi wa vyetu ni hatari mno. Kwa hivyo, haya yanahitaji yapate usimamizi wa hali ya juu.

Nafikiri nikitoka kwenye Idara ya Mazingira niingie kwenye madawa ya kulevya, Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya. Mhe. Mwenyekiti, katika hili naunga na serikali kuendelea na ule ushaur nasaha wanaowapa watu wanaotumia madawa ya kulevya. Wale wanaojidunga sindano na kula kuwapa ushauri nasaha ni jambo zuri, lakini nadhani serikali iweze kudhibiti kwa kutumia rungu ya dola kidogo, kwa sababu binadamu ndio binadamu, ikiwa Mwenyezi Mungu aliyemuumba mwanadamu kamuumbia moto seuze wewe binadamu mwenzake utamshauri atakusikia? Kwa sababu kama ushauri unasikilizwa basi Mwenyezi Mungu asingeumba moto ingetosha ile *Quraan* kutoa ushauri na ina ushauri mzuri. Lakini pamoja na ushauri ulio ndani ya *Quraan* Mwenyezi Mungu kaumba moto kwa ajili ya kumdhibiti binadamu.

Sasa ushauri nasaha pekee hautasaidia, lakini nadhani ilikuwa itumike sheria, iandaliwe na ifanyiwe marekebisho na kwa kweli watakaopatikana na kadhia hii ya kutumia madawa ya kulevya waadhibiwe tena waadhibiwe hasa.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak pale alisema kumuazibu yule anayevuta ukawa hujamchukulia hatua yule anayeleta hiyo ni kazi bure. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani mkazo mkubwa zaidi na kwa kweli mimi nachelewa kusema ni aibu lakini naona tabu sana kwamba kinchi kidogo kama hiki watu wawe wanaingiza madawa ya kulevya humu wakati tuna asakari waliotuzidi kipimo. Tuna vikosi vitano vya serikali na vyote ni vikosi vya ulinzi na usalama. Tuna Jeshi la Polisi, Jeshi la Ulinzi, tuna Askari wa Usalama wa Taifa, hivi kweli mtu anaweza kuingiza madawa ya kulevya humu akawa hakamatwi?

Mhe. Mwenyekiti, hili mimi linanipa wasi wasi mkubwa na nina wasiwasi katika hili basi ukisikia duniani kuna rushwa, rushwa inatumika hapa, hawa wanaonekana. Mhe. Mwenyekiti, wanaoleta madawa ya kulevya wanajulikana na wanaonekana, lakini inaonekana pana rushwa iliyopindukia mipaka wanaachiwa wafanye hivyo, na kama wanaachiwa kwa sababu ya maslahi binafsi, kwa sababu rushwa ni maslahi binafsi, anipe pesa nitie mfukoni nimuachie afanye shughuli zake maisha halikomi hili. Sasa nilikuwa nadhani

kila mmoja ajiangalie mwenyewe, je hahusiki? *Otherwise* kwa kweli tutakuwa tukipiga kelele kila siku lakini jawabu haitopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, kabla hujanambia kama bado dakika mbili nataka nizungumze madawa ya kulevya na vyuo vya mafunzo. Mimi nilikuweko kule Chuo cha Mafunzo kwa muda wa siku 17. Mhe. Mwenyekiti nilikuwa naona mambo mengi na moja katika mambo niliyoyaona niliwaona wale wafungwa labda hapa wanaitwa wanafunzi lakini mimi nawaita wafungwa. Wale wafungwa wanasaidiwa kuvuta bangi na wale askari wa Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kile chumba ambacho mimi nilikuwemo siku moja kaletwa mahabusu mmoja alipoletwa kwanza ile kambi nzima ya jela ilishangilia nikauliza mimi kaja rais hapa? Kumbe kaingia mhalizu sugu, alipofika kwa bahati nzuri akaja kwenye kile chumba changu, kawavulia wenzake viatu vya raba akawaambia hivyo hapo toeni humo, ilitolewa bangi ndani ya viatu vya raba haipungui nusu kilo, walitoa halafu akawaambia bado imo, nikashangaa sana, sasa nikasema haya bangi hii itafanywa nini? Itavutwa yote humu?

Mhe. Mwenyekiti, usiku anakuja askari wa jela anagonga mlango, ile milango ya zile selo ina vidirisha, wanapenyeza mikono analeta pesa anachukua bangi anakwenda kusambaza kwenye vyumba vyengine, nimeyaona kwa macho yangu haya. Sasa ikiwa Askari wa Jela wanafanya kazi hiyo na yule aliyekamatwa kapelekwa kule kakamatwa kwa sababu nje alikuwa akivuta bangi hivyo kweli ndio tunafanya tiba hivyo? Sasa nataka kusema kwamba, kama serikali haijatoa mafunzo na kuwadhibiti askari wa jela kwanza basi tusihangaike bure kuchukua watu wanaovuta bangi mitaani tukawapeleka kule tukasema tunakwenda kuwafundisha tabia hawafundishiki na wale wengine ambao hawavuti basi nao watavuta.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, ni kuhusu UKIMWI. Mhe. Mwenyekiti nimetishika sana na kitabu hiki cha Mhe. Waziri kwamba pahali palipo na asilimia kubwa zaidi ya maambukizi ya ukimwi ni jela. Katueleza hapa Mhe. Waziri katika ukurasa wa 17, ukisoma kifungu cha 42 mwanzo mwanzo pale utaona kuna 2.8 ya wale wanafunzi wa jela walioko kule wanambukizana ukimwi. Sasa haya ni mazingira hatarishi na tumekuwa tukipiga kelele sana hapa, moja ni sababu hii ya kutumia madawa ya kulevya kule.

Lakini (b) hakuna uhifadhi mzuri. Wale wafungwa hawadhibitiwi vizuri kule jela, wengine wanatoka wakisambaza ukimwi kwa wenzao. Tulikwenda pale Kilimani kuna watoto wadogo masikini wamewekwa ndani kule hawahifadhiwi Mhe. Mwenyekiti, haya mababe huku yanatoka yakenda kule. Jambo hili tumelisemea sana mpaka siku moja Mhe. Zahra alisema mpaka akalia ndani ya

Baraza, lakini bado hali hairidhishi. Sasa nadhani Mhe. Waziri halimgusi yeye moja kwa moja kwa sababu ni wizara nyengine, lakini huyo waziri wa wizara nyengine humu yumo nafikiri hili ni jambo la kulitilia mkazo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini nadhani ushauri nilioutoa kuhusu machimbo ya matofali uzingatiwe vizuri. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa kidogo ya kuchangia bajeti ya Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Mengi najua yameshasemwa yanayohusiana na Ukimwi, Ulemavu na Mazingira, lakini bibi yangu aliniambia kama unataka kupiga ndizi mbivu na kutaka ikolee utamu basi kidogo uongeze chumvi.

Mhe. Mwenyekiti, wengi tumezungumzia suala la mazingira na hili hivi sasa limekuwa ni jambo la ulimwengu kwa ujumla na sisi hapa petu tumo katika wanaofuata mikataba ambayo inatulazimisha kufuata masuala fulani yakiwemo ya mazingira. Ninachotaka kukisema hapa ni kwamba hili ni suala geni kwetu ambalo wenzetu wamelianza zamani na katika kuanza kwao wameshajitayarisha, baadae wakalileta kwetu na sisi tuanze kuliandaa ili tufanye hiyo *globalization* yaani tuweko pamoja.

Sasa athari zake ni nyingi sana kama alivyosema somu yangu aliyetangulia, kwamba kuna hasara na faida. Katika hasara zake ni kwamba sisi ni moja katika sehemu yetu ya kupatia wananchi wetu ajira, kuna wananchi wengi ambao wanajishughulisha na kupiga mkaa, kuna wananchi wanajishughulisha na kukata miti pamoja na kuchimba mawe.

Hawa wote ukiwaangalia kipato chao kinategemea moja kwa moja na maisha yao kutokana na kazi hizo, sasa tukienda tu moja kwa moja tukisema leo wewe msumeno wako usiufanyie kazi tunamtia katika umasikini mkubwa mwananchi yule.

Sasa kwa vile serikali ina nia nzuri na wizara imeshajipanga kwamba inataka kutekeleza majukumu yake kisawasawa, basi naomba wangeiga ule utaratibu ambao unafanywa na Wiara ya Miundombinu na Mawasiliano, kwamba wao wanapotaka kujenga barabara au kuitanua wanalipa fidia.

Nakusudia na hapa Mhe. Mwenyekiti, yule mtu ambaye anaonekana ana msumeno yeye keshajenga kwamba mimi huu ndi utakaonipatia maisha, kwa hivyo ili kumfanya asiendelee na shughuli ile na ili tusije tukapigishana mbio misituni usiku, bali na yeye msumeno wake tuuchukue baadae tumpatie fidia ili akafanye shughuli nyengine.

Sammbamba na hilo, nakuja kidogo kwenye Madawa ya Kulevya. Mhe. Mwenyekiti, madawa ya kulevya pia nayo ni tatizo linalotokana na huko huko kwa wenzetu. Wao wamejipanga vizuri katika vituo vingi sana wanakuwa wana vitu vya kuangalia jinsi gani mtu huyu kabeba madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano mdogo tu kwamba juzi kuna taarifa kwamba Wazanzibari wenzetu wamekamatwa Japan na wamefungwa miaka 16 wakiwa wamebeba madawa ya kulevya. Sasa wao wameweza kufikia hatua hiyo lakini sijui sisi kwamba tumejiandaa na vyombo ambavyo vitaturuhusu kuweza kutambua kwamba huyu ana dawa fulani, au huyu kachukua kitu fulani. Hayo ndio mambo ya kuangalia kabla ya kusema tu kwamba sisi tunataka tudhibiti madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, ninachokijua mimi ni kwamba hivi sasa chanzo kimoja cha kitakachoweza kutufikisha kujua nani analeta madawa tunacho kwa sababu wanaotumia madawa haya wapo. Kama wapo kuna vyombo mbali mbali hivi vya usalama wa taifa ambavyo vinaweza kutambua kupitia hawa hawa wananchi ambao tunawachukua tukawapeleka *Sober House.* Badala ya kutumia pesa zetu kwa ajili ya kuwalisha hawa labda kwanza tungewapeleka jela, baada ya kutoka jela ndio tukawapeleka *Sober House* wakapata mafunzo na sheria ndivyo inavyosema.

Sasa kwa kupitia vyombo hivi basi nahisi tungelipata taarifa sahihi za nani au vipi madawa haya yanaingia katika nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, hili ni suala la serikali kama tulivyosema kwamba serikali yetu tunaitegemea mara hii itakuwa ina umakini wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbusha tu kwamba kuna mshairi mmoja katika nchi ya Uingereza kulikuwa kuna tatizo la kujua nani mhusika wa mauaji, lakini mwisho wa suluhisho lake alisema *"To be or not to be that is the question".* Kwa hiyo, hapa petu hili ndio tatizo tulilonalo kuwa au kutokuwa. Hili ni tatizo dogo sana na mwaka unaofuata ningeiona bajeti ikitumia pesa ndogo sana kwa ajili ya hawa wenye madawa ya kulevya. Kwa sababu ikiwa atatumia zile mbinu au yale malengo aliyoyaweka ya kudhibiti haya madawa basi moja kwa moja tunaweza tukawaondoa. Lakini sio hivyo, matokeo yake leo tunasema tu kwamba tunataka tudhibiti madawa ya kulevya. Wanaotumia si wapo kwa nini wale wasikamatwe wakatupa vyanzo vya nani analeta na njia zipi zinatumika kuleta madawa.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo, nakwenda kidogo kwenye Ukimwi. Mhe. Mwenyekiti, ukimwi upo zamani hapa na unaendelea sijui kama unakua au unapungua. Tukiiangalia Bajeti ya Wizara inasema kwamba mwaka 2010/2011

walitumia karibu shilingi milioni 440, lakini kuna mikakati mingi ambayo waliiandaa wakiwa na nia ya kupunguza tatizo hili. Ni imani yangu kwamba kutokana na mikakati ile pesa hizi zilizotumika zilipunguza angalau idadi fulani.

Lakini mwaka huu wameomba tena shilingi milioni 472, kwa hiyo hii inamaanisha kwamba katika pesa zile walizotumia matokeo yake hayakuwa mazuri. Kwa hiyo, ningeliwaomba tena kwamba ikiwa mwaka uliopita kuna mikakati fulani waliyoifanya haikufanikiwa sasa mara hii waandae mikakati mingine. Nategemea kuwaona kwamba mwaka 2012/2013 wasije tena katika Baraza hili wakaomba milioni 472 au zaidi kwa ajili ya kushughulikia matatizo ya ukimwi. Ni matarajio yangu kwamba matatizo haya yatashughulikiwa mwaka huu na kumalizikia mwaka huu huu. Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru lakini nitakuomba radhi sitosimama. Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kutujaalia tukawa jioni hii tumeshirikiana pamoja sote na ikawa tuko salama. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na wewe uliyenipa nafasi katika kiti chako, Mwenyezi Mungu akujaalie twende salama. Pia nampongeza Mhe. Waziri halafu nampa pole.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Watu wenye Ulemavu usije kuona kuwa umetupwa mzigo leo lakini huu mzigo uko zamani sana. Mzigo huu ulianzia hapa hapa, mwiba uchomeapo ndiko utokeako.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Watu wenye Ulemavu siku hizo ilikuwa ni jumuiya, mwaka 1984 ndio tulipoanza kuunda, mwaka 1985 tayari tukapata usajili. Mhe. Mwenyekiti, kadi yangu ya mwanzo mimi nilichukua Afisi ya Waziri Kiongozi na Waziri Kiongozi alikuwa ni Mhe. Seif Sharif Hamad. Leo imerudi hapa hapa lakini nina kilio kikubwa katika Idara ya Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Watu wenye Ulemavu nitaanzia Pemba. Kuanzia miaka hiyo mpaka kufika hapa tulikuwa tuna wahisani mbali mbali, serikali kutusaidia misaada ya ndani na nje. Lakini nathubutu kusema ofisi Pemba mpaka leo hakuna. Iikuwa ni nyumba ya kukodi, hakuna usafiri, fedha ikipatikana wenzetu wanajenga maofisi, wananunua magari, Idara ya Watu wenye Ulemavu Pemba ni dhalili mno. Hivi sasa jengo wanalokaa limeshamaliza muda wake mwenye jengo anataka jengo lake. Jengo linakodiwa kwa mwaka milioni moja wataipata wapi watu wenye ulemavu. Wanaambiwa wafadhili wameshanawa wajitegemee.

Mhe. Mwenyekiti, kilio changu cha pili kuweza kupunguzwa watu wenye ulemavu katika idara. Pale tukenda sisi katika ofisi yetu mfanyakazi ni mmoja huyu wa pili ni msaidizi watu wote wameondolewa kuambiwa hawana kitu cha kulipa ni jambo la kusikitisha.

Sasa hapa sisi tuliunda jumuiya kwa pamoja na tukafanya idara hii kwa pamoja. Mhe. Mwenyekiti, linalonisikitisha tukija Makao Makuu tuna kumbi za mikutano, tuna maofisi, tuna magari tunatembelea, lakini kule shughuli zao watu hawa wana matatizo sana. Hawana gari na hata wakipata ile gari ya kukodi wanaambiwa mfuko wa kupata pesa za kutia mafuta pia hakuna. Wana shida sana walemavu Pemba za kuweza kushajihisha watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa kwenye Kamati ya Ushajihishaji Makao Makuu, Mwenyekiti wetu alikuwa Bi. Zulekha aliyekuwa mbunge zamani. Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa na kigari kimoja tu tukipakizana humo tukenda kila pahala Makangale na kwengineko kufanya ushajihishaji wa watu wenye ulemavu. Lakini mpaka sasa Mhe. Mwenyekiti, mafanikio Pemba ni madogo sana ya watu wenye ulemavu na wamekata tamaa. Wamekata tamaa kwa sababu linalotokea lolote linamalizia upande mmoja, upande mmoja ni malalamiko.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikenda wenzangu wanasikitika sana, mimi ndio kichuguu chao sasa hivi. Hata hiyo ofisi kama ulisikia mara moja matangazo anaambiwa mwakilishi ajenge ofisi ya walemavu Pemba. Sina nyumba ya kulala nitajenga ofisi, ni matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, halafu tukija kwenye huu ushajihishaji sasa hivi hakuna mlemavu yeyote tunakwenda kwa hiyo hali ngumu, lakini kuwaita na wakakufuata wanakwambia msile mapesa yenu huko sisi mkaja mkatudanganya. Kwa sababu hata ukiitazama kamati basi watu wakichaguliwa wengi wanatoka upande mmoja kuliko upande mwengine wa pili, watu wamevunjika tamaa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ana kazi kubwa ya kuweza kutushajihisha na nakuombea kheri *inshaallah* Mwenyezi Mungu mwanamke mwenzangu atakuwezesha.

Mhe. Mwenyekiti, tukija kwenye unyanyasaji hawa wananyanyaswa kwa mambo yote sio kwenye magari tu, hata barabarani. Mhe. Mwenyekiti, mimi nathubutu kusimamisha gari kugombana na watu. Mtoto ni mlemavu wa akili anaambiwa tuimbie ucheze tukupe shilingi mia. Wewe unajisahau kuwa umeumbwa. Wewe Mwenyezi Mungu kukubadilisha ni mara moja. Mhe.

Mwenyekiti, mambo haya ni makubwa mno na serikali iweze kusimama kidete kuwashughulikia watu kama hawa.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza letu lililomaliza mimi nilisema hata hili Baraza la Taifa hapa nilimwambia mimi Mhe. Waziri Kiongozi ndio tulipokuwa sisi wakati huo, nilimwambia Baraza hili haliko halali. Kwa sababu Baraza lililoundwa la Kitaifa la Watu wenye Ulemavu Mpemba hamna. Mna Mpemba lakini yupo hapa Unguja toka ana miaka minane mpaka kishakonga sijui atatusaidia vipi kule kama hakutolewa mtu kule na akaingia kwenye Baraza lile. Nilimwambia mimi Mhe. Waziri Kiongozi.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, tuna kilio kikubwa cha watu wenye ulemavu hata maskulini. Mara moja mimi nilichangia vile vile nikawaambia jamani watu wenye ulemavu skuli ni watu wa kunyenyekewa na kuweza kutoa taaluma kwa kuweza kuwa karibu nao.

Mhe. Mwenyekiti, mtoto mwenye ulemavu wa akili ikiwa hajasindikizwa kwenda skuli basi akija mwenyewe ataingia saa tatu, lakini akifika yule mpokee na umuweke pahala pazuri umfundishe yale yale mafundishaji yake. Mtoto huyu akishakuwa hakubali anataka akupige wewe tu lakini yeye hataki kupigwa, akipigwa skuli anakimbia. Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mhe. Waziri aweze kusimamia mpaka maskulini kwenye watoto hawa.

Mhe. Mwenyekiti, pia hawa watoto wenye ulemavu naona lilitoka tangazo kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali aliyemaliza muda wake watoto hawa wasilipishwe skuli. Mhe. Mwenyekiti, nashangaa sana siku zote naitwa mimi mwakilishi skuli zilizo karibu watoto hawa nikawagomboe. Mama yake ni maskini, baba yake ni maskini hana kazi yoyote ada inamshinda, anaambiwa usije kama hujaleta malipo. Jamani tutalipa mpaka tufike wapi, ina maana mawaziri wetu wakitoa kauli hazifuatwi. Nitakuja kusema zaidi siku ya bajeti ya Wizara ya Elimu.

Mhe. Mwenyekiti, watu wenye ulemavu ni watu wanaotaka watazamwe kwa hekima nzito kuanzia jamii mpaka majirani, aliyekuwa hana mtoto mlemavu basi atakapomuona mtoto mlemavu amuone kama ni wake kwa sababu watoto hawa wapo kila aina. Kuna watoto hawaoni, kuna watoto hawana akili, kuna walemavu wa viungo na mambo mengine na hawa ndio wanaohujumiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano mimi mwenyewe nimemshuhudia mtu kwa macho kumkamata mtoto mwenye ulemavu, nikauliza nikaambiwa leo siku ya mwanzo. Haya siku ile aliyopelekwa kushtakiwa naambiwa kesi ilipelekwa mara ya kwanza na mara ya pili akaachiliwa na hakomi. Alimpa ujauzito na mtoto yule ni mlemavu, baba yake ni mlemavu, mama ni mzima, hujazidisha

mzigo kwa mtu mwenye ulemavu. Jamani serikali ione sio mtu huyu akifika aachiwe kuwa mzee wake aje pale anajiweza atoe chochote aachiliwe, hivyo ndio ilivyokuwa. Ni mtoto wa nani muachilieni, haiwezekani mharibifu ni mharibifu tu.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba serikali ituone kupitia waziri wetu mwanamke hili lionekane, tuna idhilali ngumu, tuna idhilali nzito sana. Kutumwa ovyo ovyo watoto hawa waliokuwa akili zao ni taahira tunathubutu kugombana na watu majumbani, anaoneshwa kigori anaambiwa huyu ndie mkeo nichangie kuni. Kutwa na magogo mtoto huyu anataka kuchanja eti anataka kupewa mke. Jamani kama ni mtoto wako wewe unaweza. Maana usimfanyie mtoto wa mwenzio jifikirie wewe kama mimi ni mwanangu naweza kumfanyia. Mhe. Mwenyekiti, hayo ni mambo ya yanayotokea mitaani.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala la Ukimwi. Mhe. Mwenyekiti, hawa watoto wenye ulemavu na wao huu ukimwi wanapata kwa sababu wanabakwa na watu tusiowajua. Tukiwapeleka hospitali tunaambiwa huyu ameshatibiwa mchukue hatupati takwimu sahihi ya watoto hawa. Tunaomba serikali iwe makini tutakapowapeleka watoto hawa hospitali kwanza tunasema huyu mtoto mlemavu yaondolewe hasa haya malipo yawe hayapo. Kwa sababu siku nyengine mtoto ni mlemavu na mzazi ni mlemavu na hawezi kazi yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru sana katika vikundi tumeshajihishwa sana tumefanyiwa kila kitu cha kupata hivi vikundi lakini vikundi hivi soko hatuna. Walemavu wana vikundi aina kwa aina, wenzetu hawa wa *ZANAB* kazi zao ni ma-*dormet* na vikoba vyengine na mambo mengine hawana soko. Ukija kwenye walemavu wa viungo wanasuka mikili, wanapakasa, wanafanya mikeka lakini hakuna soko, ina maana hawa wote vitu wanafanya lakini lile linalokusudiwa haliwezekani, wamo kwenye vikundi vyao lakini havizalishi.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, wamesema hapa kuwa wanapita katika hizi shehia na wilaya mpaka katika majimbo. Kwa upande wa Pemba naona bado na katika hichi kitabu sikuona hasa kama wametiwa watu wa Pemba kuwa wamepitiwa kukaguliwa au kupewa mafunzo yoyote. Sasa na kule kuna walemavu wengi sana tunaomba ikiwa huu ushajihishaji umeshaanza kuanzia awamu ya upande mmoja na kule yapelekwe mafunzo ili watu wajue wanafanya nini na haya mafunzo waweze na wao kupatiwa ili kuweza kujisajili.

Mhe. Mwenyekiti, nikikueleza walemavu tutafika kutwa maana sitamaliza. Mlemavu anaambiwa aende kwenye semina Wete anatoka kijiji kwake mfano meli nzima au meli moja na nusu hapana gari lakini akifika analipwa shilingi elfu mbili zimsaidie nini. Hii hali halisi ilivyo, mimi mwenyewe nimeshahudhuria semina mbali mbali unapewa shilingi elfu mbili na ukifika

pale pale unaambiwa kadi yako umekuja nayo ina deni linakatwa lile pengine urudi na nauli tu utakayopandia gari.

Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mhe. Waziri aweze kutusimamia na litakapotokezea suala hili watu wote wapate haki zao, ikiwa wa kupewa shilingi elfu kumi basi apewe ile ile, sio zitoke kwenye mkono wa huyu zije za mkono wa huyu akifika na yeye achukue huyu amdhalilishe.

Mhe. Mwenyekiti, halafu tuna watu wenye ulemavu wa akili hawezi huyu kutoka peke yake lazima apelekwe pengine na mzazi wake au apewe mtoto mwenziwe aliyekuwa mzima wa akili kumpeleka. Tunaomba huyu akimpeleka nae alipwe japo nusu ya zile atakazolipwa yule kwa sababu wanashinda kutwa pamoja kule. Wenyewe wanavyosema wakifanya semina mtie tu kwenye gari ateremshwe, nani anayeweza kumtia mwanawe aliyekuwa hana fahamu, hajui pa kuteremka, hajui chochote, haiwezekani.

Mhe. Mwenyekiti, watu wenye ulemavu tuna mtihani mzito kweli kweli kuanzia majiani, majumbani mpaka kwenye jamii, maana zimo jamii zilizokuwa wanawaadhibu watoto kama hawa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto wana jengo la watoto. Mhe. Mwenyekiti, naomba waziri wangu awezeshwe apewe kiwanja ajenge jumba wamo watoto wenye ulemavu na wazee wao hawajiwezi aweze kuwadhibiti hawa. Mhe. Mwenyekiti, watoto wenye ulemavu wanatanga ovyo ovyo, pengine mtoto huyu mzee wake hajiwezi maskini mchana kutwa anazurura macho yanamtoka, mafua yanamtoka, hajui kula, hajui chochote. Tunaomba mashirikiano mazito kuweza kusaidiwa jinsi ya kudhibiti hali iliopo ya unyanyasaji ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi kwa kuwa kitabu kimechangiwa sana sitaki niharibu mambo lakini naunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri mia kwa mia.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kutusomea kitabu hichi kinachoeleza mazingira, madawa ya kulevya, uchimbaji wa mchanga, kukata matofali, ukataji wa miti ovyo na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda kidogo kwenye mazingira. Mhe. Mwenyekiti, waheshimiwa wengi wameshazungumzia sana mazingira lakini mimi nitazungumzia mazingira ya mwanadamu kwa sababu hapa pamezungumzwa mazingira ya uchimbaji mchanga ili tutunze mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, bila ya kutazama mazingira ya kuchimba mchanga au kukata matofali lakini kwanza tumtazame mwanadamu mazingira yake. Kwa nini mwanadamu anakwenda kukata matofali au anakwenda kuchimba mchanga. Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ya Zanzibar wananchi wake wanategemea sehemu mbili tu, sehemu ya ardhi na sehemu ya bahari, hatuna viwanda.

Kwa mfano Jimbo langu la Matemwe lina watu si chini ya elfu kumi, watu hao ndani ya nyumba kila mmoja hakosi watoto wanane, huyo aliyekuwa hakuzaa sana watoto watatu. Sasa mtu huyu hana mradi wowote ila atumie bahari, hana mradi wowote ila atumie ardhi, ardhi yenyewe ni kulima na kukata mwitu apate kuni akauze, mwananchi huyu huyu aende akavue ili apate samaki aje ale. Sasa mwananchi huyu serikali haikumtazama mazingira gani aliyokuwa nayo na maisha yake yanakwenda vipi. Lakini anaambiwa tu usikate kuni wala usichimbe mchanga. Je, mwananchi huyu atafanya kazi gani.

Kwa hivyo, naiomba serikali tuwatazame wananchi mazingira yao kwanza yako vipi na maisha yao yako vipi na utajiri gani waliokuwa nao. Sasa hapa ndio tutampata mwananchi asichimbe mchanga au achimbe mchanga, kama hakuchimba mchanga kutwa nzima ile au usiku umeingia na kule kwetu watu saa kumi na mbili wameshalala. Je, kama hakwenda kuchimba mchanga au akakata kuni akenda akauza au akenda akavua hiyo bahari inayoambiwa kwamba uchafuzi wa mazingira, wapi atapata maisha yake kwenda mbele.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali iwatazame wananchi kwanza mazingira yao, iwatazame hali zao, wapi watawafanyia miradi yao halafu pale itungwe sheria ya kuhifadhi mazingira. Si hivyo, tutakuwa tunagombana na wananchi siku zote mazingira ikifika asubuhi hana pakwenda anakwenda kuchimba mchanga. Mhe. Mwenyekiti, natoa rai serikali iwatazame wananchi wanyonge wawafanyie mbinu mbadala ili maisha yao yaende mbele.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wameogelea sana katika madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, madawa ya kulevya ni sawa sawa na mpiga ngoma na mchezaji. Ngoma kama haijapigwa na mtu wachezaji hawachezi, atafutwe mpiga ngoma ndio mchezaji atacheza, lakini unamkamata mchezaji mpiga ngoma anapiga. Mhe. Mwenyekiti, madawa ya kulevya yanaletwa na watu wenye madaraka ndani ya serikali, madawa ya kulevya yanaletwa na watu wenye mapesa wenyeji katika nchi za Ulaya na kama hawakuzuiliwa hawa madawa ya kulevya Unguja hayaondoki.

Kama wenzangu walivyosema kwamba unamzuia mtumiaji wa madawa ya kulevya huyu mletaji unamfanya nini. Mhe. Mwenyekiti, sehemu zinazodhibiti madawa ya kulevya ni mbili, bandarini kwenye mameli na uwanja wa ndege.

Mhe. Mwenyekiti, hatuchimbi sisi hapa madawa ya kulevya, wala hatulimi madawa ya kulevya, kwa hivyo huku ndio kunakopita na huku ndio kunako wakubwa. Askari akishaambiwa hii mali ya mheshimiwa haikamati, ataikamata wapi, anapiga saluti pale anaambiwa pita. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, tudhibiti sehemu hizi.

UTARATIBU

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni zetu ziko wazi kwamba Mhe. Mwakilishi hatakiwi kusema maneno ya kudhania au ya kufikiria, au yaliyokuwa hayana uhakika. Kwa sababu huko nje kitu kikisemwa humu ndani kinachukuliwa kwamba kina ukweli kimesemwa katika chombo kikubwa.

Kwa hivyo, kusema kwamba kuna waheshimiwa waliomo ndani ya serikali wanaleta madawa ndani ya nchi na askari wanajua na wakiambiwa wanapiga saluti madawa yanapita. Hii nadhani ni tuhuma kubwa sana sio dhidi ya serikali tu lakini dhidi ya askari vile vile. Hiyo maana yake tumefika pahala serikali na nchi hii yote ni nchi ya kimafia. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Abdi Mosi Kombo ama athibitishe kauli hiyo au aondoe maneno hayo.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Mwenyekiti, binadamu anaweza akateleza kwa hivyo naondoa maneno yangu haya. Mhe. Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala la Ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi naishukuru na kuipongeza Wizara ya Afya, kwamba imeweka kila mwananchi wa Zanzibar aende akapime na wanapimwa. Naipongeza sana Wizara ya Afya kwa kuweka kitengo hiki cha kupimwa.

Pili, ili tuondoshe ukimwi kila mmoja awe ni mwalimu kwa kumsomesha mwenziwe. Halafu na sisi wazazi tuwe ni walimu wa kuwasomesha watoto wetu na kuwafunza watoto wetu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwa vile mchango huu umechangiwa na watu wengi sana na yanarejewa yale kwa yale. Lakini napenda tena kuishauri serikali ili tuweke mazingira safi, kwa hivyo serikali itoe ajira kwa wananchi hasa vijana ambao hivi sasa wapo wengi na hawana ajira. Sasa hivi kazi yetu ndio hiyo hiyo ya kuuza madagaa na kuchimba mchanga. Sasa ili tusalimike na tatizo hili Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, serikali ifanye mpango iwaajiri wananchi ili wananchi waondokane na matatizo ya maisha.

Kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, mimi napongeza tena Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kitabu chake hiki. Ninampongeza tena Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kutuletea kitabu hiki na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Matemwe nawaombea kwanza wapelekewe

vifaa vya kufanyia kazi, hasa vile vifaa vya baharini na vifaa vya kulimia ili wapunguze ukali wa maisha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe na mimi mwenyewe naunga mkono hotuba hii asilimia mia fil mia. *(Makofi).*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze katika Idara ya Mazingira ambapo idara hii ndio muhimu sana ya kuizungumza kwa sababu ina mambo mengi yanayohusu nchi hii na mwenendo mzima. Kwa hivyo, nashukuru kwamba iko sera ya mazingira ya mwaka 1992 kama itahitaji kidogo marekebisho ya sera hii ili kufuata mambo ambayo yamejitokeza mengi ya mazingira sio vibaya sera hii ikaanza kubadilishwa na kufuata mfumo mpya, kwa mujibu wa mambo ambayo yanatokezea.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la mazingira nataka niseme mambo mawili ambayo katika mazingira kuna kitu tunaita athari za mazingira. Kama kutatokea athari za mazingira basi ni lazima tuyatunze mazingira yale kutokana na athari ambazo zimetokea. Kwa hivyo, katika athari za mazingira mara nyingi kunatokezea kitu tunaita mmong'onyoko wa ardhi, hizo ni athari za kimazingira.

Kuna athari nyengine ambazo zinatokezea za sehemu za fukwe za pwani. Katika athari hizi mikono inakuwa miwili, ama ni za kimaumbile au zinasababishwa na binadamu. Kwa hivyo, kama tukisema mazingira haya ya uharibifu ya ufukwe wa bahari, inawezekana hata maji ya bahari yanaweza kutoa athari ya mazingira. Hii athari ya mazingira inatokana na mategemeo hasa kwa nchi zetu au visiwa vyetu, kama kule kwetu Pemba sehemu ya Kaskazini ya Pemba ambapo usawa wa bahari na ardhi uko sawa sawa. Kwa hivyo, unahitaji kufanywa kwa uangalifu kabisa maeneo kama yale ambayo tambarare ziko sawa sawa baina ya bahari na ardhi, inawezekana maji yakaingia ndani. Kwa Kaskazini mwa Pemba mara nyingi maji yanaingia ndani na matokezeo yake inapatikana uharibifu wa kilimo katika maeneo ambayo watu wanalima.

Kwa hivyo, hayo ni upande mmoja wa maumbile ambayo hayawezi kuzuilika. Lakini kwa upande wa pili unapatikana uharibifu wa mazingira kwa binadamu kuweza kukata mikoko ambayo ilioko pwani yakaruhusu maji kuweza kuingia na yakaharibu kilimo ambacho kinatarajiwa kulimwa na wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, athari nyengine ni ile ambayo kwa makusudi sisi binadamu tunakata miti. Siku zote tunafahamu tunapokata miti tunaleta uharibifu mkubwa. Kwanza tunaikimbiza mvua isinyeshe, pili mazingira yenyewe ya ardhi tunayaharibu kwa sababu yanakuwa yako wazi zaidi. Kwa hivyo, ukame unaweza kupatikana kutokana na kukata miti. Hayo yanasababishwa na sisi binadamu.

Athari nyengine Mhe. Mwenyekiti, ni ile ya mvua ambayo inanyesha, kwa kawaida mvua huwa inanyesha na inaleta uharibifu wa mazingira na mmong'onyoko wa ardhi. Hii haiwezi kuzuilika kwa sababu ni ya maumbile.

Vile vile kuna nyengine ambayo tunaisababisha sisi wenyewe binadamu, kama hii ya mifuko ambayo tumeshaiona athari yake, ambapo hii haileti mandhari nzuri na inaleta uchafu wan chi. Pia mifuko kama hii ikitupwa hata ikipigwa moto inaleta athari zake wala haiozi katika ardhi. Kwa hivyo, hicho ni kitu ambacho sisi hatutakiwi kukitumia, lakini sisi tunatumia. Sasa hapa ni juu ya waziri kutilia mkazo kwenye suala la mifuko hii ili ipigwe marufuku na badala yake tukatumia vitu vyengine ambavyo tukitumia baadae vinaoza.

Halafu kuna huu uchimbaji wa mchanga, utengenezaji wa matofali huo wote unasababisha uharibifu wa mazingira. Kitu kama mchanga ambao unachimbwa, mchanga sisi tunauhitajia, matofali tunayahitajia, mawe tunayahitajia na yote haya yanachimbwa katika ardhi. Sasa tufanye nini, mchanga lazima tuupate ili tupige matofali tujenge, mawe ni lazima tupate ili tujenge na matofali ndio kama haya yanatoka katika ardhi na ndio yanatusaidia kujenga. Hapa ni lazima utaratibu uangaliwe vizuri namna ya matumizi ya vitu kama hivi. Baada ya watu kutumia jee watu wafanye nini baadae.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengine ambayo yanajitokezea sio kwa binadamu lakini yanatokezea. Mimi nataka niseme kwamba hii mashariki ya Afrika ni *volcano*, angalia Kilimanjaro, angalia katika mito yote ambayo iko Tanganyika, kuna maziwa mbali mbali yote haya yanaingia kwenye *volcano*. Pia sisi hapa tulipo tumo katika *volcano*, *volcano* tunazo na athari ya *volcano* ikitokezea kule, sisi lazima itatufika. Angalia yale yaliyotokezea juzi. Hii haikutokezea juu ikaonekana wazi wazi lakini ilitokezea chini kwenye ardhi juu kuna maji lakini chini kuna ardhi. Angalia matokeo yake yaliotokea kule kwenye ardhi, basi athari zake tuliziona mjini Unguja, athari iliyojitokeza tumeona jengo ambalo lilikuwa ni la Wizara ya Kilimo limeathirika, na hii ni kwa manusura makubwa tu.

Niseme jengine ambalo muda mrefu tulipambana nalo katika ujenzi wa bandari ya Unguja. Kipindi kilichopita miaka ya nyuma bandari ile kwa siku za nyuma ilikuwa ni ya mvungu, baadae watu wakasema wajenge bandari ya tuta ambayo

ndio hii tuliyonayo hivi sasa. Mazungumzo yalikuwa ni makubwa ya kusema kwa nini tujenge bandari ya tuta tusijenge bandari ambayo maji yanaingia chini ya mvungu, kwa sababu ya mawimbi makali ambayo yanatokezea kule yanaweza kuleta athari ya bandari yetu.

Lakini wataalamu wakasema hayo mazungumzo waliyoyazungumza, tumeyasikia na tunayajua lakini sisi kwa utaalamu wetu tutajenga bandari ya tuta na athari isitokezee. Lakini angalia baada ya bandari kwishakujengwa, haidhuru ujenzi ulikuwa madhubuti, haujatokezea athari. Lakini angalia hii iliyotokezea juzi ambayo iliathiri kwenye sehemu ya pwani ambayo ni bandarini. Angalia jengo lile la Wizara ya Kilimo lilipata athari kidogo. Kwa hivyo, hatujui kwa hivi sasa pengine baadae yanaweza kutokezea hayo makubwa.

Kwa hivyo, ninachomshauri waziri hapa kwenye masuala ambayo yanapigiwa mfano mara kwa mara kuwa kuna masuala ya kuweza kuathiri mji mkuu wa Unguja, ambao Mji Mkongwe ndio unaoathirika. Sasa mimi ningemuomba waziri juhudi zake kubwa awe mwangalifu wa kujenga ukuta madhubuti wa *concrete* ambapo ukuta huu utaweza kuzuia athari zinazotokezea baharini. Nafikiri hizi Mhe. Waziri mwenyewe amekwishakuzifahamu.

Jengine ambalo nataka nilizungumzie Mhe. Mwenyekiti, ni hizi bidhaa chakavu ambazo zinaingia nchini mwetu. Sisi tulio ndani ndio tunasababisha haya, tunajua kwamba redio, TV na vyombo vyengine vyote vya anasa vina sumu kali sana. Nchi hii inakuwa ni jaa la kukusanya vitu kutoka nje tunaletewa sisi. Watu wameingia kwenye *digital*, kwa hivyo, sisi yale matumizi ya *analogue* ndiyo tunayoletewa sasa hivi. Tukumbuke tu kwamba kwa maelezo ya Mhe. Waziri wa Habari, mwala 2015 *analogue* inaondoka na tutaingia moja kwa moja katika *digital*. Je, hizi zana ambazo tunazo hivi sasa nyingi ambazo tunatumia *analogue* tutazipeleka wapi, itakuwa ni jaa kubwa ya kuweka mambo haya. Haya mambo yana sumu kali sana, tutayaweka kwenye ardhi hii, hiyo ni hasara kubwa.

Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri vitu ambavyo ni vichakavu na ni vitu ambavyo si vizuri, bora vipigwe marufuku visiingie katika nchi. Mimi ningemuomba Mhe. Waziri kama wakitokezea wafanyabiashara wanaleta vitu kama hivi, basi tuoneshwe katika TV vinakanyagwa kanyagwa, doza linapita linakanyaga ili kila mtu ajifunze kwamba hiki kitu hakitakiwi, tuoneshwe kwa mfano wa vitendo sio kwa mazungumzo ya maneno tu, tunataka mfano wa vitendo. Maneno mengi hayatotusaidia kitu tufanye kwa vitendo. Yaoneshwe kila mtu aone ili watu waogope kuleta vitu vichakavu.

Mhe. Mwenyekiti, tuingie katika mazingira mengine ambayo nataka kuyazungumza. Mazingira ya nchi kavu tumeshayaona namna hiyo. Sasa tuingie katika mazingira ya bahari. Mhe. Mwenyekiti, katika mazingira ya bahari sisi hatuwezi kuyaona mambo yote yanayotokezea katika bahari, lakini kuna watu wanakuja wakimwaga sumu ya vitu vyao kama hivyo tulivyovitaja sasa hivi katika bahari yetu, ambapo vitu hivyo vina sumu na sisi tuna samaki katika bahari yetu.

Mhe. Waziri tunakuomba uwe mwangalifu sana katika uchunguzi wa bahari kwa watu ambao wanakuja na zana za sumu kuja kumwaga katika bahari yetu. Kwa hivyo, vitu kama hivi sio rahisi kuweza kuviona kwa mkono. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri tuweze kupata kitu kinachoweza kutambua mambo yanayofanyika katika bahari, na yale mambo ambayo kwenye mtetemeko wa ardhi tuweze kuhakikisha kwamba vitu hivi tunapata taarifa mapema kabla tokeo halijatokezea. Suala hili ningemuomba Mhe. Waziri alifikirie vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengine ambayo yanafanyika katika ardhi, mambo hayo ni hiki kilimo tunachokifanya sisi binadamu, tunaweza kufanya athari kwenye kilimo. Kuna watu wanalima kwenye sehemu za juu ya mlima. Ukilima juu ya mlima kama huna utaalamu basi unaweza kuleta uharibifu wa mazingira, yaani mmong'onyoko wa ardhi.

Kuna jambo jengine ambalo tunalifanya sisi binadamu katika kuchafua mazingira. Mhe. Mwenyekiti, wanyama tunaowafunga pembezoni mwa milima au juu ya milima, vile vile wanyama wanaweza kuleta uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo, hayo yote nasema yanaweza kusababisha matatizo ya mazingira mabaya. Kwa hivyo, tunaweza kuchafua mazingira na vile vile tunaweza kuyatunza mazingira. Sisi wenyewe kama huu uchafu ulioko katika mji huu ni nani aje atusafishie. Yule anatupa uchafu na yule anatupa uchafu, ni sisi wenyewe wa kufanya haya.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante. Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka niende haraka haraka na mengine niyakate ni suala zima la ajira. Mhe. Mwenyekiti, ajira katika afisi hii inasimamia udhibiti wa bajeti pamoja na ajira za wananchi, haki pamoja na maslahi ya wafanyakazi. Kama ikiwa ofisi hii inaingia ndani kuangalia katika udhibiti wa serikali na vile vile inajikita kwenye ajira ambayo ni haki na maslahi ya wafanyakazi.

Mimi namuomba Mhe. Waziri katika suala hili, kwanza niseme suala la ajira. Ajira katika nchi hii ni ngumu sana, kazi hamna, maofisi yamejaa wafanyakazi na watu hawajui wende wapi. Lakini pamoja na kuwa hayo baadhi ya wakati

serikali inatoa nafasi kwa watu kupata ajira, ni jambo la kusikitisha serikali yetu hii ya Umoja wa Kitaifa ambayo tunasema ni *National Government*, tunakubali sote. Kwa nini ajira zinakwenda upande mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina malalamiko makubwa na nina masikitiko makubwa sana katika Wilaya ya Micheweni, ajira haziendi sawa, haki sawa kwa wote. Kwa hivyo, ajira zinakwenda upande mmoja ningemuomba Mhe. Waziri awe mwangalifu sana katika ajira ndogo ndogo ambazo zinatokezea katika serikali. Ajira katika Wilaya ya Micheweni zinakwenda vibaya.

Kwa mfano inatokezea kazi ya utiaji wa dawa katika majumba, hapa hatwendi sawa. Ajira iliyotokezea pale watu wamepiga kelele na sisi tumeletewa taarifa ile kwamba haki haikwenda sawa. Ningemuomba Mhe. Waziri katika ajira ndogo ndogo kama hizi zifuatiliwe. Hivi sasa pia kuna kazi nyengine zinatokezea zipo tayari na bado wanaambiwa wao nafasi hawana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kama anashughulikia kwenye suala hili basi ajaribu kuziangalia vizuri.

Suala la maslahi ya wafanyakazi Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Muda umekwisha Mhe. Mjumbe.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante namalizia Mhe. Mwenyekiti. Maslahi ya wafanyakazi kuna kilio cha muda mrefu. Inasemekana kwamba haki haikutendeka ipasavyo. Kwa mfano kwa kipindi hicho tunapigania kwamba tunamwambia afisi hii ya waziri huyo aweze kuishughulikia, kulikuwa kuna suala zima la *seniority* ya wafanyakazi, watu ambao waliofanyakazi muda mrefu, suala la *scheme of service*, suala la elimu ya Chuo Kikuu.

Mhe. Mwenyekiti, haya ni malalamiko ya muda mrefu kwamba mambo haya ya *seniority* hayakufanywa haki sawa, hawakupatikana wale watu ambao wameingia kazini muda mrefu wakajua mshahara wangu ni huu, basi anapitwa na mtu ambaye kaingia leo. Kwa hivyo, hapa haikuwekwa kwenye *consideration seniority*. *Scheme of service* zilikuwa hazipatikani baada ya miaka 10 ndio zinafanywa au miaka 20. Halafu na elimu ya vijana wetu ambayo ni *graduate* haki haikufanywa kwao. Mtu anamaliza miaka yake saba bado anapata mshahara mdogo. Kwa hivyo, kama ofisi yako inashughulika na mambo haya basi nakuomba sasa hivi afisi yako ni mpya na tunategemea wafanyakazi watapata mishahara mipya.

Kwa hivyo, naomba haya ambayo nimeyasema mimi uweze kuyapitia na kuona, je hapa haki imetendeka au haikutendeka. Mhe. Mwenyekiti, naheshimu sana wakati wako, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza

kuzungumza. Kwa hivyo, na mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia juu ya mia. Kwa niaba ya wananchi wenzangu nasema ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Tunamuomba Mhe. Hassan Hamad Omar, lakini atumie dakika 10.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa fursa hii kwa kuchangia angalau mambo mawili au matatu katika hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Utaratibu

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni kifungu cha 57(6) kinachohusu muda wa kuchangia kwa Waheshimiwa Wajumbe, kinaeleza kwamba naomba kunukuu:-

Kanuni ya 57(6) "Kila mjumbe anayejadili hoja ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 20 wakati wa mikutano ya kawaida na dakika 30 wakati wa mikutano ya bajeti. Lakini Spika, akiona inafaa anaweza kumuongeza msemaji sio zaidi ya dakika 10".

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti kwa kifungu hiki na sisi tunajadili bajeti na bajeti ndio uti wa mgongo wa taifa, na kwa sababu nashtuka zaidi kuona kuwa wizara muhimu kweli kweli ambazo sisi ndio tutakaojadili na kuzipitisha, basi zimepewa siku moja na nusu ni chache kabisa au zimepewa siku mbili. Kwa hivyo, hiki kitendo cha kuwa mheshimiwa atumie dakika 10 kinazidi kuniumiza zaidi.

Katibu wa Baraza: Mhe. Mwenyekiti, tunapenda kutoa ufafanuzi kwamba kanuni hiyo ya 57 ambayo Mhe. Mjumbe ameisoma, inakwenda sambamba na Kanuni ya 95. Kanuni ya 95 inasema:-

Kanuni ya 95 'Siku 35 za kazi zitawekwa kwa ajili ya Baraza kushughulikia makadirio ya matumizi ya mwaka ya kila wizara'.

Kwa hivyo, tangu tumeanza mpaka tutakapomaliza ni siku 35, na ndio maana wizara zote zikapangiwa ili ziweze kukidhi Kanuni hii ya 95 ambayo imeweka muda wa siku 35 za kazi. Ndio maana utakuta baadhi ya wizara zimepata siku moja, baadhi ya wizara zimepata siku moja na nusu kutokana na Kanuni hii nyengine ya 95.

Kwa hivyo, Kanuni zote mbili ile ya muda wa kuchangia na hii ya muda mzima wa bajeti zote kwa pamoja, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa kuongezea Waheshimiwa Wajumbe, tuna wajumbe ambao wanataka kuchangia hapa wanafikia 12. tukiangalia muda ambao Mhe. Mjumbe ulikuwa umeutaka, tutapata wachangiaji sio chini ya watatu au wanne na ukiangalia kwamba wote wana haja ya kuchangia. Ukiangalia na mchango unaokuja ni ule ule ambao tayari waliokuwa wameshachangia mwanzo wameuchangia.

Kwa hivyo, ndio maana tukasema kwamba ili kila mtu aweze kupata nafasi ya kuchangia basi tumsikilize yule anayetangulia anazungumza nini ili mwengine aweze kuja kubadilisha na sote tuweze kuchangia kama utaratibu unavyotaka. La kama tutasema tufuate Kanuni basi tupate hao wahusika wanne ili tuendelee na utaratibu, halafu baadae waendelee na mawaziri na wengine. Kwa hivyo uamuzi mnasemaje?

Waheshimiwa Wajumbe: Tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee, haya sawa.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, angalau mambo mawili au matatu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mambo mengi yamekwisha kuchangiwa, lakini kwa sababu tuko kazini, basi kuna haja ya kusisitiza mambo na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi naanzia katika suala la mazingira. Neno mazingira lina maana pana sana. Kuna mazingira ambayo ni usafi wa mazingira, suala hili namuomba Mhe. Waziri aliangalie kwa kina kwa sababu unafika wakati huu wa masika basi watu hushajihishwa sana katika suala la mazingira ya usafi, hasa katika kipindi cha mvua. Lakini utakuta kila Shehia ina kamati ya mazingira ya usafi, lakini ukiangalia wanaofanya usafi huo basi vitendea kazi hawana.

Tunamuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie kwa kina, hasa katika sehemu yangu ya Shehia ya Kojani na Shehia ya Mpambani kule tunahamasisha sana hili na kuweka mikutano, lakini ukija kuangalia wale wana kamati wanatuambia kuwa hatuna vitendea kazi yakiwamo mapauro, mareki na vyombo vyengine vya kufanyia usafi. Huku kuna mambo 17 ya malengo

yaliyoainishwa katika kitabu hiki, lakini halikuelezwa hilo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunaomba hilo ulizingatie kwa nguvu zote katika mambo ya usafi.

Hasa ukizingatia ziara ya Mhe. Rais wa Zanzibar alipotembelea katika mazingira ya usafi, alikuta ng'ombe na punda wanatembea ovyo katika mji wa Zanzibar. Hii nayo ni uharibifu wa mazingira. Ukipita katika barabara zote basi utawakuta ng'ombe wamelala barabarani na kuleta vinyesi, huu ni uharibifu wa mazingira nao.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili la mazingira kama nilivyosema kuwa lina maana pana. Vile vile ndani ya Jimbo langu la Kojani, kuna kiwanda cha kukaushia mipera pale Migurani. Lakini kiwanda hiki kimekuwa ni kero kwa wananchi wanaoishi sehemu zile kwa sababu kinawaathiri afya zao na wanalalamika sana. Kwa hivyo, kama kuna njia mbadala ya kukaushia mipera kwa njia ya umeme basi izingatiwe hivyo. Lakini wananchi wanapata tabu sana. Vile vile wanakata kuni kupita kiasi huo nao ni uharibifu wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye sehemu ya ulemavu, sehemu hii iko katika maeneo yote ya Zanzibar, ikiwemo vijijini. Lakini ukizingatia vijijini kunatupwa sana, kuna walemavu wengi ambao hawajaorodheshwa. Tunaomba walemavu walioko vijijini nao wafaidike na huduma kama walivyo walemavu wengine wa mjini. Walemavu hawa wanatakiwa kuishi kama binadamu wengine, kama tunavyoishi sisi ambao Mwenyezi Mungu hajatujaalia ulemavu huo, tunamuomba Mwenyezi Mungu atuepushie, hivyo wanataka kuenziwa kama wenzao wanavyoishi ili nao wajisikie kuwa wanaishi nchini kwao kwa raha mustarehe.

Mhe. Spika, nikija katika mambo ya ukimwi, kuna mambo mengi yanayochangia ukimwi. Kuna mengine tunaweza kuyadhibiti na mengine yako nje ya uwezo wetu. Haya yaliyokuwa ndani ya uwezo wetu basi tuyadhibiti. Kumekuwa na mtindo wa mavazi mabaya ya akinamama, sio akinamama peke yao pamoja na wanaume. Wanaume wanavaa suruali zinateremka chini linaathiri vazi alilovaa. Hili ni kero kubwa sana, tunaomba hawa wanaume nao wadhibitiwe katika mavazi wanayovaa. Hawa akinamama wanaleta mvuto mbaya ambao unaharibu mazingira, kwa hivyo mavazi hayo yenye kuharibu mazingira basi yadhibitiwe.

Hata vyombo vya habari navyo vinaleta matatizo. Katika vipindi vyengine vinachangia kuharibu, yaani vinakaribisha ukimwi. Zamani kulikuwa kuna utaratibu mzuri sana. Kulikuwa kuna vipindi vya watoto vile ikifika saa 1:30 basi mtoto haruhusiwi kutazama tena, nafikiri saa 1:30 au saa 12:00 ilikuwa hawaruhusiwi. Lakini siku hizi mtoto anaangalia TV mpaka saa 4:00 usiku, kuna mambo mabaya katika TV. Tunaomba mikakati ipangwe madhubuti ili

kuweza kuweka malezi mazuri ya watoto wetu na kupata taifa lenye afya njema.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu madawa ya kulevya, hizi ni kero kubwa sana na tunashuhudia sisi wenyewe. Wenzetu wanaovuta unga hawa wameenea sehemu zote za Zanzibar na kwengine kote, lakini tunawafikiria vijana hawa wanaovuta unga wanadungana sindano, mwisho mizizi ya kudungana sindano haipatikani mpaka mtu wanadungana katika sehemu zao za siri, hii ni athari kubwa sana. Mhe. Waziri tunaomba suala hili ulichukuwe na ulifanyie kazi ya kutosha, kwa sababu mambo haya tunayozungumza kama yatasimamiwa vizuri, basi wimbi hili litapungua lakini kama yatazungumzwa tu ndani ya Baraza basi hakuna mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya mambo manne niliyochangia, basi naunga mkono mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Kojani kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Allah Subuhanahu Wataala kunijaalia jioni hii kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwa kweli mimi binafsi nitakuwa na machache sana, kwa sababu wenzangu wengi tayari wameshazungumza mambo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza na mchango wangu katika hotuba hii kuhusu suala la mazingira. Katika maeneo ambayo yaliyoathirika zaidi na mazingira ya baharini kwenye Jimbo langu la Tumbe miongoni mwa Wadi mbili zifuatazo.

Wadi ya Kinoe kuna mabonde ya ukulima wa mpunga kama vile Kwamuhoro, Kwahashimu, Kwapape. Kwa hivyo, hili bonde la Kwapape hivi sasa serikali ina mpango kupitia *TASAF* kujengewa tuta katika sehemu hiyo, kwa sababu ni eneo moja ambalo ni kubwa limeshukuliwa na maji ya bahari.

Vile vile kuna mabonde mengine kama vile Kwamwinyiuziwa, Kwamzigua, bonde la Chwaka Mashariki Pemba, bonde la Kwamwanasoza na bonde la Kwamwanga Sizini. Mhe. Mwenyekiti, maeneo yote haya kwa kweli yameathirika na tayari yameshavamiwa na maji ya bahari. Kutokana na hali hiyo, wananchi wengi wa maeneo haya kipindi hiki mpunga wao wote umekufa kutokana na uchafuzi huo wa mazingira. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, chanzo ni kitu gani. Kwa kweli chanzo ni mambo mbali mbali moja wapo ikiwemo ukataji wa miti ya mikoko ambapo mabonde haya yako karibu na bahari.

Pamoja na hayo, Ukanda huu wa Mashariki kuna Mradi wa Uoteshaji wa Chumvi. Kutokana na mradi huu kuna maeneo mengi ambayo yamekatwa mikoko na wale waliofanya mradi huu hawakurejesha miti ile kwa kupanda upya.

Kwa hivyo, imekuwa ni tatizo sugu na maji ya bahari yamepata nafasi ya kuvamia maeneo mengine ya juu. Mhe. Mwenyekiti, licha ya chumvi ni sehemu moja ambayo wananchi wetu kupata ajira na kupunguza ugumu wa maisha. Pia ni tatizo kwa maji ya bahari yamepata nafasi ya kuja kuvamia maeneo yale ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, tunaiomba sana wizara hii kuliona suala hili na kulipa kipaumbele kabisa, ili wananchi wetu waweze kupata mashamba yao, kwani walio wengi ni wakulima kwa ajili ya kuweza kumudu maisha yao.

Vile vile nizungumzie kuhusu suala la Madawa ya Kulevya. Kwa kweli suala hili limeshapigiwa kelele sana na kama ni nyimbo, basi Wazanzibari wote wameshaipata na ikiwa ni mawaidha tayari watu wameshawaidhika. Lakini tukiangalia suala la Madawa ya Kulevya ndio kwanza linashamiri katika Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napatwa na mshangao mkubwa kinachochangia ni nini, kwa sababu hujiuliza hivi sheria zilizopo haziendi na wakati au utaratibu tulionao ni mbovu, kwa hiyo jawabu sipati. Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kuhakikisha kwamba wameweka utaratibu mwengine mpya na sheria iliyokuwa ni mpya ya kuweza kusimamia masuala haya. *(Makofi)*

Sasa ikiwa kila siku tunasema basi tutasema na hali ya nchi vijana watakuwa wanaendelea kupotea. Kwa hivyo, ni vyema serikali ikajipanga kama kweli wanayo azma ya kuondosha madawa haya, basi ni vyema serikali ijipange, ili kudhibiti maeneo ya viwanja vya ndege, bandari pamoja na bandari za ndani.

Mhe. Mwenyekiti, nahisi kwamba unapomuweka mtu kwenye maeneo ya kazi kwa muda mrefu kama vile miaka 25 au 30 yupo pale, basi hufanya ile kazi yeye ndiye mhusika mkuu, kwa hiyo anao uwezo wa kubadilisha mambo mbali mbali na wala hakuna yeyote wa kumkemea.

Kwa maana hiyo, naomba kuishauri serikali suala hili iliangalie sana, kwamba watu ambao wamo kwenye maeneo haya, basi wanakuwa wanafanya kama ni sehemu zao na wala hakuna mtu wa kuwaondosha. Sasa wakati atakapokuja mpya basi na utaratibu pia utakuwa ni mwengine, lakini tukiacha watu na

kusema wenye uzoefu pamoja na mambo mengine na hali ya nchi inazidi kuwa mbaya basin a watoto wetu watazidi kupata maangamizo.

Mhe. Mwenyekiti, niungane na wenzangu waliosema kwamba *Bars* zinachangia kwa asilimia mia moja suala la madawa ya kulevya, kwa sababu pale kazi yao ni ulevi na tumeshaambiwa kwamba mkuu wa maasi basi ni ulevi. Sasa kama ni ulevi na serikali inaona kwamba itapata mapato kwa ulevi basi pia serikali ijue itapata maangamizi ya vijana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ni vyema kuangalia faida na hasara, kwamba tukiona mapato ya *Bars* ni muhimu zaidi kuliko vijana wetu, basi sawa serikali iende huko, lakini vijana ndio rasilimali ya nchi. Kutokana na hali hiyo, naishauri sana serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ipime sana na tuhuwishe nchi, ili vijana wetu waje kuwa viongozi wa baadaye. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tukiliangalia suala zima la Maradhi ya UKIMWI ambalo limezungumzwa kwenye ukurasa wa 16 hadi 19 kweli Zanzibar sasa imefikwa na janga moja ni kubwa ambalo limeshakuwa ni donda ndugu. Kwa mfano, vyombo vya habari kila siku vinazungumzia kuhusu suala la UKIMWI, Baraza la Wawakilishi ni nyimbo tunaimba pamoja na taasisi nyengine mbali mbali, lakini tatizo hili ndio kwanza linashamiri. Sasa ikiwa kusema ni kusikika basi tayari tumeshasema.

Lakini nataka kuishauri serikali na wala si vibaya, ili kuinusuru nchi basi tukatumia utaratibu wa kuweza kuwatafuta ndugu zetu wa dini na kulisimamia suala hili, kwa ajili ya kuondosha UKIMWI Zanzibar. Kwa mfano, tukiangalia wakati dunia ilipopata Mtikisiko wa Kiuchumi, basi wameangalia mambo ya kidini na kupunguza riba zao, yaani wameweka taratibu za Kisheria za Kidini. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Baraza si vibaya ili kuinusuru nchi, basi suala hili la UKIMWI wakatafutwe watu wa dini na kuliendesha suala hili, ili kuwafanya vijana pamoja na nchi yetu itoke kwenye dimbwi hili kubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu muda wangu ni mfupi na wengine wanahitaji kuchangia, basi naomba kuunga mkono Bajeti hii ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa asilimia mia moja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii jioni ya leo kwa ajili ya kutoa mchango wangu mfupi katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, hotuba ambayo imewasilisha na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kwanza nianze na Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, jambo jema huigwa kwenye hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais iliandikwa kwa *pages* tatu na utaona hasa uongozi wa ofisi hii walijiandaa na kujua hasa wanafanya nini. *(Makofi)*

Kwa kweli wameeleza ofisi ilivyo, ziara za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, fedha zilizotengwa pamoja na faida ya ziara zake. Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya watu wa Kiwani nawapongeza sana wataalamu wa wizara hii na kweli wanajua wanachokifanya. *(Makofi)*

Lakini kwa masikitiko makubwa kama kwamba Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais haina Ofisi ya Faragha, maana yake kama kwamba mtu amelala na kuamka na tushtuka kuwa amesahau kitu. Kwa kweli wametuletea karatasi ambayo haijitoshelezi, yaani haielezi vipi ofisi hii wala mapato.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anieleze Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Ofisi ya Faragha atatumia fedha kiasi gani ambazo mimi sizioni kwa ile karatasi ambayo ametuletea. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, hii ni aibu na wala mimi siungi mkono utaratibu huu, kwa sababu uwajibikaji ni pamoja na kuweka mambo kitaalamu na ufanisi. Lakini karatasi hii labda kama mtu ameshtuka na kuambiwa umesahau kisu safari hii ya kwenda kula machungwa Jambiani, yaani ndio ilivyokuja karatasi, kwa sababu haielezi chochote na wala haifurahishi kwa utendaji mzuri wa serikali.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, Wake wa Viongozi siku zote hujenga taaswira nzuri katika, tumekuwa tukisikia Mke wa Mhe. Rais anavyoshajihisha wanawake kujenga nchi hii, pia tumekuwa tukimsikia Mke wa Makamu wa Pili wa Rais anavyozunguka nchi hapa katika kujenga wananchi, lakini hatujamsikia Mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais kuwashajihisha wanawake katika maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*
Nadhani sababu kubwa ni Ofisi ya Faragha na kama mambo ndio haya basi hakuna siku tutakayowasikia. Mhe. Mwenyekiti, Wake wa Viongozi wanayo sababu kubwa ya kujenga nchi na Wazanzibari wanafurahi sana kusikia Wake wa Viongozi wetu wakiwasaidia kwenye ujenzi wa taifa la Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje aniambie kwa nini hatumsikii Mama Awena katika kuwatetea Wazanzibari wa nchi hii hasa wanawake. Nafikiri ni tatizo la Ofisi ya Faragha. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi siwezi

kusema Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais anawivu, isipokuwa ni tatizo la fedha hazipo. Kwa hiyo, Mhe. Waziri atueleze tatizo nini na kwa nini Mama Awena hatumsiki akiwashajihisha Wazanzibari wanawake katika maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine kwenye Ofisi ya Faragha ni kuhusu safari ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Tumeelezwa kwamba Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais alifanya safari ya nchi za nje, kwamba alikwenda Uholanzi, Omar pamoja na nchi za Kiarabu. Sasa wakati aliporejea na mimi binafsi nilishiriki katika kumpokea, jambo moja ambalo alilizungumza ni udhaifu wa viongozi wa Wazanzibar kutembea nje bila ya kuwa na waandishi wa habari, jambo ambalo huwalazimu Makatibu wao kuwa ndio waandishi wa habari. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ninaiomba serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba iandae utaratibu wa makusudi kuwa viongozi wetu wakati wanapokwenda nje, basi waondoke na waandishi wa habari, ili yale wanayoyapata kule jamii ya Zanzibar ielewe nini wanachokifanya. *(Makofi)*

Suala jengine ni kuhusu Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Mhe. Mwenyekiti, nitoe masikitiko yangu kwamba idara hii nyeti imetengewa shilingi milioni 15 kwa ajili ya *other charges*. Idara hii nyeti ambayo inakusudiwa kufanya Mipango, Sera na Utafiti kwa shilingi milioni 15. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana Idara ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais angalau zipo shilingi milioni 100 ni wapi na wapi Mhe. Mwenyekiti. Hivi tunategemea mtaalamu huyu apange nini na kwa ajili ya nani kwa kiasi hicho cha fedha cha shilingi millioni 15.

Kwa kweli sijui idara hii imekosa nini na Mhe. Waziri naomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, anielimishe kwa nini fedha hizi zimepangwa kwa ajili ya idara hii muhimu ambayo inakusudiwa kufanya Mipango Sera na Utafiti. *(Makofi)*

Vile vile suala jengine ambalo ninataka kulizungumza na nimueleze Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kuwa mimi ni miongoni mwa watu wanaoishi katika maeneo ambayo yenye uharibifu mkubwa wa mazingira, kwa hili wala sioni aibu nasema kifua mbele kwamba watu wa Mwambwe pamoja na Jimbo zima la Kiwani wanaharibu mazingira. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hawaharibu kwa utashi, isipokuwa wanaharibu kwa matatizo ya umasikini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumchukuru Mhe. Rais wa Zanzibar pamoja na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kufanya ziara maalum kule Mwambe na walielezwa matatizo ya watu wa Mwambe, waliambiwa watu wa Mwambe watafute dawa, ili waache kuchimba matofali ya mawe, basi wewe unasemaje waliandika karatasi kwamba sisi tuko tayari kufukia mashimo na wala tusichimbe tena. *(Makofi)*

Lakini kwanza serikali isiharibu mazingira, kwa sababu asilimia 70 ya watu ya Mwambe mazingira yao yanaharibiwa na watu wa Idara ya Mawasiliano, kwani wao wanachimba kifusi pamoja na mawe na wala hawafukii, huku wakijua kwamba kila mradi anakuwa na asilimia 10 ya fidia na wala hatuioni. Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo walipendekeza watu wale ni kwamba wapatiwe mradi mbadala na serikali. ikaji-*commit* kwamba itafanya suala hilo.

Sasa leo naiona bajeti ya Mhe. Waziri kuna malengo zaidi ya tisa lakini hakuna hata shilingi moja. Mhe. Mwenyekiti, hii ni Kusadikika, yaani ni nchi iliyoangani, kwa sababu malengo haya saba ambayo yametengwa na Mhe. Waziri hayatekelezi, isipokuwa ni hadith tu na maandishi kwa ajili ya kufurahisha Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mazingira imetengewa shilingi millioni mia mbili na zaidi, lakini zote ni mshahara na matumizi ya kawaida na wala hakuna mradi wowote. Sasa leo utamwambia vipi mtu wa Mwambe afukie mtaro ule wakati wewe mwenyewe hujali kufukia mtaro. Kwa kweli mimi sitaki niwaambie watu Mwambe kwamba wanoe visu na mitaimbo kwa ajili ya kuchimba, lakini kwa mtaji huu hakuna.

Mhe. Mwenyekiti, nistahamilie nimalize dakika zangu mbili na niseme tu kwamba sitopitisha bajeti hii kwa kuziona fedha nyingi zimetengwa Tume ya UKIMWI na kuachwa Idara ya Mazingira. Mwambe sina takwimu lakini sidhani kama kuna watu wenye maradhi ya UKIMWI wanaofika sita, lakini watu wenye athari za mazingira ni asilimia 90. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti sioni busara kwamba niidhinishe shilingi milioni 2 kwa watu kupatiwa elimu ya UKIMWI na niache watu wa Mwambwe ambao wameathirika kwa mazingira.
Mhe. Mwenyekiti, Mwambe ina zaidi ya visima sita vya Chumvi kutokana na machimbo ya kifusi na mawe ya Idara ya UUB, sasa leo ukiniambia niidhinishe shilingi milioni 2 kwa ajili ya kutoa elimu ya UKIMWI tu. Mhe. Mwenyekiti, elimu ya UKIMWI imo ndani ya *Quraan* na wala tusihangaike kutafuta fedha tukala kwa kisingizio cha UKIMWI. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namheshimu sana Mhe. Waziri, lakini nitatoa shilingi ikiwa sikuona fedha zimetengwa kwa ajili ya mazingira na hususan Mwambe, Micheweni na Unguja sehemu ambazo zimeharibika. *(Makofi)*

Mwisho kabisa naomba nimalizie kwa kusema kwamba mimi ni mlemavu na kadi yangu ni 344, lakini serikali imekuwa na kawaida ya kuzungumza walemavu na Mhe. Raya Suleiman Hamad amesema hapa kwamba hatuioni jitihada ya serikali. Kwa mfano, jengo hili lilipojengwa walemavu walikuwa wapo na Mhe. Raya Suleiman Hamad alikuwepo Barazani, lakini wapi tumeweka kuwa Mhe. Raya Suleiman Hamad apande kama mlemavu labda pembeni sehemu ya kwenda kunywa chai. Kwa mfano, leo unamuona Mhe. Raya Suleiman Hamad amebebwa kwa kweli haipendezi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mipango ya serikali inayopangwa lazima izingatie maslahi ya walemavu. Kwa kweli walemavu ni watu na wengine wanazo akili kuliko watu ambao si walemavu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, pia naiheshimu sana Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini nitatoa shilingi ikiwa sikuona Idara ya Mazingira ikitengewa fedha. Kwa kweli nimeona kuwa safari za ndani, mafunzo pamoja na semina Wizara ya Fedha na Uchumi ni shilingi bilioni tano na Idara ya Mazingira ni *zero*. Kwa hiyo, hali hii haiwezekani na wala siungi mkono. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ambayo imebeba mambo mengi tena ni muhimu sana katika ulimwengu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na mambo mengine hayakuingizwa kwenye hotuba yake, lakini ndio mambo na tayari ameshazungumza Mhe. Mjumbe ambaye amemaliza kuchangia hivi punde. *(Makofi)*

Lakini niseme hii Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imebeba mambo ambayo ni ya ulimwengu na ni ofisi idara zake zinamgusa mtu mmoja mmoja. Kwa hivyo, niseme kwamba niungane na wenzangu kwamba imepewa fedha kidogo sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze mchango wangu kwa Watu Wenye Ulemavu. Kwa kweli tumshukuru Mwenyezi Mungu kuwa nchi yetu ni ndogo na watu wenye ulemavu hatujakuwa nao kwa wingi wa kusema watushinde.

Kwa hivyo, naomba sana Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais ikae itafakari na nimuunge mkono Mhe. Raya Suleiman Hamad kwamba ipite kila Shehia na kuhakikisha tunao walemavu wangapi tena wa aina gani, kwa sababu ulemavu uko wa aina nyingi, ili tuweze kuwasaidia, kwani na sisi miongoni mwetu tusijione leo tunakwenda bado hujesha kuumbwa mpaka siku yako ya kufa, yaani ukeshakutiwa kaburini pale huna ulemavu basi umshukuru Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niunge mkono kwa wenzangu waliozungumza pamoja na Mhe. Mjumbe aliyemalizia kuchangia, kwamba jengo hili wakati tunapitisha jengo la Baraza la Wawakilishi kujengwa jipya, tulizungumza kuhusu masuala ya walemavu. Sasa mimi nashangaa kwa nini haikutiwa sehemu ya walemavu na wala tusione leo na sisi miongoni mwetu na Mwenyezi Mungu atuepushie mbali, tunaweza kuja kuwa walemavu humu na watu wakashindwa.

Nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu Tume ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya na Kurekebisha Tabia. Mhe. Mwenyekiti, niungane na wenzangu kwamba kweli tume hii ni muhimu na mimi nasema huyu ambaye ametuletea madawa haya basi Mwenyezi Mungu amlaani na wanaoleta kuyaeneza pia Mwenyezi Mungu awalani, kwa sababu wametuharibia nguvu kazi ambazo tunazitarajia huko baadaye.

Kwa mfano, leo vijana wetu ukifanya mchezo hata mwanao uliomzaa basi anaweza kukukaba roho na kusahau kama ni mama kutokana na madawa haya ya kulevya. Kwa kweli naiomba sana serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba tudhibiti kwa sababu tunaambia hii ni nchi ya tatu ambayo inapita madawa ya kulevya hivi, bado hatujawa na utaratibu wa vyombo ambavyo kwa kweli vinaweza kusaidia madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu suala la Tume ya UKIMWI. Mwenyezi Mungu tunakuomba utusamehe, lakini hili ni janga kubwa sana ambalo limeingia katika dunia. Kwa kweli Tume hii nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mama Shadiya Karume ni mtu ambaye amesaidia sana katika janga hili. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naiomba Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, vile vitu ambavyo amesaidia Mama Shadiya basi viendelezwe na wala asiachiwe Mama Shadiya peke yake, viendelezwe kwa

sababu vimeshajihisha na vimesaidia sana. Kwa hivyo, naomba kuwe na mahusiano na vituo hivi. *(Makofi)*

Vile vile niunge mkono kwa hizi fedha ambazo tunazitoa na nyengine tunazosaidiwa zinapigwa kuni, yaani zinaliwa tukubali kwa ajili ya kufanyia semina za kila siku, safari nyingi. Mhe. Mwenyekiti, nadhani Ofisi hii iwe *alert* na fedha hizi za UKIMWI. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, ni vizuri tukawashajihisha wenye vikundi tukawatafutia miradi ambayo itaweza kuwasaidia hawa wenye Virusi vya UKIMWI na wala si vizuri tukawaacha hivi hivi, kwa sababu usimcheke mwenzako wakati wewe unao msururu kama si wa mjomba au shangazi ama wa babu. Kwa kweli haya ni majanga ambayo yameingia na wala tusichekane isipokuwa tuyadhibiti kwa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala la mazingira ambalo wenzangu wamezungumza sana. Kwa kweli suala hili itakuwa tunalipigia kelele kila siku, kwa sababu ni jambo ambalo linalohatarisha maisha ya visiwa hivi. Kwa mfano, ukija kwenye mazingira ya ufukwe, mazingira machafu haya ndiyo yamekithiri. *(Makofi)*

Kwa mfano, leo Maruhubi kumefanywa jaa ambako kuna shughuli za utalii, yaani magofu ya utalii na watalii wanashindwa kufika kule, hivyo limekuwa jaa ambalo ni aibu kubwa sana. Kwa hivyo, naiomba sana Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ishirikiane na wizara nyengine husuka kwa ajili ya kupanga mikakati na kuwasiliana kwa pamoja na mazingira yapewe kipaumbele, kwa kweli isiwe ni nyimbo ambayo tunaimba humu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sisi ndio tunaona huko na watu wengi au wananchi wanakuja na kutupigia hodi na kusema nyinyi Waheshimiwa gani mnaacha Mji hali kama hii, kwamba huku kuna hivi na kule kuna vile na wanatusikia kuwa tunawasemea.

Sasa kusema kwetu tusiwe tunasema kwenye *microphone* na hapa Barazani tu. Kwa hivyo, tuseme na vitendo vichukuliwe Mhe. Mwenyekiti. Nikimalizia niseme kwamba pamoja na yote naunga mkono hoja mia chini ya mia na nawaombea waongezwe fedha katika Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti kwanza naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Lakini la pili kwa sababu ndio mara yangu ya mwanzo kusimama na kuzungumza rasmi kwenye Baraza hili

naomba nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kunipa fursa na heshima ya kuwa Mwanasheria Mkuu na baadae nikaingia kwenye Baraza hili tukufu.

Kwenye sheria zamani tuliambiwa kwamba kabla hujasoma sheria usome *theology na medicine* ndio baadae unasoma sheria. Sasa nashukuru mimi humu ndani nitapata fursa ya kusoma yote hayo maana yake nimeona watu wa utabibu madaktari wamo, watu wa dini pia naona kuna mamufti wakubwa wakubwa.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hapo naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa matayarisho na umahiri wake katika kuwasilisha hii bajeti, mimi ningependa nizungumzie mambo mawili tu ambayo yamezungumzwa katika michango mbali mbali iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe.

La kwanza ni kuhusu mazingira hasa katika suala la mifuko ya plastic, Mhe. Mwenyekiti ni kweli katika eneo hili tuna tatizo pengine la kuona kwamba labda ilikuwa ni suala zaidi la serikali, mimi nadhani kwamba yaliyotokea yamethibitisha kwamba hili ni jambo ambalo lazima tulisimamie sote kwa pamoja. Kwa upande wa usimamizi nadhani moja tatizo lililokuwapo ni matatizo ya kisheria, sheria yetu bahati yenyewe sheria mama ile ya mazingira haikuwa imeeleza suala hili la mifuko ya plastic, lakini kwenye kanuni wakati wa kutungwa bahati mbaya jambo la kutengenezwa na binaadam ilichokataza ni kuingiza mifuko ya plastic na baadae kuwa nayo mifuko ya plastic, sasa ukitizama tafsiri ya kuingiza yaani *in put*.

Kwa mfano mifuko kama hii iliyokamatwa Bawe kisheria ilikuwa haijafika Zanzibar kwa sababu kufikishwa Zanzibar ni lazima uonyeshe uhusiano baina ya kile kilicholetwa na kuingizwa kwake Zanzibar, bahati mbaya kabla ya kutayarishwa hiyo operesheni hao watu walipokwenda kukamatwa kisheria.

Nasema mnapokwenda kwenye sheria inawezekana mtu kakosea ni muhalifu alikuwa na nia hiyo lakini anaweza kukutoa kwa sababu za kitaalam kwa kupitia sheria ilivyokuwa inaeleza, sasa nasema hilo ndio jambo moja ambalo tumekaa kulitafakari na kulirekebisha, ndio hivi vikao ambavyo vilikaa ilikuwa ni kurekebisha hilo ili mara nyengine litakapotokea tuwe na misingi madhubuti ya sheria ya kuweza kulisimamia.

Mimi niseme kwamba hata hizo hatua zilizochukuliwa naomba nimtoe wasi wasi Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kwamba hakuna mtu, kwanza kesi yenyewe haikuwahi kufunguliwa na hakuna mtu ambaye kwa kadri ninavyofahamu kwamba aliitoa mifuko hii kwa kificho, ilitolewa au ilirejeshwa kwa utaratibu na ikaondolewa nje ya Zanzibar chini ya usimamizi wa vyombo vya sheria.

Lakini jengine ni suala la madawa ya kulevya mimi naomba niungane na Mhe. Asha Bakari Makame kama kungekuwa na neno kubwa zaidi ya lana nadhani tungetumia hilo dhidi ya waingizaji wa madawa ya kulevya, kwa kweli hili ni janga ambalo kama hatukulikabili kwa pamoja litatufikisha pahala pabaya, lakini naomba niwakumbushe wenzangu tu kwamba kwanza tatizo la madawa ya kulevya halikuanza juzi na jana hapa kwetu. Sheria ya mwanzo iliyotungwa ya madawa ya kulevya kwa Zanzibar ilikuwa ni mwaka 1917 sheria namba 22 ya mwaka 1917, wakati huo wakiita kasumba wenyewe.

Sasa hii inaonyesha kwamba haya mambo ya kuramba ramba hivi vitu yalianza zamani na mwaka 1929 ikarekebishwa ikaitwa sheria ya madawa ya hatari, tokea miaka hiyo mwaka 1986 ndio tukatunga sheria ambayo iliimarisha usimamizi ambayo ilirekebishwa tena na mpaka juzi 2009 imetungwa sheria mpya nayo pia tunaifanyia mapitio, kwa sababu tunaona kuna mambo yanahitaji kufanyiwa marekebisho.

Kwa hivyo hivi ni vita ambavyo kwa kutumia sheria peke yake basi mimi nasema haitotusaidia sana, lakini nadhani tujue kwamba ni vita vya pamoja na vita vya kuweza kusimamia jambo hili kwa sababu sheria mpaka mtu umkamate unapokwenda Mahakamani tunajua kwamba sheria ni mambo ya mitego mitego unaweza kupeleka watu ishirini akafungwa mmoja.

Lakini pia jengine ambalo mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti ni kweli katika usimamizi wa mambo haya katika vyombo vya sheria ni kweli wapo ambao wana matatizo, kama ambavyo wamesema waheshimiwa lakini kwa ujumla binaadamu wako ambao wana matatizo kwa sababu isingewezekana kwamba mtu amkate binaadam mwenzake mkono kwa kuambiwa tu atapata utajiri, kwa sababu ya ubaya wa baadhi ya binaadam, au kumchuna mtu ngozi akiwa mzima kwa sababu tu ya kuahidiwa atapata utajiri. Kwa hivyo wapo ambao katika kupata utajiri hajali mtu gani ataangamia lakini mimi niseme kwamba katika vyombo hivi wapo watu ambao ni wazuri na wanafanya kazi kwa moyo na dhati kabisa.

Kwa hivyo tunapoyazungumza haya kwenye vyombo vya sheria mimi naomba tusifikirie sana kwamba kila mtu katika vyombo hivi vya sheria basi ni mbaya, mimi najua kwamba ndani ya polisi wapo ambao ni wazuri kuanzia Kamishna wa Polisi mwenyewe mimi nadhani tushukuru tumepata mtu ambae ana hisia na anafanya kazi kwa mapenzi yake na wako wasaidizi wake pia ni wazuri, mahodari wanafanya kazi. Kwa hivyo mimi nadhani tuwatie moyo pale ambapo wanafanya vizuri tuwasaidie katika hilo, lakini kwa kweli wapo watu wazuri na hayo madawa yanayokamatwa ni kwa sababu kuna watu wazuri ndani ya hao baadhi yao wabaya, lakini wapo wazuri wanafanya kazi kwa dhati na wameweza kukamata na kuzuia.

Kwa sababu hiyo hisia kwamba Zanzibar labda ni kituo cha madawa ya kulevya ilikuwepo kuna wakati tuliwahi kupata ujumbe kutoka jeshi la polisi la Holland wakidhani kwamba kuna kontena walifuatilia wakafikiria linakuja Zanzibar, lakini hata na wao kontena wameifuatilia kutoka Hong Kong ikapita vituo vyote mpaka wakaja kutua Zanzibar kwa sababu wameambiwa inakuja Zanzibar, lakini hata na wao wakapigwa chenga ya mwili ikateremshwa Mombasa. Sasa walipokuja kuangalia kwamba imeteremshwa Mombasa kama tuliwahi kusikia kwamba ilikamatwa kontena nzima ya madawa ya kulevya basi huko ilitoka ikiambiwa kwamba inakuja Zanzibar.

Kwa hivyo hiyo picha ya kujengwa kwamba Zanzibar yanaingizwa lakini kumbe ni katika mtando wa kupitia tu lakini pamoja na hayo mimi nasema bado kuna haja ya kushirikiana katika kuyasimamia mambo haya, hivi ni vita vya kwetu sote na mimi naomba kwamba mashirikiano na kuyasimamia katika ngazi tokea familia basi ndio jambo ambalo litatusaidia, lakini vyenginevyo kama tutaviachia vyombo vya sheria peke yake na serikali peke yake Mhe. Mwenyekiti, basi ndio hayo ninayosema kwamba sheria ya kusimamia mambo haya imeanza tokea mwaka 1917. Mimi ninachoomba Mhe. Mwenyekiti ni kwamba tujitahidi sote kwa pamoja kupiga vita mambo haya, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipa fura hii naomba kuunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsane sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii tena kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kwa kuanzia napenda nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba nzuri aliyosoma kwa ujasiri na kwakweli inatupa moyo wanawake tuliomo humu kwamba kweli sasa mambo yanaanza kwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba niunge mkono bajeti hii mia kwa mia kwa kuanza kabsa sijaanza kuchangia, mimi ningependa kuchangia sehemu mbili ambazo naona hazikuguswa watu wa Wizara ya Afya, kama kuna majanga makubwa yaliyoko katika Wizara hii ni mawili ya madawa ya kulevya na Ukimwi, haya yana mahusiano makubwa kiasi ambacho kama kutia moto katika petrol, moto ni tatizo na petrol ni tatizo na hasa vikikaa pamoja ni tatizo kubwa zaidi. Mhe. Mwenyekiti, madawa ya kulevya na ukimwi mwisho wake ni kifo na kifo cha watu ambao wako katika rika ambayo tunaitegemea katika maisha yetu kama nguvu kazi, madawa ya kulevya na Ukimwi yote yapo kuanzia miaka 15 mpaka miaka 35 kwa zaidi sio kwamba wakubwa zaidi hawafanyi isipokuwa hapo ndipo yalipo hayo.

Kwa upande wa Afya madawa ya Kulevya yanatuathiri kwa sababu watu wanapokwisha kutumia madawa ya kulevya hali zao zinakuwa mbaya,

kinachofuata wanachanganyikiwa kwa hivyo tunakuwa na mzigo mkubwa katika hospitali ya wagonjwa wa akili kuweza kuwasaidia watu hao, dawa nyingi inabidi zitumike kuwarudisha katika hali ya kawaida kabla hawajafanyiwa matatizo waliyokuwa nayo. Vifo vingi vinatokea na sasa hivi kwa sababu vijana wanakuwa wanatumia madawa ya kulevya zinawazidi nguvu na saa nyengine huku wanakofanyiwa wakiona hivyo wanaacha na vifo vinatokea wanakuja kugundulika baada ya muda.

Lakini sio hivyo tu Mkemia Mkuu nae ana dhamana yake kwa sababu vipimo vikubwa vyote vinafanyika huko kwa hivyo nae anapata mzigo wa kutosha, si hivyo tu watumiaji wa madawa ya kulevya wengi wao kwa kuwa wanatumia sindano wanaishia kuwa na virusi vya ukimwi kwa sababu wanachangia sindano. Kwa hivyo katika kitengo cha kulisha dawa za ukimwi nako pia kuna mzigo wa watu hawa.

Sasa tukiangalia kwenye upande wa ukimwi watu wa madawa ya kulevya kwa kuwa wanapata ukimwi kikubwa wanachotumia ni sindano, sio ukimwi tu lakini kuna na maradhi mengine pia yanapatikana kwa njia hiyo kwa hivyo kuna tatizo kubwa kwa hilo. Isitoshe ukimwi na madawa ya kulevya yanachangia kwa kiasi kikubwa hasa kuwakomesha *sex worker* kwa sababu *commotion sex worker* wengi shoga zao ni hao wanaotumia madawa ya kulevya, na mengine wanayafanya kwa sababu ya kuona haya kufanya uso wazi kwa hivyo wakitumia madawa ya kulevya kwa kiasi fulani inamsaidia kuondosha ile hisia aliyonayo na kuweza kufanya anachotaka bila ya kuona aibu.

Vile vile wanaotumia madawa ya kulevya wanapata matatizo kwa sababu anapohitaji daya ya kulevya kwa hali yoyote ile atafanya lolote lile, kwa hivyo wengi nao wanaingia katika vitendo vya kujamiiana wanaume kwa wanaume kwa sababu yeye nia yake ni kupata fedha apate dawa za kulevya, kwa hivyo yuko tayari kufanywa lolote au kufanya lolote. Lakini sio hivyo tu hao ambao wanatumia madawa ya kulevya ni waume zetu ni watoto wetu wanoweke wakishapata ukimwi wanakwenda kwa wake zao nao wanawaambukiza ukimwi, wakichukua mamba watoto zao wanawaambukiza ukimwi kwa hivyo imekuwa ni mtihani kwetu.

Sasa hili suala la kwamba liko chini ya Afisi ya Makamo wa Rais tu nafikiri yeye ndio dhamana lakini jukumu liko kwetu sote, kama serikali kama wana jamii ili tuweze kulivamia janga hili na kuona jinsi gani tutakavyoweza kuliondosha au kulipunguza kwa kiasi kikubwa, ndio maana kila idara kila Wizara watu walifanyie jitihada ili wafundishwe kwenye Mawizara kuna mitaala tofauti tofauti kwa ajili ya vyuo tofauti tofauti ingawa watu wengi wameyatumia hayo. Lakini ko ndiko elimu inakotakiwa ipelekwe ili tuweze

kupunguza hili janga ambalo lina mahusiano makubwa na Ukimwi na madawa ya kulevya.

Sio hivyo tu tunaotoa huduma tuko majumbani na mahospitalini kwa bahati mbaya tu shindano ikikuchoma basi wewe ujue uko katika hatari na wale akinamama wengi ambao ndio wanahudumia wagonjwa majumbani, kwa bahati mbaya kwa kutoelewa wanachokifanya kwa huruma zao na imani zao wengi wanaambukizwa maradhi ya ukimwi, matokeo yake unakuta kwamba takwimu za kinamama ni kubwa kuliko za kinababa. Kwa hivyo kinamama tuko katika hatari kubwa ya kuambukizwa ukimwi kutokana na maisha yetu tunayoishi.

Mhe. Mwenyekiti, wengi wamesema hapa maisha tunavyovaa, wanaume na wanawake lakini tuangalie kwanza kilichopo hapa ni kupunguza maambukizi ya ukimwi huko ndiko tunakotakiwa tuangalie, kilichopo hapa ni kuangalia njia gani tutapunguza madawa ya kulevya vimetajwa vyanzo mbali mbali tunavyofikiria. Lakini vyanzo kufikiria tu peke yake haitoshi tafiti ndizo zinazosema kwamba hili linasababisha na hili halisababishi, bila ya utafiti dhana tu au fikira zako hilo haliwezi kutufikisha kusema kwamba hili linasaidia. Kwa hivyo tuchukue tafiti kwa sababu hizo ndizo zenye uhakika wa kile kilichotendeka na wameangalia kwa nini wametafuta huku ili kuweza kusema kwamba hili linasababisha hili.

Kama kuvaa vibaya ulaya wanavaa vibaya kuliko sote na ukimwi hauko huko, kwa hivyo tuangalie vyanzo vya ukimwi tuangalie jinsi gani tutakavyoweza kuyapunguza maambukizi yasiendelee katika jemii yetu, tuangalie kitu gani kiatakachoweza kupunguza ukimwi na madawa ya kulevya, ili tupunguze maambukizi tumepewa fursa ya kupima, sehemu za kupimia ziko nyingi kwa hivyo twendeni tukapime na wale tunaowajua wana ukimwi wakapime.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wajumbe kabla ya kuahirisha kikao kuna tangazo hapa nimeletewa, tunaambiwa kwamba wawakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya Afrika ya Mashariki kwa Klabu Bingwa *Kagame Cup* 2011 *Zanzibar Ocean View* imeendeleza ushindi kwa mechi ya pili baada ya kuifunga timu ya *Red Sea* ya Ethiopia kwa magoli 2.0 katika uwanja wa Taifa Dar es Salaam *(Makofi)*

(Saa 1.45 Usiku Baraza liliahirisha mpaka
tarehe 28/6/2011 saa 3.00 asubuhi)